ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani

25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga

75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake
Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tano - Tarehe 13 Disemba, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamwita muuliza swali letu la mwanzo, napenda nikuarifuni kwamba wale Maofisa wa Tume ya Maadili ya Viongozi leo wapo hapa ofisini kutwa nzima. Kwa hiyo, kwa wale ambao watakuwa wameshakamilisha ule mchakato wa kujaza zile fomu mmoja mmoja anaweza akatoka kwa ajili ya kwenda kufanya marejesho kule. Na kwa wale ambao watakuwa hawajakamilisha basi watapewa mwongozo na hao hao maofisa wataweza kuwasaidia ili kukamilisha hilo zoezi. Baada ya hapo naomba sasa nimwite Mhe. Suleiman Sarahan Said ili aulize swali la mwanzo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, awali ya yote napenda niungane na nyinyi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma na mwenye kurehemu aliyeumba mbingu na ardhi na vilivyomo vyote. Na tumtakie kheri Mtume wetu Muhammad (SAW).

Mhe. Spika, naomba swali langu Nam. 100, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ lijibiwe.

Nam. 100

Mazingira Salama kwa Wafanyabiashara Ndogo Ndogo Chake Chake

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kuendeleza miji na maendeleo yake. Ktika mji wa Chake Chake ipo barabara iliyobuniwa ya kutoka Gombani Mwembe Karata kwenda Pondeani lakini barabara mpaka sasa bado haijakamilika kwa sababuya kuwepo kwa kiwanja cha mtu katika eneo la kutokea upande wa Pondeani.

a) Je, suala la kutomalizika kwa barabara hiyo ni kuwepo kwa kiwanja cha mtu ni kweli.
b) Je, Serikali inachukua hatua gani za gharura kuimaliza barabara hiyo ili kupunguza msongamano wa magari yanayokwenda Wete kutoka Wesha au yanatoka Wesha kwenda Wete bila kupitia kati kati ya mji wa Chake Chake.
c) Je, ni lini barabara hiyo itakamilika kwa matumizi rasmi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 100 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda nikiri kuwepo kwa mwananchi ambaye ameanza ujenzi wa nyumba ya kudumu katika eneo la ujenzi wa barabara hiyo kutokana na kudai kuwepo kwa kiwanja chake, na kupelekea kikwazo katika ujenzi wa barabara hiyo. Baraza la Mji la Chake Chake tayari limechukua hatua na kusitisha ujenzi katika kiwanja hicho, na kumtaka mhusika asiendelee na ujenzi huo ili kuruhusu ujenzi wa barabara hiyo uendelee ambapo taratibu za kumuondoa mwananchi huyo zinaendelea. Vile vile ofisi yetu itawasiliana na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ili kupata uthibitisho wa uhalali wa matumizi ya eneo hilo.

(b) Mhe. Spika, Serikali inaendelea na matayarisho ya ujenzi wa barabara hiyo ambapo kazi ya tathmini na makisio ya gharama za ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha kifusi imeshafanyika na kuwasilishwa Serikalini kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mazingatio na hatua zaidi. Kazi za ujenzi wa barabara hiyo zitafanyika mara tu baada ya kukamilika taratibu za upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini. Nimuombe Mhe. Mwakilishi aendelee kustahamili wakati Serikali ikiendelea kulifanyia kazi suala la ujenzi wa barabara hiyo.

(c) Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema katika jibu langu la (b) kwamba barabara hiyo itakamilika mara tu baada ya kukamilika kwa taratibu za upatikanaji wa fedha za ujenzi kutoka Serikalini na malipo ya fidia ya mali za wananchi akiwemo mwananchi aliyejenga katika eneo la barabara kuondolewa kwa mujibu wa Sheria.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nataka niseme barabara hii ambayo inatoka Gombani kuelekea Wesha ni barabara ambayo itakaa kwa muda mrefu kwa kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Inawezekana barabara hii imeshatumia pesa nyingi kwa kuanzwa halafu haimaliziki, na ni barabara muhimu ambayo inapunguza joto la msongamano wa barabara za Chake Chake na pia ni magari makubwa yanayobeba mafuta ambayo hayatopitia mjini yatakuwa yanakwenda Konde, Wete na maeneo mengine.

Kwa umuhimu wa barabara hii, pamoja na kusema unatafuta fedha. Ni bajeti gani barabara hii utaweza kuimaliza.

Lakini swali (b) ni nyumba hii ambayo ina maneno mengi kwamba muda mrefu sana inazungumziwa. Nyumba hii tatizo lake ni nini. Kama ni *compensation* au ni kitu gani, muda mrefu sana. Je, unasemaje kuhusu nyumba hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwenye eneo la nyumba naomba arejee Mhe. Mwakilishi nisikie vizuri.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nasema nyumba hii tokea wakati wa Mawasiliano inazungumzwa nyumba hii kwamba ipo kati kati ya barabara. Katika mazungumzo ambayo wengine wanasema ni kiwanja cha kwao cha asili, wengine wanasema ni kiwanja alichouziwa. Sasa Waziri unanambia nini kuhusu nyumba hii. Maana yake kama tatizo ni nyumba hii, basi ni tatizo dogo ama ni kulipwa au kuondoshwa kwa nguvu. Naomba jibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba kutoa majibu ya ziada kwa Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli suala la nyumba ambalo limezungumzwa ni ikwazo kwenye nyumba hii kama nilivyotanguliza kutoa majibu ya awali kwamba mmiliki wa eneo lile au mtu ambaye amejenga katika eneo lile tunachotaka kuangalia sisi kama Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, sisi hatuna mamlaka ya kutoa hati ya umiliki katika ardhi ile au katika eneo hilo ambalo linazungumziwa au linalolalamikiwa. Kubwa zaidi sisi tulitaka kuona kwamba mwananchi yule anaondoka katika eneo lile pale ili kusudi serikali iendelee na utaratibu wa kujenga barabara wananchi waondokane na usumbufu ambao upo katika eneo hilo.

Vile vile kuhusiana na ni kwa vipi. Kama nilivyosema kwamba tutafanya ufuatiliaji wa mawasiliano kati yetu sisi na wizara husika ili tuone kwamba yeye, huyu amekaa au kuna kizuizi katika hatua zipi katika kuona kwamba, pale ambapo itaonekana yeye ni mali yake nadhani hatua nyengine zitafuata ambazo nilisema masuala ya fidia hayapo katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Hapa sisi letu zaidi ni kumuondoa huyu mwananchi na sio kwamba labda kutakuwa na fedha za kuweza kujenga barabara hiyo kwa sababu barabara hii inaonekana kwamba ipo katika wizara husika ya Mawasiliano ambayo sisi mawasiliano haya tumejibu kupitia UUB.

Kwa hiyo, naomba niseme tu Mhe. Mwakilishi akubaliane na mimi kwamba sisi tunaendelea kufanya ufuatiliaji na wizara husika ili baadae tuone uhalali hasa na ndio maana tukasema hatua nyengine zitafuatia.

Nam. 102

Mazingira Salama kwa Wafanyabiashara Ndogo Ndogo Chake Chake

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuboresha miji yake. Lakini katika mji wa Chake Chake kwa sasa umekuwa na biashara ndogo ndogo maarufu wamachinga,

na kwa sasa hata barabara zote za mji zimekuwa hazipitiki na ni hatari kwa usalama wa wafanyabiashara hao na magari.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia eneo rasmi wafanyabiashara hao katika mji wa Chake Chake.
(b) Je, Serikali ina mpango gani hivi sasa kuwaweka wafanyabiashara hao katika mazingira salama kuliko kuwaachia kuzagaa kila mmoja sehemu yake na kuleta msongamano wa mji.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 102 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mhe. Spika, Serikali kupitia Baraza la Mji la Chake Chake linaendelea kulifanyia matengenezo eneo la soko la Michakaini kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo na wakubwa. Kwa sasa Ofisi ya Baraza la Mji la Chake Chake limeshajenga mabanda awili na kupeleka huduma ya maji na umeme na kutengeneza njia ya kuingia na kutoka katika soko hilo. Soko hilo litakapomalizika litawaondolea usumbufu wafanyabiashara wadogo wadogo pia kuweka Mji katika haiba yake.

(b)Mhe. Spika, kwa sasa wafanyabiashara wadogo wadogo wamewekwa eneo la mbele liliopo Hoteli ya Chake Chake na eneo la Jua Kali. Wafanyabiashara wa mitumba wamewekwa katika eneo la Chachani karibu kabisa na Maktaba Kuu. Mara tu baada ya kukamilika kwa ujenzi wa soko la Michakaini wafanyabiashara wote wakubwa na wadogo watahamishiwa katika soko hilo la Michakaini.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba Chake Chake ndio mji wa pili katika Zanzibar ambao unakua kwa kasi sana. Mhe. Spika, nataka nimhakikishie Mhe. Waziri kwamba mimi ndio Mwakilishi wa Jimbo lile na ninafahamu mwanzo mpaka chini na chanzo cha historia ya Chake Chake. Ninachokwambia hivi sasa kinachoendelea, Mji wa Chake Chake kuanzia Hoteli ya Chake Chake kuelekea mjini haipitiki kwa wafanyabiashara wadogo wadogo waliokaa juu ya mabaraza na chini ambapo yanapita magari ni hatari sana, gari itakapofeli basi itaua watu wengi sana na ndio njia kuu ya kuingia sokoni.

Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Waziri pamoja na kunambia wametengewa pahala, bado hawajatengewa maeneo kwa Chake Chake. Mhe. Spika, naomba watafutiwe pahala hawa wamachinga ambapo watakaa maeneo ya salama kwa sababu bado wamezagaa katika mji hata magari mjini hayawezi kupita.

Lakini (b) nilikuwa natoa kama rai. Mhe. Spika, Chake Chake sasa hivi pale mjini kuna masoko mawili, moja likiwa lile la Tibirinzi, jengine soko la juu lililopo. Kwa ukweli kama Mhe. Waziri atanikubalia kuna haja na soko la juu la mboga likahamishiwa chini,

na kama lile eneo bado litahitajika kwa muda mfupi basi wamachinga watatiwa mle ili kupunguza msongamano kwa muda huu.

Mhe. Spika: Ahsante, nafikiri yote sio maswali ni ushauri.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niipongeze wizara kwa kutafuta njia muafaka ya kuwaweka hawa wamachinga. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ameeleza kabisa kwamba wanawatengenezea Michakaini.

Mhe. Spika, inaonekana soko hilo la Michakaini ujenzi wake unasuasua sana. Je, Mhe. Waziri unaweza kutwambia ni kiasi gani cha fedha zimetumika toka ujenzi ule wa soko uanze hadi hii leo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wawi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba ujenzi ule *target* yetu ni kutumia milioni 80 kwa *phase* ya mwanzo. Lakini hadi sasa hivi tumeshatumia kiasi ya shilingi milioni 60 ambazo tumebakia kutumia milioni 20 ili kukamilisha kwa hatua ile ambayo tumekusudia kuitekeleza.

Nam. 17

Uongezaji wa Huduma za Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)*

Mhe. Mussa Foum Mussa – Aliuliza:-

Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)* ilitarajiwa kutumia jumla ya Tsh. 46.06 bilioni kwa ajili ya kufungua tawi katika Mkoa wa Dodoma, kuongeza vituo vya huduma katika maeneo ya Kigamboni na Tandika jijini Dar-es-Salaam, kuweka mashine za kutolea fedha *(ATM)* katika maeneo ya Kivunge, JKU Saateni, Paje, Chwaka na Mahakamani – Vuga kwa upande wa Unguja, na kwa upande wa Pemba mashine zinatarajiwa kuwekwa katika eneo la Micheweni, Machomane na Konde.

(a) Je, Mhe. Waziri kazi hiyo imeshaanza.

(b) Ni sehemu zipi zimeshakamilika uwekwaji wa huduma hizo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kujibu swali Nam. 17 la Mhe. Mwakilishi lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Kwa sehemu nyingi kazi hiyo imeshaanza.

1. Kwa upande wa kazi ya kuanzisha vituo vya huduma katika maeneo ya Kigamboni na Tandika Dar es Salaam na Tawi Mkoa wa Dodoma kazi ya kufanya Upembuzi Yakinifu imekamilika. Kwa sasa uongozi wa Benki unapitia taarifa ya upembuzi huo, na kazi zitaanza hivi karibuni za kuanzisha matawi hayo katika maeneo hayo.

2. Kwa upande wa Unguja kazi ya kuweka mashine za *ATM* katika maeneo ya JKU Saateni, Paje na Chwaka ujenzi ushakamilika na mashine zimeshafungwa, hivi sasa *PBZ* inaendelea na kazi uunganishaji wa *ATM* hizo na Mtandao wa Benki.

3. Kuhusu *ATM* inayotarajiwa kuwekwa Vuga Mahakamani eneo tayari limeshapatikana. Hata hivyo, Benki inatafakari iwapo iendelee na uwekaji wa *ATM* au Kituo cha Huduma kitakachowezesha wateja pia kuweka pesa.

4. Kwa upande wa Pemba, *ATM* zote zimeshanunuliwa na kupelekwa Pemba. Kazi ya uwekaji katika maeneo yaliyokubaliwa itafanyika hivi karibuni.

(b) Kwa sasa hakuna sehemu ambayo kazi imeshakamilika. Hata hivyo, kama nilivyoeleza, maeneo ya JKU Saateni, Paje na Chwaka yameshawekwa mashine za *ATM* na yapo katika hatua za mwisho za kuunganishwa na mtandao na kuanza kutumika.

Mhe. Spika, pamoja na maelezo haya naomba kusahihisha taarifa iliyotolewa na Mhe. Mwakilishi kuwa TZS 46.06 bilioni kwamba ndio zilizopangwa kutumika kwa shughuli hizi. Fedha hizi zilipangwa kwa ajili ya Bajeti nzima ya matumizi ya *PBZ* kwa mwaka wa fedha 2017/18. Kwa hiyo, hizi fedha sio kwa ajili ya shughuli hizi alizozisema Mwakilishi.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwanza, naipongeza Benki yetu ya Watu wa Zanzibar kwa kazi zao nzuri walizoahidi.

Mhe. Spika, kwa kuwa kwa upande wa Bara hii kazi bado haijafanyika vizuri. Na kwa kuwa wengi wetu Wazanzibari huwa tunatembelea sana Bara hasa Mkoa wa Dodoma. Je, Mhe. Waziri ni lini kazi hii itakamilika kwa upande wa Bara.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mussa Foum Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu nililolitoa la swali mama kwamba kazi hii inaendelea. Kwa upande wa uwekaji wa tawi katika eneo la Kigamboni kazi *almost* imekamilika. Kwa maeneo mengine ya Tandika na Dodoma kazi hiyo inakwenda kwa *speed* nzuri. Ni matarajio kwa sababu benki hii ni benki ya biashara tunataka kufanya biashara, basi tutaendeleza kazi hizo kwa ufanisi mkubwa ili haraka iwezekanavyo shughuli za utoaji wa huduma katika vituo hivyo ziweze kufanyika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Katika majibu yake amesema kwamba kwa upande wa Pemba *ATM* zote zimeshanunuliwa na kupelekwa Pemba na kazi ya uwekaji katika maeneo yaliyokubaliwa yanafanyiwa kazi hivi karibuni.

(a) Je, ni maeneo gani ambayo yatawekwa *ATM* hizo.

(b) Haoni kwamba ipo haja ya kuweka *ATM* katika eneo la mji wa Kengeja ili kuondoa dhiki ya wananchi wa Muambe, Kiwani na Kengeja yenyewe kwa kufikisha huduma karibu na wananchi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza kwa upande wa maeneo, eneo la kwanza ni Chake Chake *ATM* itawekwa, lakini maeneo mengine nitampatia baadae kwa maandishi. Lakini kama nilivyojibu jana Mhe. Spika, kwamba maeneo yote ambayo yataonekana yana mvuto wa kibiashara na huduma hiyo inahitajika basi *ATM* hizi zitafungwa. Sio Kengeja tu, lakini maeneo mengi Micheweni, kuna jana pia nilielezwa sehemu ya Wesha. Sasa maeneo haya yote yatafanyiwa ukaguzi na benki yenyewe na yakionekana kwamba kuna haja ya kuwekwa huduma hiyo, basi *ATM* hizo zitawekwa. Benki ipo kwa ajili ya kufanya biashara, kwa hivyo *demand* ikiwepo mahitaji yakiwepo hawatasita kuweka *ATM*.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza, lakini nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake. Mhe. Spika, katika ukuaji wa benki kiuchumi na kimapato ni lazima benki yetu ibadilike na ibadilike ielekee katika kutoa huduma za kisasa kama *mobile bank, internet bank* na *Visa*. Lakini pia iendane na mfumo wa utoaji wa huduma ile ya malipo kwa kupitia kadi.

Je, benki yetu ina utaratibu gani wa kuingia katika mabadiliko ya kibiashara na kuachana na mfumo huu wa Umoja *Switch* ambao hauwezi kutuletea tija, kama ambavyo matarajio ya mabadiliko ya uchumi ndani ya nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba Mhe. Mwakilishi arudie lile swali, naomba awe karibu zaidi na *microphone*.

Mhe. Spika: Kaa karibu na *microphone* halafu pia uliza kwa ufupi kidogo isiwe hotuba.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, nikirudia kwa ufupi sana itakuwa haikai sawa, lakini nitajitahidi sana. Katika ukuaji wa benki zetu, hasa hii *PBZ* kiuchumi na kimapato kwa kuingia katika huduma za kisasa, maana yake tuko katika huduma ambazo sio za kisasa. Kama, nitatolea mfano wa *mobile bank, internet bank, Visa* na kuachana na ule mfumo wa *Umoja Switch* ambao unaishia tu mikoani. Lakini na huduma

zile za malipo ya kadi kama unakwenda *shopping mall* unatoa kadi yako malipo. Mtu anaweza kufanya malipo kwa urahisi zaidi kuliko kwenda kuchukua *cash* akapoteza muelekeo.

Je, ni lini benki yetu itaachana na mfumo wa huduma hizi ambazo tunakwenda nazo sasa hivi na zimeshapitwa na wakati na kuingia katika mfumo mpya wa soko la kisasa ambalo litatusaidia kuongeza mapato zaidi nchini.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza mara nyingi nimekuwa nikisema kwamba benki yetu imo katika kufanya mageuzi na kuingia katika mfumo wa kisasa kwa kutumia Tehama zaidi katika utoaji wa huduma zake. Jana nilisema kwamba benki hii imeshaanzisha huduma za *mobile bank*, na kwa kupitia huduma za *mobile bank* sasa mteja anaweza kutoa fedha zake na kuhaulisha katika mitandao ya Mpesa, Ezypesa, Tigopesa.

Vile vile *PBZ* imeshaanzisha *internet bank* ambayo watu sasa wanaweza wakapata huduma kwa kutumia mtandao wa kompyuta. Pia *BPZ* ni mwanachama wa *Umoja Switch*, kwa hivyo unaweza kutumia kadi ya *PBZ* na kuweza ku- *access* huduma katika benki nyengine. Lakini vile vile *PBZ* nao baadae watakuwa na utaratibu wa matumizi ya *Visa* na *Master Card*.

Nam. 18

Kiasi cha Makusanyo ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:-

Katika Bajeti ya mwaka 2017/2018, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) ulipanga kukusanya jumla ya Tsh. 93.6 bilioni, kati ya hizo Tsh. 52.04 bilioni kutoka kwa wanachama wa Serikalini, Mashirika ya Umma, Taasisi binafsi na waliojiajiri wenyewe, Tsh. 4.99 bilioni zitakusanywa kutokana na uwekezaji wa majengo na Tsh. 36.57 bilioni zitakusanywa kutokana na uwekezaji wa masoko ya fedha na mitaji ya muda mrefu na mfupi.

(a) Je, mpaka muda huu *ZSSF* imeshakusanya kiasi gani

(b) Je, kwa sehemu zote tatu zimefikiwa nusu ya lengo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Hadi kufikia 27 Novemba 2017 *ZSSF* imeweza kukusanya jumla TZS 38.3 bilioni.

(b) Kwa kuwa ndio kwanza tumemaliza miezi mitano ya mwaka wa fedha 2017/2018, naomba kueleza kwamba hadi tarehe 27 Novemba 2017, sehemu zote tatu bado hazijafikia lengo la mwaka huu wa fedha. Hata hivyo, kwa kuzingatia malengo ya nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/2018, na kukusanya jumla ya TZS 42.00 bilioni, *ZSSF* imefikia asilimia 91 ya lengo hilo baada ya kukusanya jumla ya TZS 38.30 bilioni, wakati bado mwezi mmoja kukamilisha nusu mwaka. Sehemu ambayo haikufikia nusu ya lengo la kipindi hicho ni mapato yanayotokana na ukodishaji wa majengo ambayo kwa lengo hili *ZSSF* imefikia asilimia 44 ya lengo.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu mazuri. Lakini Mhe. Spika, ukiona *ZSSF* inakusanya pesa na pia inaingia katika uwekezaji mbali mbali na tukizingatia uwekezaji huu ni lazima uwahusishe pia na wale wenye fedha zenyewe, nawakusudia wale wanaochangia mfuko huu.

(a) Je, kuna utaratibu gani wa kuwahusisha wenye mtaji huu au wadau husika wa hizi fedha katika uwekezaji wenyewe.

(b) Hisa gani wanayoipata baada ya uwekezaji kwa sababu wao ndio wenye zile fedha zenyewe. Sasa ile faida inayopatikana kwenye uwekezaji wa fedha hizi za wadau. Je, ni hisa gani anayoipata kwa kila anayechangia mfuko huu wa *ZSSF*. Nashukuru.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Kwanza kazi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni kukusanya michango ya wanachama, lakini baada ya kuikusanya michango hiyo kuwekeza michango hiyo kwa ajili ya kuuwezesha mfuko kulipa mafao ya wanachama ya muda mrefu. Kwa hivyo, wanachama wanafaidika sio wa hisa, kwa sababu mfuko haujengwi kwa hisa. Michango ya wanachama inawekezwa kwa ajili ya wale wanaochangia kuja kupata mafao yao.

Mhe. Spika, mafao yako ya aina nne kwa sasa. Mafao ya uzeeni, iwapo kitatokea kifo, mafao ya ulemavu, lakini na sasa mafao ya uzazi. Kwa hivyo, sio suala la hisa hakuna hisa ni suala la kupata mafao yao kwa mujibu wa sheria.

Nam. 108

Kuvuja Kwa Skuli ya Madungu Sekondari

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi katika jitihada zake za kuendeleza na kujenga maskuli mapya na ya kisasa. Katika mji wa Chake Chake ipo skuli ya Madungu Sekondari ambayo ni ya kisasa na takriban Wilaya zote za Zanzibar zimejengwa skuli hizo ili kukuza elimu. Katika skuli ya Madungu Sekondari skuli hiyo ina takriban miaka miwili tokea ianze kufanya kazi lakini skuli hiyo sasa hivi imekaa kama gofu, maana yake skuli hiyo inavuja na dari (*Ceiling*) zake zote zimeharibika na

ikinyesha mvua, maji yote yanaingia ndani mpaka wanafunzi wanashindwa kusoma wakati wa mvua inakuwa hakuna tofauti kati ya uwanjani na ndani ya skuli.

(a) Je, Serikali inalifahamu suala hilo na imechukua hatua gani kwa mkandarasi aliyejenga skuli hiyo.

(b) Je, Mkandarasi aliyejenga skuli ya Madungu Sekondari ndie aliyejenga skuli zote za Zanzibar za aina hiyo.

(c) Je, wakati wa ujenzi wa skuli ya Madugu Sekondari ilikuwa na msimamizi wa Wizara ya Elimu au wa Serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 108 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangalizi.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imejenga skuli 19 za Sekondari na Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa huko Mchangamdogo, na imezifanyia matengenezo makubwa skuli sita za sekondari, Unguja na Pemba. Kazi za usanifu michoro ya Skuli hizo zilifanywa na Kampuni ya "*PSM Architect*" ya Dar es Salaam, na michoro ya Skuli tatu za ghorofa zilizojengwa katika Mkoa wa Mjini/Magharibi Unguja, iliandaliwa na Kampuni ya Otieno Odongo ya Kenya. Kazi za ujenzi zilifanya na Kampuni mbali mbali za ndani na nje ya nchi.

Baada ya maelezo hayo sasa namjibu kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inalifahamu suala la kuvuja kwa skuli ya Sekondari ya Madungu, ambayo limesababishwa na baadhi ya mapaa yake kukosa *slope* ya kuteremsha maji. Tatizo hilo halikusababishwa na Mkandarasi bali limesababishwa na mchoro wa ujenzi wa mapaa ya skuli ulioandaliwa na Mshauri Elekezi wa Kampuni ya *PSM Architect* ya Dar es Salaam, Mkandarasi alikuwa na wajibu wa kujenga kwa mujibu wa mchoro na maelekezo ya msimaizi ujenzi, kutoka kwa Kampuni ya "*PSM Architect*". Mshauri Elekezi ambae aliwahi kushauriwa kubadili mchoro wa mapaa na hakukubaliana na ushauri huo kwa kuamini kazi ya mapaa hayo hayatovujisha kwa utaalamu wake. Kutokana na kuvuja kwa mapaa ni kweli baadhi ya madarasa ya skuli hiyo yameathirika na wizara hivi karibuni imeomba ushauri kwa wataalamu wa ujenzi kutoka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ili kuweza kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo.

(b) Mkandarasi aliyejenga Skuli ya Madungu hakujenga skuli zote za Zanzibar. Jumla ya wakandarasi nane walijenga skuli hizo kwa kufuata michoro iliyotarishwa na Mshauri Elekezi. Wakandarasi hao ni Kampuni ya *RANS* na *Quality Building Contracto*r za Zanzibar, *CRJE*, *China Hainan*, na *Group Six*

Internation za China. Skuli nyengine zimejengwa na Kampuni ya *Electric International*, B.H.Ladwa na Lukumbulu *Contractor* za Dar es Salaam.

(c) Usimamizi wa ujenzi wa Skuli ya Madungu ulifanywa na Kampuni ya Ushauri Elekezi na Wahandisi wa Wizara walikuwa na jukumu la kuwasimamia Mkandarasi na Mshauri Elekezi. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake mzuri, lakini nataka nizungumze kwamba Skuli ya Madungu Sekondari au Madungu mpya ni skuli ambayo imetia aibu sana katika ujenzi wake. Mimi nataka kumuuliza Mhe. Waziri kwamba kama Mshauri Mwelekezi alikataa kwamba mapaa yale hayako sawa na mchoro ambao ulikubalika na yeye akakubali. Je, ina maana yeye ndiye aliyebeba jukumu hilo la kwamba yeye ndio amekubali kuwa likivuja atalipa.

Pia niulize kwamba hata kama ni kutokupata kwa ushauri elekezi, kuna bati gani kwa muda wa mwaka mmoja au mwaka mmoja na nusu mpaka miaka miwili zikaoza na zikawa hazifai, zina *guarantee* gani bati hizi, maana yake tatizo ni bati ndio chanzo cha matatizo yote.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, katika mchakato wa ujenzi kuna hatua nyingi ambazo zimechukuliwa mpaka kukamilika kwa ujenzi. Kuna Mshauri Elekezi, Mkandarasi, *Management* ya Wizara na mambo mengi mbali mbali.

Sasa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuelewa utata uliopo, ameshaunda timu ya uchunguzi kulichunguza suala hili kwa undani wake na timu yenyewe inahusisha wataalamu kutoka wizara mbali mbali na hata katika mashirika binafsi, ili kujua nini hasa chanzo cha uvujaji wa skuli hizi. Sio Madungu peke yake, hizi skuli 19 nini hasa chanzo chake. Kwa hivyo, tusubiri mapendekezo ya kamati na wizara itachukua hatua, pale ambapo itakuwa tatizo ni huyu Mshauri Elekezi basi wizara itachukua hatua, lakini ikiwa ni *contractors* wizara itachukua hatua, lakini na hata ikiwa ni management ya wizara basi wizara itachukua hatua, tusubiri mapendekezo ya kamati hiyo.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kupata wasaa huu wa kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri. Kwanza nimpongeze kwa majibu yake mazuri yenye ufasaha.

Mhe. Spika, kinachogomba ni kwamba hili suala la huyu Mkandarasi na huyo *Architect* wake, imebainika kwa wadau wengi sana na wizara imejulishwa mara nyingi kuhusu hili suala. Mbali na alivyotuambia Mhe. Naibu Waziri kwamba imeundwa kamati, lakini kamati hiyo itatoa lini ripoti yake ikamilishe huku mapaa yanavuja.

(a) Sasa atuambie ni hatua gani wizara itachukua ili kurekebisha hayo majengo na mapaa ya skuli zinazovuja.

(b) Mhe. Spika, kumpa tena au kuwapa tena kazi wakandarasi wale wale ambao tumeona kwamba wame-*perform below standards* na wame-*perform* kitu ambacho hakina *valuefor money*. Huo ni ukweli kabisa usiopingika.

Sasa mimi kwa kupitia kwako Mhe. Spika, ningeshauri sana hiyo kamati aliyounda Mhe. Waziri tunaiheshimu. Lakini mimi ningeshauri tuunde kamati yetu Barazani hapa kupitia kamati zako, ili twende tukaipitie mikataba hii wakati ujenzi ndio kwanza mchanga, tusingoje mpaka jengo liko kasorobo au karibu kufunguliwa, tuka-*check* mikataba hivi sasa. Ahsante hili lilikuwa ni ombi kwako maalum.

Mhe. Spika: Ahsante, jibu swali la mwanzo kwa sababu swali la pili ni ushauri tu, jibu lile la mwanzo. Waziri majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo. Mhe. Spika, suala hili la uvujaji wizara tunalielewa na tumeshawatuma Ma-*engineer* wetu kufanya gharama za matengenezo na tutaanza mara moja kuikarabati Skuli ya Madungu na skuli nyengine zitafuatia hatua kwa hatua. Ahsante.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii pamoja na majibu ambayo hayatutii moyo kuhusu hasa upoteaji wa fedha nyingi sana za *contractor* hii. Mimi ninavyofahamu, naomba nimuulize Mhe. Waziri haya yafuatayo. Ninavyoelewa mimi katika *construction* kunakuwa na *general condition*, halafu kuna *consultant*, halafu na wizara nayo supervision. Paa linalovuja skuli hii linavunja moyo.

Kwa hivyo, nini tatizo baina ya *general condition* au mkandarasi au huyu ambaye ni *consultant*, na kama ni *consultant* yeye kaadhibiwa vipi, analipwa huyu na anakuwemo katika *bill of quantity*, kwamba huyu atashauri upande wa kulia na upande wa kushoto, yaani baina ya mwenye kazi na baina ya aliyepata kazi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri huu mzigo hasa uko kwa nani, uko kwa *general condition*, sisi tumekosea au tumeteleza mkandarasi kiwango chake kidogo, au huyu ambaye tumempa mshauri mwelekezi. Naomba majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo. Mhe. Spika, nadhani swali lake ni la msingi na zuri sana na sisi wizara pia tulikuwa tunajiuliza hivyo na ndio tukafikia hatua ya kuunda kamati ya kuchunguza. Hiyo kamati itatueleza wapi tatizo *contractors*, *consultant* au *management* ya wizara, tufanye subra tusubiri tutamjua nani anahusika na suala hili. Ahsante sana.

Nam. 69

Mpango wa Kupeleka Wataalamu wa Kilimo Nje

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ilifanya maonesho makubwa pale Kizimbani/Dole, na kwa sababu ni nzuri kwani wananchi wetu walipata fursa ya kujionea mazao mbali mbali yanayozalishwa hapa Zanzibar ambapo pia wakulima wetu wameweza kujifunza mengi kupitia maonesho hayo. Vile vile, JKU nao walionesha bidhaa zao ambazo wamelima na wanaushirikiano kutoka Misri.

(a) Je, Wizara ya Kilimo Zanzibar ina mpango gani wa kupeleka wataalamu wetu nchini Misri kwenda kuongeza utaalamu wa kilimo cha umwagiliaji, hasa kwa kilimo cha mboga mboga ili tuweze kuongeza uzalishaji kwa wakulima wetu.
(b) Je, kuna utaratibu gani wa kuwapatia wakulima wetu zile mbegu bora kutoka Misri hasa za nyanya, vitunguu, pilipili boga n.k ambazo zilionesha kwenye banda la JKU.
(c) Je, Wizara imefikiria ni lini utaratibu wa kuanzisha maonesho mazuri ya kilimo kama yale yatafanywa pia kwa upande wa Pemba.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara ina ushirikiano wa muda mrefu na Serikali ya Misri katika kuendeleza kilimo, ikiwa ni pamoja na kubalishana wataalamu wa kilimo cha mpunga, matunda na mboga. Aidha, wizara yangu bado ina nia ya dhati ya kuendeleza ushirikiano huo mzuri uliopo.

(b) Mhe. Spika, wizara haina mkataba wa utekelezaji wa moja kwa moja na shamba la kilimo la JKU. Aidha, wizara kwa kushirikiana na Shamba la JKU Bambi, wanafanya tafiti ili kuona uwezo na ustahamilivu wa mbegu hizo kabla ya kuigawa kwa wakulima. Baada ya kukamilika kwa utafiti huo wizara itazigawa kwa wakulima.

(c) Mhe. Spika, wizara imeshafanya maamuzi ya kuanzisha maonesho ya kilimo katika kisiwa cha Pemba. Aidha, siku ya Chakula Duniani ya mwaka 2018 ndio iliyopangwa kufanyika maenesho hayo. Eneo la ekari 10 katika shamba la Chamanangwe limeshatengwa kwa ajili ya maonesho hayo.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuniruhusu nimuulize Mhe. Waziri mwalimu swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba serikali inakuwa na mashirikiano mazuri na Serikali ya Misri.

(a) Je, nataka nijuwe ni wataalamu wangapi tumeshawapeleka kule Misri kwenda kujifunza hichi kilimo na kuongeza utaalamu wetu hasa wa kilimo cha *green house*, ambacho tunaamini kwamba kilimo hichi kitakapowezeshwa basi kinaweza kikaleta tija kubwa sana kwa wakulima wetu hapa Zanzibar.

b) Je, Wizara ya Kilimo, haioni kwamba iko haja kwa sababu wao hawajakuwa na mikataba ya moja kwa moja na shamba la JKU Bambi, haioni kwamba kwa kuwa wao ni taasisi ya Serikali na JKU ni taasisi ya Serikali kwa kuwatumia Wataalam wa Wizara ya Kilimo na vijana wa JKU wanaoingia makambini, wakaweza kuwezeshwa kiutaalam kwa kutumia kilimo hiki wakawafundisha ili na wao wakitoka pale wakaweza kuwa wataalam wazuri, wakenda wakawafundisha wenziwao nje na wakaweza kumudu maisha yao?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:

a) Suala la *Green House* kwa bahati nzuri utaalam upo wa kutosha, tatizo ambalo tumeligundua katika suala la *Green House* ni gharama za uwekezaji wenyewe ndio tatizo la msingi. Lakini kwa taaluma tunayo ya kutosha tunayo kutoka kwa wenzetu wa history, tunayo ndani ya Wizara yenyewe, tunayo vile vile kutoka na taasisi mbali mbali za kilimo zilizoko Bara na hapa Zanzibar. Kwa hivyo nasema taaluma ipo hata ukienda kwenye chuo chetu cha Kilimo pale Kizimbani vile vile tunao wataalam pale na tunayo *green house* tumeweka pale kama ya kufundishia. Kwa hivyo taaluma ipo tatizo kubwa tulilogundua sisi ni kiasi cha kuwekeza katika kila nyumba moja ya *green house* inagharimu si chini ya milioni sita mpaka saba.

Kwa hivyo hilo ndio tatizo la msingi na sasa hivi tunalikabili tatizo hilo kwa kushirikiana na benki ya kilimo ili wale wakulima ambao watakuwa tayari kuingia katika kilimo cha *green house* waweze kupatiwa mikopo na waweze kuingia katika ukulima huo wa *green house.* Kwa hivyo nasema taaluma kwa kweli kwa kiasi kikubwa tunayo kazi kubwa tuliyonayo ni ile *infrastructure* yaani *investment* katika *infrastructure* yenyewe.

b) Suala la Wataalam ambao wanajifunza kutoka JKU na kadhalika, Mhe. Spika, ni kweli vijana wanaofundishwa pale JKU madhumuni yake makubwa ni kwamba wakatoe taaluma waliyonayo kule wanakokwenda ndio maana ya JKU hasa, si pahala pa kudumu pale kwao wanapata taaluma wakiondoka hapo waendeleze taaluma yao. Kwa hivyo nasema hilo linafanyika na tunashirikiana na Chuo chetu cha Kilimo vile vile kuendeleza taaluma hiyo.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuuliza suala dogo la nyongeza, lakini kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake fasaha juu ya suala mama la Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Spika, suala la *green house* ni suala ambalo ni muhimu sana kwa kilimo cha wakati huu na gharama zake ni kubwa.

a)Je, Wizara imefanya utafiti kuona kwamba kutakuwa na mbinu nyengine mbadala za kuweza kupunguza gharama hizo kwa kutumia mali ghafi au bidhaa zilizokuwemo ndani.

b)Wizara ina mkakati gani wa kuweza kuisambaza elimu hii hadi vijijini mkiacha maonyesho ya kilimo.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mhe. Rashid Makame kama ifuatavyo.

Kwanza ni kweli kwamba kunahitaji kutumia teknolojia nyengine mbali ya hii ambayo imezoeleka ya *green house* na kama ulihudhuria katika maonyesho yetu tuliyofanya pale Kizimbani, vijana wale wa Malindi walionesha kwamba tunaweza tukatumia malighafi zetu tulizonazo ndani ya nchi kwa kuweza kumwagilia maji kwa matone, lakini vile vile kutumia njia nyengine ya *green house* badala ya kutumia *important materials* ambazo zinatumika hivi sasa. Kwa hivyo nasema ni kweli nakubaliana na wewe kabisa kuna haja ya kuangalia *technologia* mbali mbali za kupanda kwa *green house*.

Lakini kubwa katika *green house* nimejifunza ni kule ku-*control* maradhi, kuhakikisha dawa zinapatikana kwa wakati na maji yanapatikana kwa wastani unaotakiwa. Kwa hivyo kama utafanya *drip irrigation* kwa mfano yenyewe vile vile inakusaidia sana katika kupunguza matatizo haya ambayo tunayoyazungumza. Kwa hivyo nasema teknolojia nakubaliana nae kuna haja ya kuangalia *technologia* nyengine ambazo zita-*suplement* haya *material* tunayotumia.

Kuhusu suala la pili sijalipata vizuri.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Spika, suala langu la pili kwamba Wizara ina mikakati gani ukiacha maonesho ya kilimo ambayo yameanza mwaka huu, kuweza kuieneza taaluma hii vijijini kwa wananchi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, hivi sasa Wizara mbali na kazi tulizofanya kwenye maonesho nasema imeleta *impact* kubwa sana Mhe. Spika, vijana pale wameendelea kuja mpaka sasa hivi ndugu zetu wa JKU wapo pale wanakwenda wanatoa mafunzo na watu wanapata taaluma. Kwa hivyo kwanza maonyesho yamesaidia sana katika kupanua umuhimu wa watu kupata taaluma ya kilimo.

Lakini la pili tulilofanya bwana shamba na bibi shamba ambao tumewapeleka katika maeneo mbali mbali na wenyewe vile vile wasaidie katika kutoa taaluma, na kwa bahati nzuri hawa sasa wamegatuliwa wako kwenye Serikali za Mitaa mimi nafikiri taaluma kwa wananchi wa vijijini itakuwa imefika kwa urahisi zaidi.

Nam. 73

Uimarishaji wa Vitalu vya Mikarafuu

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa msimu wa kuatika miche kwa ajili ya matayarisho ya upandaji miti kwa kipindi cha masika kitakachoanza mwezi wa March 2018, na kwa kuwa sababu miche ya aina tofauti hupatikana kwenye vitalu vya Serikali pamoja na miche ya mikarafuu ambayo wananchi wengi wamehamasika kuipanda kwa wingi sana.

Je, kuna mpango gani kwa Wizara kuongeza vitendea kazi kama vile "*Rainboot"*, "*wheelbarrow"* na keni za kumwagilia maji sambamba na kuongeza wafanyakazi ambapo inaonekana kuna upungufu mkubwa katika vitalu vya Serikali.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 73 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli wafanyakazi waliopo katika vitalu vya Serikali ni wachache pamoja na upungufu wa vitendea kazi. Katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Wizara imepanga kununua vifaa vikiwemo keni 48, Mabero 16 pamoja na viatu vya mvua 120 ambavyo vimepangwa kununuliwa katika Bajeti ya mwaka huu. Aidha, Wizara imewasilisha maombi ya ajira ya Wafanyakazi 83 katika Wizara husika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya mwelekeo ya Mhe. Waziri, lakini naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kuna upungufu wa wafanyakazi Mhe. Waziri umekiri na kuna upungufu wa vitendea kazi kama nilivyouliza kwenye swali langu mama na wewe umeainisha hivyo vifaa ambavyo mmepanga kuvinunua.

a) Je, kwanza hivyo vifaa mulivyopanga kuvinunua ndio vifaa vitakavyokidhi haja kwa vitalu vyetu vyote vilivyopo Unguja na Pemba.

b) Je, ni lini vifaa hivyo vitanunuliwa na kuvipeleka kwa wafanyakazi wetu kwenye vitalu ambapo sasa hivi msimu wa upandaji wa miche tunayoitegemea kwa mwezi wa tatu unakaribia, ni lini na mpaka sasa hivi havijanunuliwa lini vitanunuliwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwakilishi kama ifuatavyo:

Kwanza kama unavyofahamu hivi sasa katika ugatuzi sehemu za vitalu sehemu kubwa tayari tumeshavipeleka kwa ndugu zetu Tawala za Mikoa, lakini kwa upande wetu sisi kama Wizara Vifaa tulivyonunua tunaamini kabisa vitatosheleza vile vitalu ambavyo tunavyo hivi sasa, kwa hivyo suala la kutosheleza hatuna wasiwasi vitatosheleza kabisa kabisa.

Lakini la pili lini vitanunuliwa Mhe. Spika, katika *quarter* hii tuliyonayo hivi sasa tayari tenda imeshatangazwa na mimi naamini kabia wakati wowote vifaa hivi vitanunuliwa ili kusambazwa na viwahi msimu wa mvua kama vile ambavyo tumekusudia kufanya.

Nam. 62

Kupelekwa Huduma ya Umeme Kisiwani Kokota na Uvinje

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Serikali ina Mpango wa kupeleka umeme Kisiwa cha Kokota kutokea Fundo na Uvinje na kwa sababu wakaazi wa Kisiwa cha Kokota wanakwenda zaidi kupata huduma zao nyingi eneo la Kivumoni ambapo kuna vijiji havijapata kufikishiwa huduma ya umeme navyo ni Mtekofi, Mtemani, Kipangani, Migombani na Utaani ambapo kuna zaidi ya nyumba zao za Makaazi na kwa sababu "Transformer" iliyofungwa Fundo Mabaoni ina uwezo wa kutosheleza matumizi kwa ajili ya Mabaoni na Uvinje.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kupeleka umeme Kisiwa cha Kokota kupitia Kivumoni kutapunguza gharama za mara ya pili ya ujenzi wa laini kubwa nyengine kwa ajili ya vijiji vya Kivumoni na pia kutasaidia kupeleka huduma hiyo kwa wakaazi wa Kisiwa cha Funzi ambacho kipo karibu na Kisiwa cha Kokota.
(b) Je, ni lini kazi za awali za upelekaji wa umeme kisiwani humo zinatarajiwa kuanza.
Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62 lenye vipengele (a) na (b) lakini kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Ni kweli Serikali imeweka *transformer* yenye uwezo wa 50KVA kwenye kijiji cha Mabaoni – Fundo, lakini uwezo wa *transformer* hiyo hauwezi kuwahudumia wananchi wa Kisiwa cha Uvinje walioko masafa ya 3.5km kutoka mahali ilipo *transformer* ya Mabaoni. Kitaalamu, *transformer* inatakiwa iwahudumie wananchi kwenye mzunguko usiozidi 2km ili waweze kupata umeme wenye kiwango kinachokubalika. Hivyo, ili wananchi wa Kisiwa cha Uvinje wapate huduma nzuri na salama Serikali itapeleka Umeme na kuweka *transformer* maalum kwa Kisiwa cha Uvinje.
.
Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, katika kazi za upelekaji Umeme kwenye visiwa ambavyo uwezekano wa kutumia nguzo ni mdogo na badala yake kulazimika kutumia waya wa baharini, gharama ya upelekaji huwa kubwa kutokana na masafa ya matumizi ya baharini baina ya pande mbili. Kwa upande wa Kisiwa cha Kokota, masafa yaliyopo baina ya Mkanjuni na kokota ni 8.23km (kati ya hizo 3.8km utatumika waya wa baharini) na kwa kutokea Fundo masafa ni 8.12km (kati ya hizo 2.1km utatumika waya wa baharini), hivyo kwa namna yoyote gharama kwa kutokea Fundo kwenda Kokota ni pungufu kulinganisha na Mkanjuni kwenda Kokota.

(b) Mhe. Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2017/18, Serikali imepanga kupeleka huduma ya Umeme kwenye Kisiwa cha Uvinje, ambapo kazi za awali zikiwemo Ukaguzi wa Njia *(Route Survey)*, Upimaji, Utambuzi wa waathirika wa Vipando na Uthamini wake utafanyika kwenye robo ya pili ya mwaka. Kazi za ujenzi wa njia kuu, uwekaji

transfoma na ujenzi wa njia ndogo zitafanyika kwenye robo ya tatu ya mwaka huu wa fedha.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kumuuliza Mhe. Waziri suali la nyongeza pamoja na majibu mazuri na hisabu alizozifanya lakini mimi siamini kama hivi hisabu zimefanywa vyema.

Kwa sababu mimi katika swali niliainisha kwamba kuna baadhi ya vijiji ambavyo vinastahiki kupata umeme ukiachilia mbali kijiji cha Uvinje ambacho kina wakaazi wasiozidi 200 na Kokota labda 500, lakini vijiji nilivyovitaja ambavyo nimeviainisha vina wakazi zaidi ya 700 ambavyo Wizara itawajibika kutumia gharama mara mbili.

Je, ikiwa dhamiri ya Serikali ni kupeleka umeme kwa wananchi wote, lini wananchi wa vijiji vilivyozunguka kijiji cha Kivumoni na Kisiwa cha Funzi Serikali itawafikiria kuwafikishia umeme, kama ilivyopanga kuwafikishia Uvinje na Kokota ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni sahihi kwamba Serikali imelenga kuhakikisha wananchi wanafikiwa na huduma lakini tunakwenda awamu kwa awamu. Sasa kama niliwahi kusema hapa mpaka kufikia 2020 vijiji vyote vile ambavyo vilivyokuwepo basi vitafikiwa na huduma hii ya umeme ahsante sana.

Mhe. Makame Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Sekta ya nishati hususan umeme ni nyezo muhimu katika kuwawezesha wananchi katika hali ya kimaisha, hiyo ni ilani ya Chama cha Mapinduzi ndivyo inavyosema ukurasa wa 154.

Lakini ni sababu gani inayopelekea kwamba wafanyakazi wa Shirika la Umeme au shirika la umeme wanapopata ufadhili yaani kama mfano wawakilishi kuwapa gharama kubwa ya kuwapeleka nguzo wananchi mpaka taimu nyengine kushindwa ili kuweza kuwahudumikia sisi kuweza kuwahudumia wananchi na kupandisha bei, yaani nguzo kama tano unaambiwa ulipe milioni saba au kumi.

Ni sababu gani inayopekea hivyo kwamba wapandishe bei hizo za nguzo na kushindwa sisi kutekeleza wajibu wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Shirika la Umeme halijawahi, halitawahi kumpandishia Mhe. Mwakilishi au mwananchi wa kawaida gharama bali unazopewa ni zile gharama ambazo *reasonable* kutokana na eneo lilipo. Lakini inapotokezea hali kama hiyo basi ni vyema tuambizane tujue namna ya kukamatana mikono. Ahsante sana.

Nam. 63

Uchakavu wa Vifaa vya Kutendea Kazi Idara ya Upimaji

Mhe. Omar Seif Abeid **-** Aliuliza:

Kwa kuwa Idara ya Utawala wa Ardhi ina jukumu kubwa la kusimamia maswala yote yanayohusiana na Ardhi *(Security of Land Tenure),* na kwa sababu kitengo hiki ni muhimu kwa ajili ya kutunza kumbukumbu pamoja na utayarishwaji wa ramani. Pamoja na kazi zote muhimu, Idara hii inakabiliwa na changamoto za ukosefu wa vitendea kazi kama vile kompyuta za kuingizia taarifa ambazo zimeshachoka sana na "printer" kubwa kwa ajili ya kutolea ramani na kutayarisha hati mbali mbali zinazohusiana na umiliki wa ardhi n.k.

(a) Je, ni kwa sababu gani Idara muhimu kama hii kutopatiwa au kubadilishiwa kompyuta na *"printer"* nyengine kila mara, pale ambapo itabainika kwamba kompyuta hizo au "printer" zimeshachoka ili kuleta ufanisi wa kazi katika Idara hiyo.
(b) Je, kuna mpango gani kwa Wizara kuipatia Idara ya Upimaji kwa upande wa Pemba vifaa vipya kwa ajili ya shughuli za upimaji ukitilia maanani kwamba vifaa vilivyopo ni vya zamani toka miaka ya 1990.
(c) Je, Wizara ina mpango gani wa kutatua tatizo la usafiri kwa kuwapatia gari Kamisheni ya Ardhi ambayo wana gari 1 "*Land Cruser"* ya tokea mwaka 1993 na "*Double Cabin"* ambayo limeshachoka sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Aliuliza:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Kabla ya kumjibu naomba kwanza kuwakumbusha Wajumbe wa Baraza lako Tukufu hili kuwa kwa sasa chombo kinachosimamia Utawala wa Ardhi hapa Zanzibar ni Kamisheni ya Ardhi ambayo imeundwa kwa Sheria Nam. 6 ya mwaka 2015.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kutokana na utaratibu wa Serikali wa kutumia mfumo wa *Program Based Budget (PBB)* kila taasisi inabidi ijipange kutekeleza programu zake na kuweka vipaumbele katika kufanikisha malengo yake. Bajeti ya Kamisheni ya mwaka 2017/18 imeingiza ununuzi wa kompyuta, *printer* na vifaa vyengine vya ofisini na hadi kumalizika kwa robo ya kwanza, kompyuta mpya 1 na *"printer"* 1 mpya zimenunuliwa kwa upande wa Pemba na kwa upande wa Unguja Kompyuta 2 na *"printer"* 1 zimenunuliwa kuchukua nafasi ya vile vilivyochakaa.

(b) Mhe. Spika, kwa upande wa vifaa vya upimaji hasa kwa Pemba, Kamisheni haijaweza kufanya manunuzi ya vyombo vya upimaji kutokana na ukubwa wa bei zake

kulinganisha na ukomo wa bajeti ya Kamisheni kwa ujumla wake. Hata hivyo, juhudi zinaendelea kutafuta ufumbuzi wa suala hilo.

(c) Mhe. Spika, Wizara ya Ardhi inawasiliana na Wizara ya Fedha kuona namna ya kuiwezesha Kamisheni ya Ardhi kubakishiwa sehemu ya mapato inayokusanya ili iweze kujikimu kwa ununuzi wa vitendea kazi, gari za kazi pamoja na mahitaji muhimu mengine badala ya kutegemea mgao wa jumla kutokana na Bajeti ambayo ina ukomo ulio chini ya mahitaji halisi ya Kamisheni.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri yenye mwelekeo wa kuiombea kupitia Wizara ya Fedha lakini napenda nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Yeye mwenyewe anajua umuhimu wa Wizara hii hasa Idara hiyo ya Ardhi mambo ya upimaji.

a) Je, kwa kuwa mpaka sasa vyombo vilivyopo pale kwenye ile Idara kwa upande wa Pemba vimeshachakaa ni vibovu haioni kwamba kuendelea kuviachia vyombo vile vikawa ndio vinavyotumika pale kutashusha morali ya wafanyakazi wetu kuweza kufanya kazi.

b) Lini hatua za dharura zitachukuliwa ili kuiwezesha japo robo ya *set* ya vitendea kazi wakapatiwa wafanyakazi wa Idara ya Upimaji pale Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Nafahamu kwamba ni muhimu kupata vifaa vipya na bora, lakini niseme hawakatiki morali wafanyakazi kwa sababu wanajua hali halisi tuliyonayo, lakini pia wanajua juhudi ambazo tunachukua kusudi kupata hivyo vifaa vyengine ikiwemo kama nilivyosema kwamba tunafanya mazungumza na Wizara ya fedha, basi *at least* tupate fedha kwa ajili ya haya mambo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona mimi Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Waziri na juu ya changamoto ambazo inazikabili hii Wizara katika vitendea kazi, lakini moja katika tatizo ambalo Idara hii ambayo inalikabili ni suala la jengo lake ambalo liko pale Forodhani karibu na Watu wa Zanzibar na kwa kweli Wazanzibari wengi wanahitaji huduma za tofauti, tofauti.

a) Sasa je, kutokana na mazingira ya lile jengo na eneo lipo je Wizara yake ana mpango gani kuhakikisha kwamba watapata jengo jipya ambalo litakuwa mbali na pale.

b) Unapoingia ndani ya Idara hii na wawekezaji wengi wanapokwenda kutafuta huduma juu ya masuala ya ardhi na mengineyo unashindwa kuwatambua nani ni

mfanyakazi, au nani pia ni mtu ambae amefuata huduma mle ndani. Je, Wizara yake ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba ndani wafanyakazi watakuwa wana mavazi ambayo wataweza kutambulika kama sare, lakini utambulisho wao pia utakuwa unaendana na mazingira ya kisasa pamoja na hali nzima ya uwekezaji kwa upande wa Zanzibar ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Naomba nianze na (b) tumelichukua wazo niseme lakini kwasasa ukifika pale Kamisheni ya Ardhi kuna mapokezi utaelekezwa kutokana na shida yako ilivyo, lakini kwa ujumla niseme wazo hili ni zuri basi tutalifanyia kazi.

Lakini namna ya Ofisi ni suala zuri pia niseme Wizara kama Wizara inapanga kujenga jengo lake sasa baada ya Wizara kuondoka kwenye jengo lile pale tunategemea labda tunaweza tukafanya mpango wa ku-*shift* ama vyenginevyo, lakini kwa ufupi pia umetupa kazi ya kufanya na kufikiria niseme ahsante sana.

Nam. 83

Ongezeko la Viwanda Visiwani Zanzibar

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein wanastahili pongezi kwa kuiongoza nchi na kuwaletea maendeleo endelevu kwa jamii hususan katika uimarishaji wa viwanda. Ikiwa kaulimbiu ya mwaka huu "Shiriki kupambana huu si wakati wa maneno ni wakati wa vitendo". Katika hotuba ya Rais Magufuli siku ya maadhimisho ya Mwenge wa Uhuru alisema kumeongezeka viwanda vipya 3,308 katika mwaka 2017.

(a) Je, ongezeko hilo la viwanda vipya Zanzibar tumepata vingapi ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano.

(b) Je, serikali ina mkakati gani kuona inapambana juu ya jambo hili ili kutoa fursa za ajira kwa vijana.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 83 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka wa 2017, jumla ya miradi mitano ilikuwa katika hatua mbalimbali za uwekezaji. Miradi hiyo ni:-

1. Sansi Group - Kiwanda cha maji ya chupa,
2. Kiwanda cha kutengenezea zana na vyombo vya uvuvi,
3. Kiwanda cha kutengenezea vipodozi
4. Kiwanda cha mafuta ya nazi, na
5. Kiwanda cha *"recycling of plastic bags"*.

Katika mwaka huu pia yamepokelewa maombi matano ya kuanzisha viwanda kama ifuatavyo:-

1. Kiwanda cha kuzalisha bidhaa za chuma
2. Kiwanda cha rangi
3. Kiwanda cha mbolea ya mboji *(organic fertilizer)*
4. Kiwanda cha matofali,
5. Kiwanda cha vito vya thamani na usonara.
6. Kiwanda cha mifuko na vifungashio *(paper bags)*

Viwanda hivyo pamoja na maombi mengine kwa kupitia Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi - ZIPA.

(b) Mhe. Spika, serikali inatambua haja ya kuimarisha sekta ya viwanda kwa ajili ya kutoa nafasi za ajira na kuinua vipato vya wananchi na vya serikali kwa jumla. Kwa lengo la kuimarisha mazingira bora ya usaidizi na maendeleo ya viwanda vidogovidogo nchini. Serikali inaandaa taratibu za kuanzisha chombo maalumu kitakachojulikana kwa jina la Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogovidogo na vya Kati, Zanzibar (SMIDA) ambapo moja ya majukumu yake itakuwa ni kusimamia uanzishwaji wa viwanda na kuviendeleza.

Aidha serikali imeandaa mpango ya kutenga maeneo maalum ya kuendeleza viwanda kila Wilaya ili kutanua nafasi za ajira na kuongeza kipato kwa wananchi kupitia maendeleo ya viwanda. Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

Changamoto kubwa inayokabili maendeleo ya viwanda hapa Zanzibar ni ukosefu wa soko la bidhaa.

a) Je, serikali inamikakati gani ya kutumia masoko ya nchi za Afrika Mashariki na Kati ili kupunguza changamoto hiyo.

b) Wizara ina mpango gani wa kuwashajihisha wananchi kwa kuwapa mitaji ili kuongeza kasi ya uwekezaji katika viwanda.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:

a) Ni kweli kuna changamoto ya masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa hapa Zanzibar. Kweli kuna fursa katika Soko la Afrika Mashariki na Soko la Afrika ya Kati kwa mfano kama Kongo na kwengineko.

Mhe. Spika, tatizo jengine linalotokea ni kwamba hawa wazalishaji mali wetu au wazalishaji wa biashara zetu yaani vitu vyetu pia bado bidhaa zao hazijafikia viwango vinavyotakiwa, kwa sababu kama tunavyojua tunapotaka kuuza bidhaa nje ya Tanzania au hata ndani ya Tanzania lazima viwango vikamilike. Kwa mfano upate *certificate* zile za viwango vya *ZBS* na ZFBA, ZFBB na kadhalika.

Mhe. Spika, jambo jengine linalosababisha watu wasipate soko ni kwamba bado hii taaluma ya masoko haijapatikana, hawajaweza kuijua wananchi watu wawekezaji hasa wajasiri amali. Kwa hivyo tunajitahidi sasa hivi kuwapa taaluma na kuwapa taarifa ya kujua masoko yako wapi na yanapatikana kwa sifa za aina gani na kwa bidhaa zipi. Taaluma hiyo tutaanza kuitoa kwa ajili ya kuwasaidia wajasiri amali wetu ili waweze kupata masoko.

Kama nilivyosema jengine wajasiri amali wetu pia ni waoga, hawapo tayari kujaribu kutoka nje ya Tanzania kwenda kuuza bidhaa zao, lakini pia biashara zao ndogo ndogo, kwa hivyo tunachotaka kufanya sasa hivi ni kuwawezesha biashara zao kukua ili waweze kwenda katika masoko ya nje. Lakini kubwa vile vile waweze kufanya biashara kwa ajili ya kutosheleza masoko yaliyokuwemo humo humo ndani ya nchi ya Zanzibar na Tanzania.

b) Mhe. Spika, kupatikana kwa mtaji sio tatizo moja peke yake linalowafanya wajasi amali wetu wasiweze kufanya shughuli zao vizuri. Lakini pia kwa sababu hapa Zanzibar tuna tatizo kwamba mabenki yetu hayatoi mitaji au mikopo au fedha nafuu kwa ajili ya wawekezaji au wajasiri amali. Kwa hivyo kuna haja kupitia Wizara ya Fedha serikali tukae tutizame utaratibu gani tunaweza kuwawezesha wajasiri amali kuweza kupata mikopo nafuu bila ya usumbufu.

Sasa hivi Benki nyingi hazina taratibu maalum za kutoa mikopo, wanasema sasa hivi kuwe na dirisha maalum kwa ajili ya wajasiri amali ili waweze kupata mikopo yao. Huwo utaratibu haujaanzishwa ingawa kuna nchi kama India katika Mabenki makubwa wameanzisha utaratibu wa kuwa na dirisha maalum kwa ajili ya wajasiri ambali. Hili nalo tutalizungumza na kulifanyia kazi ili waweze wajasiri amali wengine na wao wote waweze kupata mkopo kwa ajili ya kujiendeleza.

Nam. 84

Ongezeko la Idadi ya Watalii Zanzibar

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:

Katika hotuba yake Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa kilele cha Mwenge wa Uhuru katika Kiwanja cha Amani,

alimpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuwepo idadi kubwa ya uingiaji watalii hapa Zanzibar na pongezi hizi zimekuja kutokana na kuwa Zanzibar ndio yenye vivutio vingi na fukwe zake ni nzuri.

(a) Je, ni watalii wangapi wameingia katika kipindi hiki cha miezi sita (6) hadi hivi sasa.

(b) Je ni kiasi gani cha fedha zilichopatikana kwa kipindi hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 84 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa kipindi cha Januari – Septemba, 2017 Zanzibar imetembelewa na wageni wapatao 345,510 sawa na ongezeko la asilimia 18 kwa kipindi kama hicho mwaka 2016.

(b) Mhe. Spika, mapato yanayotokana na watalii ni kodi na tozo za malipo ya huduma mbalimbali za utalii ikiwemo malazi, chakula, usafiri, vivutio na vinywaji ambazo hulipwa katika taasisi tofauti za umma. Kwa msingi huo ni vigumu kwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kujua fedha zinazopatikana kutokana na uingiaji wa watalii kama Mheshimiwa Mjumbe alivyohitaji. Hata hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, Ofisi ya Mtakwimu, Idara ya Uhamiaji na Wizara ya Maliasili na Utalii hufanya utafiti kila mwaka wa kujua mapato yaliyopatikana kutoka kwa wageni waliongia nchini kwa mwaka husika. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a. Mhe. Spika, utaratibu wa makundi ya watalii wanaoingia Zanzibar kulipia baadhi ya malipo wanakotoka kunaikosesha fedha nyingi serikali yetu. Je Wizara yako inalijua hilo.

b. Nini maana ya tozo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) yote kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:

a. Mhe. Spika, ni kweli kwamba Wizara inafahamu suala hili kwamba watalii wanaingia makundi kwa makundi na wanalipa ada mbali mbali katika *Airport* zetu lakini na kwa upande wa bandari.

b. Mhe. Spika, maana ya tozo, tozo ni ile *fee* ya malipo ambayo wanatoa wageni wale wanapoingia katika sehemu zetu za makumbusho na sehemu nyenginezo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona mimi, nikushukuru sana.

Mhe. Spika, kwa kuwa wiki iliyopita Mhe. Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayesimamia masuala ya utalii na maliasili Dkt. Khamis Kigangwala alitangaza Kamati ya Kitaifa ambayo ilijumuisha watu 16 wenye fani tofauti ili watakaosimamia katika mpango Mkuu wa kuitangaza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini hata hivyo siku ya Jumapili akatangaza majina matano ya Wazanzibari, huku Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa haina taarifa.

a. Je, serikali inatoa kauli gani juu ya suala hili ambapo imeelekea kuporwa madaraka yake.

b. Kumekuwa kwa muda mwingi sana Zanzibar imekuwa inakosa uwakilishi hasa unaostahiki katika maeneo ambayo matamasha tofauti hufanyika kwa mfano *World Travel Market* Uingereza pamoja na *ITB Berlin*, Indaba *South Africa* ni kitu gani ambacho kinaifanya Wizara hii kushindwa kupeleka ushiriki wa nguvu ili kuitangaza Zanzibar kwa miaka mingi, hatimae kuonyesha kwamba sisi pia ni wadogo au tuko chini kuliko wenzetu Tanzania Bara. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa kuweza kujibu maswali kwa ufasaha kabisa kama alivyoelekezwa.

Mhe. Spika, napenda nichukue fursa hii kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Simai Muhammed ametaka kujua uteuzi uliofanywa na Mhe. Waziri wa Maliasili na Utalii.

a. Uteuzi uliofanywa na Mhe. Waziri wa Maliasili na Utalii kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya uteuzi kwa mujibu wa taratibu zake na kanuni za Wizara yake zinavyomuelekeza na sheria za utalii na maliasili zinavyomuelekeza. Sisi kama Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo tunaendelea kuwasiliana nae ili kujua kwamba Kamati zinazoundwa kama ni za Muungano, kama zinahusiana na suala zima la muungano kwa hivyo tukae pamoja ili tuweze kuwasilisha majina ambayo yatapaswa kabisa kuwa na uwiano katika kuziteua Kamati hizi.

b. Mhe. Spika, suala lake la pili kuhusu nguvu ambazo zinatakiwa kuongezwa katika kuutangaza utalii ni kweli. Lakini Mheshimiwa atakumbuka kwamba bajeti tunazipitisha hapa hapa kima cha bajeti sisi ndiyo tuliyokipitisha, kwa hivyo tunatangaza utalii kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa kwa mwaka. Ni vyema kwa mwaka huu hivi sasa bajeti zikaongezwa kwa sababu manufaa yameanza kuonekana. Ni wazi kwamba katika matangazo tuliyoyafanya na nguvu tulizozifanya katika nchi alizozitaja zikiwemo

Marekani, Uingereza, India na nyengine zimeleta mafanikio makubwa sana. Tarajio letu kufika lengo la 2020 kuwa na wageni au watalii ndani ya nchi yetu wapatao 500,000 tunatarajia kulifikia lengo hilo mwaka 2018 kama inavyotangazwa inaweza kukusanywa hivi sasa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 101

Utanuzi wa Hospitali ya Chake Chake

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendeleza na kujenga Hospitali mpya lakini katika mji wa Chake Chake, Hospitali ya Chake ipo mjini na eneo ni dogo na majengo yake yote ni ya kawaida lakini kuna fedha zimeshatengwa za kuyakarabati majengo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga hospitali kuwa ya ghorofa ili kukidhi haja ya hospitali hiyo.

(b) Je, Serikali haioni kuikarabati hospitali hiyo na baadae ije ivunjwe ili kuitanua kwa ghorofa ni bora ikafanya uamuzi wa busara kukusanya fedha za kuijenga kwa ghorofa kuliko hasara mara mbili.

(c) Je, serikali haioni umuhimu wa kulitumia eneo la hospitali hiyo vizuri ili likidhi haja ya kutumika kwa karne na karne.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru na naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote tukiwa hapa wenye afya njema na wazima.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam 101 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Afya imepokea pongezi zake Mhe. Suleiman Sarahan Said pamoja na ushauri wako mzuri kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya kulingana na idadi kubwa ya wananchi wanaohitaji huduma hizo kwa Hospitali ya Chakechake kule Pemba.

Aidha, Wizara ina azma ya kupanua Hospitali hiyo ambapo hatua za awali zimeshaanza kuchukuliwa ili kukidhi haja ya utoaji wa huduma hizo kutokana na ongezeko la watu siku hadi siku. Hatua hizo ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kujenga ghorofa kwa kupima uwezo wa ardhi iliyokuwepo hapo pamoja na katika eneo hilo.

Mhe. Spika, kweli ni vyema kutumia fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa ghorofa kuliko kukarabati eneo husika. Hivi karibuni kulifanyiwa vipimo kwa eneo lote husika na

wataalamu wetu wa serikali ambao walikwenda huko kwa pamoja na hivi sasa wapo katika tathmini ya vipimo hivyo na tunasubiri ripoti yao ili tufanye uamuzi wa mwisho. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Waziri Afya kwa majibu yake mazuri sana ambayo yananitia moyo kweli kweli.

a. Mhe. Spika, nataka nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwa yeye kama anavyoifahamu hospitali ya Chake chake, lakini sasa hivi kwa muda mchache unaofuata hospitali ile itazungukwa na majumba. Je, hospitali ile ameipima ina urefu na upana wa kiasi gani kwa upande wa kwendea kwa Makamu wa Pili wa Rais au kwa nyuma kichwani.

b. Mhe. Spika, kutokana na mchoro ambao kwa sasa hivi tunasema tuna mipango miji, je, Mheshimiwa amelizingatia hilo kutokana na ujenzi wa ghorofa zake.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilsihi suali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

a. Kama nilivyosema hapo awali na nitapenda kurudia tena tathmini wameshafanya kitaalamu kuangalia *soil, structure, square miter* eneo lote lile na kadhalika, ilikwenda timu yetu ya Wizara ya Afya pamoja na timu kutoka Wizara ya Ujenzi kwa pamoja. Hayo yote yatakuja katika hiyo ripoti itakayowasilishwa.

b. Lakini kwenye afya kuna kitu mara nyingi wanaita *demographics* ni pale watu ambapo wanapendelea kwenda kupata huduma zaidi. Hivi sasa hivi mfano kule Hospitali ya Abdalla Mzee ni hospitali kubwa yenye vitanda vingi, huduma zipo nyingi zaidi, tumepeleka madaktari wengi, wengine kutoka Unguja na juzi wengine wapya tumewapeleka pale. Lakini bado malalamiko ya kwao kule ni kwamba wagonjwa wanakwenda Chake Chake kuna *congestion* kubwa sana kuliko Mkoani na hii ni kutokana na *pulling power* ya *demographics*, yaani wale wananchi wenyewe.

Haya yote tutayachukulia kama ni mawazo kwa sababu pale ni kati kati na ndiyo mjini na Mheshimiwa yeye ndiyo Mwakilishi wa pale, ile ndiyo kama *capital city* ya Pemba pale. Kwa hivyo ni kweli pale huduma pale zinakwenda kwa wingi sana na nafasi iliyokuwepo ya ku-*expand* pia ni ndogo. Kwa hivyo yote hayo yakishakuletwa kwenye ripoti tutazingatia tunafanya nini na ni eneo gani na tutawasilisha pia serikali ili Serikali Kuu ifanye uwamuzi wake kwa eneo lote lile.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza suali dogo la nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa ufanisi wake wa ujenzi wa mahospitali yetu. Lakini katika pita pita yangu asilimia 90 ya mahospitali yetu yanavuja sana kutokana na ujenzi mbovu wa ma-*contractor*. Je, amejipanga vipi katika kuhakikisha ujenzi wa hospitali ya Chake Chake hiyo itakayojengwa baada ya kufanikiwa kupata hivyo vipimo

itakuwa haivuji wala haitokuwa na *crack* za haraka katika kuwachukua makandarasi ambao hawafai.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza namshukuru kwa swali zuri sana. Ni kweli baadhi ya maeneo hutokezea mara nyingi kuvujiwa na hiyo hutokana na bati lile kutumika ama lilokuwa la miaka mingi na kukarabati au matengenezo yalikaa muda mrefu hayakufanywa. Sasa hivi yote hayo tumeyachukulia katika mpango wetu mkuu wa kufanyia ukarabati ambao mpango wa ORIO unaendelea kwa vituo vidogo vidogo, lakini kuna mpango wa kupandisha hadhi pia hospitali hizi zote za Wilaya kuwa za Mkoa na za Mkoa sasa kuwa za rufaa. Kwa hivyo katika mpango huo tunaendela na *system* ya kufanya *repair*. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kuniona, kwanza kabisa niipongeze Serikali ya Zanzibar kwa huduma bora za afya zinazoweza kutolewa katika nchi yetu.

Lakini pamoja na majibu marefu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, pamoja na udogo wa hospitali ya Chake Chake kumekuwa kunafanyika *camp* mara kwa mara za madaktari kutoka nje zikiwemo za koo ama ENT na nyengine nyingi, lakini madaktari wale wanaweza kutoa pesa zao mfukoni za kuwapa wagonjwa waje Unguja kufanya *test* ya *T3, T4 ya thyrotoxin* je, serikali ina mpango gani wa kuweza kupeleka *test* hizo katika maabara ile ya Chake Chake.

b) Kwa sababu wa madaktari hawa wa *WAMI* Umoja wa Kiislamu wa *Jeddah* na wengine wa *Norway* na wengine wamekuwa wakileta dawa zao moja kwa moja na ukifika *Airport* zinatolezwa tozo kubwa, je Serikali ina mpango gani wa kuowaombea kibali ili wakija na dawa zile ambazo wanawapa wananchi bure kusamehewa ushuru.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika nakushukuru naomba nimshukuru sana Mhe. Mohamed Said Mohamed na kujibu pia swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo kwa kweli maswali mazuri sana.

Ni kweli pale Chake chake kuna upungufu katika *laboratory* hilo ni kweli kabisa na pia kuna upungufu wa kitaalamu na Mhe. Mohamed Dimwa yeye ni mtaalamu bingwa anayajua hupatikana hawa wataalamu wa *laboratory* sio kazi rahisi wale waliobobea. Kwa hivyo hivi sasa pale Pemba wamepelekwa juzi nimeambiwa wataalamu kama watatu upande wa *laboratory* lakini ngazi ya tatu sio wataalamu bingwa katika hii *recruitment* mpya.

Naomba niseme kwamba tutaaendelea kuimarisha huduma za *laboratory* na tutaendelea kutafuta wafanyakazi ambao wataweza kuchukua nafasi ya kuzihudumia *laboratory* zile. Mhe. Dimwa atakuwa anajua kwamba Abdalla Mzee kuna baadhi ya vifaa ambavyo tumeletewa hadi hii hawajapatikana wataalamu wakuweza kuvitumia. Hivi sasa tuko

mbioni kuhakikisha kwamba angalau kwa wiki wanakwenda wataalamu kutoka Unguja kwenda kufanya *text* pale Pemba na baada ya hapo kurudi tumeanzisha mpango huo.

Wakati huo huo tukiwatafuta wataalamu katika soko la ajira kwa kutangaza nafasi hizo ili tuweze kuwapata wataalamu hao na kuimarisha maabara zetu.

Lakini pili ni kweli hawa ndugu zetu wa *WAMI* kutoka Saudi Arabia Shirika hili la *WAMI* na madaktari wao wamekuwa wakitupa msaada mkubwa sana na kweli baadhi ya wakati hutokea tatizo lakini mara hii tunashukuru Mwenyezi Mungu tumetoa barua tayari Wizara ya Afya kuwaandikia ndugu zetu na wenzetu wa *Airport* na Mamlaka husika zilizo pale *Airport* ili waruhusiwe kuingia na dawa na dawa zao na vifaa. Wakati mwengine tatizo linakuwa ni la *security l*a kiusalama kwa sababu vile vifaa wanavyokuja navyo vya vyuma na kutanulia na kujaribia na kadhalika. Sasa taaluma ile ya kuvitambua vifaa vile inakuwa haipo *Airport* na wenzetu huwa wanashutuka baadhi ya wakati kutokana na vifaa vile.

Kwa hiyo tumeshawaandikia barua na tumeshawathibitisha kwamba hawa ni madaktari ambao tunafanya nao kwa karibu sana wanakuja na dawa zao pamoja na na vifaa vya kufanyia *operation.* Nashukuru pia kwamba vifaa vingi wametuachia sasa hivi pale Pemba wametuachia vifaa vya *theatre*, wamaetuachia vifaa vingi sana na dawa nyingi pia na bahati nzuri tumefanya hafla maalum ya kuwashukuru pale ofisini kwangu na kuwatunukia vyeti wote madaktari wale vya shukrani. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 27

Uwekaji wa Taa za Kuongozea Magari Katika Maeneo ya Makutano ya Barabara

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:

Katika malengo yake ya mwaka 2017/2018 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ilipanga kuweka taa za kuongozea magari *(Traffic Lights)* katika maeneo ya makutano ya barabara ya *Muzammil Center*, Mtoni na kwa Jumapweza kwa Unguja, Mtemani na Chachani *(PBZ Junction)* kwa upande wa Pemba.

Je, mpango huo umefikia wapi utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Kiwani swali lake Nam. 27 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji katika mwaka huu wa Fedha 2017/2018 ilipanga kuweka taa za kuongezea magari *(Traffic Lights)* katika maeneo ya Makutano ya Barabara ya Muzammil Center, Mtoni, kwa Jumapweza, Mtemani na Chachani kwa upande wa Pemba.

Mpango huu kwa sasa upo katika hatua ya kutangaza Zabuni na Wakandarasi baada ya kutangazwa tanakaribisha wale wote wenye uwezo wa kushiriki katika zabuni hiyo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa hivi sasa tuko nusu ya mwaka wa bajeti na kwa kuwa hivi sasa ndio hatua zinaendelea lakini je, hiyo hatua ya kutangaza zabuni itatangazwa mwezi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mussa Foum swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kama alivyosema kuna taratibu ambazo zinatakiwa siye lazima tufanye na baada ya kuzifata hizo taratibu wakati wowote kama nilivyosema tutatangaza hiyo *tender* na asiwe na wasiwasi kwa sababu hiyo kazi tumetoA ahadi ya kuifanya kupitia Baraza hili la Wawakilishi na *Inshaallah* tutaifanya. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kama tunavyofahamu sasa hivi sasa hivi kwamba gari zote za abiria zinakatiwa leseni za biashara kwa ajili ya kufanya kazi katika miji yetu lakini cha kusikitisha katika eneo la Chake Chake Chachaani ambapo panazungumziwa pale kituo ambacho kila siku madereva wanafukuzana na watu wa Halmashauri pamoja na Mawasiliano kwa kuwakataza wasiweke gari zao pale.

Pia tukizingatia sasa hivi eneo la Chake chake hamna sehemu maalam ya *packing* ambayo inatosha kwa ajili ya magari yake ambayo watu wanalipia. Jee Wizara yako na Wizara husika ni lini itakaa kitako na kufikiria swali hili la maegesho ya magari ambayo wanalipia pesa zao kwa ajili ya huduma hiyo ili waondokane na usumbufu ambao wanaupata.

Mhe. Spika: Mheshimiwa swali lako jipya lakini kama unaweza kujibu Mhe. Naibu Waziri mpe majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Zulfa Mmaka swali ambalo pia jana liliuliziwa na Wizara husika lilijibu.

Kama ulivyosema tunajua kwamba kuna changamoto hiyo na tulikaa sisi na Wizara ya Ardhi na vile vile Tawala za Mikoa na mwanzo tuliona kuna eneo la gombani lakini

baadaye wale wenyewe wenye magari lile eneo bado itakuwa ni tabu kwa watu ambao wanakuja mjini Chake Chake.

Kwa hiyo kama alivyosema tunaendelea kukaa na kutafakari pamoja na wadau ili kuhakikisha kwamba hili tatizo ambalo kweli lipo na mimi juzi nilikuwa Pemba tunalifanyia kazi kwa haraka zaidi sana. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 53

Malipo ya Minara ya Kuongozea Meli kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania Bara (*TPA*)

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa Shirika la Bandari Zanzibar linamiliki Minara ya kuongezea Meli za Kimataifa, kama Kigomasha na Matumbini iliyopo Pemba na mnara wa Mwana wa Mwana Chumbe, Kizimkazi na kadhalika iliyopo Unguja, na kwa sababu Mamlaka ya Bandari Tanzania ndiyo inayolipwa fedha hizo na baadae kuzigawa kwa Shirika la Bandari Zanzibar.

a) Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho kinastahiki kulipwa Shirika la Bandari Zanzibar kutoka Mamlaka ya Bandari Tanzania.
b) Je, ni muda gani ambao Shirika la Bandari Zanzibar halijapokea fedha kwa ajili ya malipo kwa matumizi ya minara hiyo kutoka Mamlaka ya Bandari "THA" Tanzania.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa naiba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Omar Seif bin Abeid swali lake Nam. 53 kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, naomba kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa, Shirika la Bandari kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kwa pamoja wanakusanya malipo yote ya matumizi ya minara mikubwa inayotumiwa na meli za kigeni. Baada ya kukusanywa mapato hayo kwa kila miezi mitatu kila upande hufanya hesabu zake na kulipanana kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa ambapo asilimia 40.6 yanakwenda kwa Shirika la Bandari na asilimia 59.4 kwa Mamalaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania. Kwa wastani huo, Shirika la Bandari hupata kiasi cha Tshs.300,000,000 kwa kila kipindi cha miezi mitatu na kwa mwaka sawa sawa na bilioni 1.2.

b) Katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Septemba, 2017, Shirika la Bandari halijalipwa mapato yake yanayostahiki kutokana na huduma hizo kutoka Mamlaka ya Usimamizi Bandari Tanzania ambapo suala hilo linaendelea kujadiliwa baina Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ya Zanzibar pamoja na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi

na Mawasiliano ya Tanzania ili kulipatia ufumbuzi suala hili ambalo hata sisi kusema la ukweli tunaliona umuhimu wake, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri yenye muwelekeo lakini nilitaka nimuulize swali dogo lenye vifungu viwili (a) na (b).

1) Mheshimiwa kwa kuwa umekiri na umeeleza kwamba Shirika la Bandari huwa linapata kiasi ya shilingi milioni 300,000,000 kutokana na malipo hayo yanopatikana kutokana na minara hiyo ya nje inayotumiwa na meli za kigeni na kwa kipindi kama ulivyoeleza cha Januari 2016 mpaka leo bado pesa hizi hazijapatikana milioni 300,000,000 ukifanya hesabu ni miezi ishirini na mbili ukigawa kwa saba inakuja milioni 300,000,000 x 7 karibia bilioni 2,100,000,000 bado Shirika la bandari halijalipwa kutoka THA.

Sasa na bado mazungumzo yanaendelea lini ufumbuzi wa suala la THA kuilipa Shirika la Bandari la Zanzibar pesa zinazo stahiki litapatiwa ufumbuzi ili Shirika letu nalo liweze kupata pesa hizi liweze kununua na kukidhi mahitaji yake wakati tuna mahitaji mengi na sisi hapa.

2) Lini ufumbuzi katika vikao vyenu mutakaa ili kama ikiwezekana kila sehemu ikalipwa moja kwa moja kwenye akaunti yake. Ahsante sana Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Omar Seif bin Abeid swali lake kama ifuatavyo:-

Nategemea tutapoenda Dodoma tutakuta na Mhe. Waziri wa Ujenzi ili kujadili hili suala kama unavyosema, nilikutana mara ya mwanzo pamoja ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano na tumekutana naye juzi katika vikao vyetu vya kawaida vya kero ya muungano na keshokutwa tukienda Dodoma tutakutana naye, kwa hiyo wakati wowote tutapata ufumbuzi na tutaleta majibu katika Baraza lako Tukufu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona mimi nikushukuru sana.

Mhe. Spika, kwa kuwa hii minara ambayo imejengwa katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba mengine ina historia ambayo ingeweza kusaidia kwa njia moja au nyengine kuchangia katika soko zima la suala la Utalii. Namuuliza Mhe. Waziri ni utaratibu upi anautumia wizara yake ili kuhakikisha kwamba kumbukumbu za minara hii inatambulika kwa kushirikiana pamoja na Wizara ya Utalii ili wageni wanaokuja kutembea mbali mbali waweze kutambua hii historia ambayo tuliyokuwa nayo ambayo ni adimu hasa ambayo wanakuja kuangalia kwenye masuala ya *marine* pamoja na *culture tourism.* Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa naiba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said Mwakilishi Wananchi Jimbo la Tunguu swali lake kama ifuatavyo:-

Kwanza nataka kumwambia kwamba minara hii ipo sehemu ambazo inatakiwa uende kwa mujibu wa upepo unapotokea, kwa hiyo ni sehemu hatari kwenda, sisi pamoja na kamati kama mara mbili tulitaka kwenda tukashindwa kufanya hivyo kutoka na upepo unapokuwa unavuma kipindi hichi.

Kwa hiyo nataka kumwambia tuu bado hatujakuwa na hatua hiyo ya kuifanya hili jambo kuwa la utalii na watu kwenda kutembelea kule kwa sababu ni hatarishi, lakini tutakaa na wizara husika kama itakavyoonekana kuna haja hiyo basi tutafanya hivyo lakini bado ni sehemu hatarishi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa wakati wa maswali na maswali pia yamemalizika. Kuna tangazo la wageni. Wageni ambao tunao wanatoka *International School of Zanzibar* ni wanafunzi wa darasa la tano na sita. Jumla yao ni ishirini na nane (28), *'Student from the International School of Zanzibar you are most welcome to the Zanzibar House of Representative'*

Pamoja na wanafunzi hao wamefuatana na walimu wao:

1) Babrat Steven
2) Jennifer Gilmo

Wamefuatana pia na mwalimu wao Salama Othman *'you are most welcome'* karibuni sana ahsante sana.(*Makofi*)

Kabla ya kuendelea na hoja inayofuata sasa naomba nimwite Mwenyekiti aje anipokee ili tuendelee kuchangia mswada wetu Mhe. Mwenyekiti karibu sana.

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alikalia kiti

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uchaguzi Namba 11 ya mwaka 1984 na Kutunga Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2017 na Masuala Mengine Yahayohusiana na Hayo

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea sasa naomba nimwite Mhe. Hassan Khamis Hafidh akifuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame ajiandae.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua fursa hii ya kukushukuru wewe kwa kunipatia muda na mimi wa kuchangia mswada uliokuweko mbele yetu mswada muhumu wa kuweza kuleta maendeleo katika nchi yetu na kuyaendeleza mapinduzi matukufu ya Januari 1964 kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar Wakulima na Wakwezi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo naomba nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Baraza lake la Mapinduzi kwa kuona kuna umuhimu wa kuleta mswada wa aina hii katika kuendeleza mapinduzi matukufu ya Januari 1964. Kwani huu mswada wa mabadiliko wa Tume ya Uchaguzi ni mswada muhimu kwa maendeleo ya Zanzibar na kuimarisha mapinduzi matukufu.

Lakini tatu nichukue fursa hii kumshukuru mwana mapinduzi mtetezi wa wakwezi na wakulima Mhe. Jecha Salim Jecha kwa kufuta uchaguzi baada ya kubaini mijizi imetuibia katika uchaguzi uliopita.

Mhe. Mwenyekiti, nne nachukua fursa ya kumshukuru Mkurugenzi wa Tume ya Uchanguzi Ndugu yangu Salum Kassim Ali mwana mahesabu mzuri aliyesomeshwa Lumumba na Mwalimu wa zamani Hazadi Kidongochekundu, Mwalimu Charamila na wengine. Aliyesomeshwa hesabu na kuhitimu baada ya kujua kwamba wezi wametuibia katika uchaguzi uliopita wa 2015 na kumuambia na kumuomba Mwenyekiti wa Tume hiyo Mhe. Mwanamapinduzi Salum Jecha Salum kuufuta uchaguzi na akafanya hivyo kwa maslahi ya wana mapinduzi wa Zanzibar Wakwezi na Wakulima. Mhe. Mwenyekiti, leo tuko hapa salama tunafanya mambo yetu vizuri mijizi ile leo inalia inataka kuingia humu ndani lakini yaguju.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo sasa naomba kuchangia mswada lakini kabla ya sichangia mswada nataka kukumbusha jamii nataka kuwakumbusha wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi kwamba, maneno ya mwanamapinduzi mwenzetu hayati *Lennin* aliyekuwa Rais wa Urusi aliyefanya mapinduzi mwaka 1949 nchini Urusi.

Rais wa zamani wa Urusi Lennin alisema; haki ya kupiga kura ni haki ya kila mwananchi lakini haki ya kuhesabu na kutangaza ni haki ya Serikali naomba nirudie Lennin alisema, 'haki ya kupiga kura ni haki ya kila mwananchi lakini haki ya kutangaza na haki ya kuhesabu ni haki ya Serikali'.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba na Tume yetu ya Uchaguzi katika huu mswada twende na misingi hiyo kwanini kwa sababu hii ni nchi ya kimapinduzi, Urusi ni nchi ya kimapinduzi na nchi za kimapinduzi duniani ziko sita ikiwemo Zanzibar mambo ya kimapinduzi ni mambo ya nchi nyengine ni tafauti mambo ya kimapinduzi yanakuwa ya kimapinduzi, mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, tunaiona Korea ya Kusini, tunaiona China, tunaiona Iran, tunaiona Cuba, tunaiona na nchi nyengine zote za kimapinduzi na Zanzibar ikiwemo lazima tuendeshe nembo na msingi yetu kimapinduzi. Kama ningekuwa naruhusiwa kusema basi ndani ya Baraza hili leo ningethubutu kusema 'Mapinduzi Daima" lakini siruhusiwi.

Mhe. Mwenyekiti, naanza kuchangia ukurasa wa 15 ukurasa wa 167 namba 15 kila Chama cha Siasa kinaweza wakati wa uandikishaji kuteuwa mwanachama wake mmoja ambaye atandikisha au awe na sifa za kuandikisha kuwa mpiga kura kuwa wakala wa uandikishaji katika Shehia.

Mhe. Mwenyekiti, hii naiomba isiwemo katika mswada huu wa sheria nataka kumbushe tena maneno ya Lennin kasema, haki ya kupiga kura ni haki ya kila mwananchi kuhesabu na kutangaza ni haki ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona jinsi tunavyoingiza wanasiasa katika kila pahali Sheria ya Tume ya Uchaguzi ulipita ilikuwa inasema Rais ili ateuwe kitu gani ashauri kiongozi wa siasa, Rais sijui afanye hivi amshauri kiongozi wa siasa, hivi Rais wa nchi ya mapinduzi anashauri, shauri inamhusu nini kushauri Rais ndio Rais hata kunako Kur-an katajwa hatakiwi kushauri.

Sasa leo hii kazi ya Serikali sisi tunakwenda kuwapa wanasiasa hebu tujiulize katika vyumba vya kuandikisha kupiga kura, vyama vingapi vya siasa viko Tanzania kila chama kikileta wakala mmoja tukimuingiza watakuwa mawakala wangapi, halafu si ugomvi unakwenda kuuleta katika kila chumba cha kupiga kura.

Mhe. Mwenyekiti, Sheha anatosha kuwepo katika chumba cha kupiga kura, wanasiasa hapa si kwao si jukumu lao wanasiasa wasubiri katika kupiga kura katika kura kuchagua kiongozi wao lakini kumuingiza wakala wa chama cha siasa katika chumba cha kuandikisha kupiga kura hii tunakosea nasema tena hii tunakosea. Wakala wa kupiga kura hatakiwi tu kuwemo katika chumba cha kupiga kura, hii ni kazi ya serikali sheha anatosha kuwemo katika chumba cha kupiga kura, wakala hana nafasi. Kama alivyosema Lenin jukumu la kupiga kura ni la kila mwananchi.

Sasa leo utaenda kumuandikisha wakala wa chama katika kuandikisha ana kazi gani, jukumu lake ni nini, jamani tusikosee hii kila kitu kumuingiza mwana siasa, mwana siasa kila pahali hii haitufai. Nchi yetu ni ya Kimapinduzi, tunafuata mfumo wa vyama vingi tuone leo na kesho, wakala wa siasa hafai kuwemo katika chumba cha kupiga kura. Naomba sana Mhe. Waziri uliangalie hili, hii Nam.15 iondoke hafai kuwemo hii ni kazi ya serikali, sheha ndio mtu wa serikali anatutosha kuwemo katika chumba cha kuandikisha kupiga kura, hatutakiwi kuwaingiza wana siasa kila pahali kuna mahala mwake. Hilo moja.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu Nam.16(e) inasema muombaji, “watu wafuatao wataruhusiwa kuwemo katika kituo cha uandikishaji:. Halafu ukienda (e) 'muombaji', naomba iwe anayeomba kuandikishwa isiwe muombaji, naomba iwe hivi.

Mhe. Mwenyekiti, tukitoka hapo nakwenda katika kifungu cha 43. “Kwa kuzingatia masharti ya Katiba, mtu atakayekuwa na sifa za kuteuliwa kuwa mgombea wa urais iwapo:

Ni Mzanzibari wa kuzaliwa, *this is good*.

Mhe. Mwenyekiti, lazima azaliwe Zanzibar ndio tumjue Mzanzibari na ndio tumpe urais wa Zanzibar. Kama mtu kazaliwa alikozaliwa aah! Hapa hatufai lakini ametimia umri wa miaka 40. Rafiki yangu niliyempenda kuliko wote Robert Mugabe yeye ana miaka 70 *plus*, na juzi wakamfukuza uraisi, bado anafaa na bado anaweza lakini ah, anaambiwa mzee, sawa. Sasa basi kama tumeweka umri wa miaka 40 tunaonaje tukaweza na *limit* yakum-*limit* mtu, ingawaje kwa kipindi tulichonacho tutaambiwa tunaogopa, tutaambiwa hivi lakini ukweli hatuwezi kuwa na Rais tena ashavuka miaka 80 *plus* au miaka 75 au 70 *plus* aah.

Sisi tunataka Rais wa kuja kufanya nae kazi, tunataka Rais wakuja kuitumikia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hatutaki Rais wa kuja kumtibu iwe tena kama Rais wa nchi fulani za Kiafrika kila siku yuko Uingereza kwenye matibabu. Sisi hatutaki hayo, sisi tunataka mtu mwenye nguvu, mtu mwenye siha aje kufanya kazi keshafika tena miaka 75 sisi hatufai. Sisi hatuji kutafuta mtu wa kumtibu, sisi tunakuja kutafuta Rais wa kufanya nae kazi, wa kuhangaika nae katika kuwaletea wana Mapinduzi maendeleo ya wakwezi na wakulima. Hatutafuti mtu wa kuja kumpa *charity* ya matibabu, aah sisi hatuna *charity* ya matibabu sisi tunataka mtu wa kufanya nae kazi.

Mhe. Mwenyekiti, tukitoka hapo tunakwenda kifungu cha 66 kinasema. “Wakati wa kipindi cha kampeni, kila mgombea atakuwa na haki ya kurusha hewani ilani ya chama chake kupitia vyombo vya habari vya umma”.

Mhe. Mwenyekiti, tujiulize Zanzibar tuna mfumo wa vyama vingi, leo tunaitia katika sheria, vyombo vya habari vya umma ni vyombo vya serikali basi ndio tumpe tu ruhusa wewe nenda tu kwenye chombo cha habari cha umma kaseme tu unavyotaka, tutakuja kuleta ugomvi. Lazima tuweke kipengele kinachosema kwa kufata matakwa na kanuni na taratibu za shirika hilo. Anakwenda *ZBC* anasema leo mkutano wangu wa Chama cha TADEA nirushieni tu kwa sababu imo ndani ya sheria aah!. Lazima afate matakwa yao, lazima aombe, aridhiwe, afanye nini lakini leo tena imo kwenye sheria tena atakwenda tu aseme nirushieni mkutano wangu kama hamtaki itakuwa mnavunja sheria. Lazima hapa turekebishe tuseme kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria zilizowekwa na taasisi hiyo, isiwe mtu unampa tu kwa mujibu wa sheria. Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 66 mimi yangu ni hayo.

Mhe. Mwenyekiti, tukitoka hapo tunakwenda katika kifungu cha 82. Kidogo kwenye kifungu hiki kwenye maandishi madogo haya kura ya, imekosewa imeandikwa “mapena”. Kwa hiyo, naomba hapa irekebishwe iwe “mapema” kwenye maandishi madogo upande wa mkono wa kulia.

Mhe. Mwenyekiti, tukotoka hapo twende kifungu cha 93. "Msimamizi wa uchanguzi, kwa kufuata miongozo ya Tume ya Uchaguzi yenyewe ya Wilaya yake kuwa kituo cha majumuisho kwa ajili ya majumuisho ya kura". Mhe. Mwenyekiti, hapa napenda sana niipongeze hii *proposal* ya sheria tunayoipitisha leo niipongeze sana.

Mhe. Mwenyekiti, tulikotoka uchaguzi uliopita yalikuwa maajabu makubwa. Ukisema maajabu makubwa kwa sababu ilikuwa utaratibu uliokuwepo tume inapofika wakati wa kura wanaajiri ofisa wa jimbo. Ofisa wa jimbo huyo hafanyiwi *vetting*, ofisa wa jimbo huyo hajuulikani anatoka popote anaomba akishakuomba anaweza aka-*lobby* akapata na akishakupata anapewa ofisa wa jimbo. Ah! Ndio mwenye mamlaka ya kunitangaza mimi hasa Hassan Khamis Hafidh niliyofanya kazi kwa miezi sita ya kushinda Jimbo la Welezo mpambe anapewa mamlaka ya kunitangaza, mpambe si muajiriwa wa serikali kaomba tu *temporary* anapewa.

Nasikia kuna jimbo moja kapewa pesa chungu nzima baada ya kupewa pesa akamtangaza asiyeshinda, si keshapewa milioni 25 au 30 halafu akatiwa ndani ya gari huyo anakimbia. Lakini leo kwamba Afisa wa Wilaya ambaye ni muajiriwa wa serikali ndio amepewa jukumu la kumtangaza mshindi. Hapa kweli tumefata maneno ya Lenin kwamba jukumu la serikali ni kutangaza na kuhesabu kura, lakini zamani utaratibu ule ndio utaratibu uliotuumiza, utaratibu mbovu leo sheria hii imekuja kuurekebisha, *wallahi* napasifu sana na tusirudie tena na tuujue utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipata bahati ya kusimamia uchaguzi wa Kenya, zote mbili. Mimi sijaona matokeo ya Rais kutundikwa kwenye mabao na pia nishashuhudia nchi zilizoendelea chaguzi zao tofauti, sijaona mimi. Matokeo ya Waziri Mkuu Uingereza au matokeo ya Waziri wa Marekani kubandikwa katika majimbo. Tunabandika katika majimbo matokeo ya Rais kwani jimbo ndio lilomchagua peke yake. Bandika matokeo ya diwani, bandika matokeo ya mbunge au mwakilishi wa jimbo lile, sio matokeo ya Rais. Matokeo ya Rais lazima yaende makao makuu ya tume yakatangazwe ndio sheria.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimamia chaguzi zote mbili za Kenya sikuona hata pahala pamoja palipobandikwa matokeo ya Rais. Matokeo ya Rais yalikwenda moja kwa moja katika Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndio yakatangazwa. Leo nchi hii ya kimapinduzi unakwenda kuyabandika matokeo ya Rais katika jimbo eti tunaita demokrasia, *what kind of democracy, that is not a democracy, that is abuse the democracy*.

Mhe. Mwenyekiti, tunaitukana demokrasi ya kimapinduzi kwenda kubandika matokeo ya Rais katika kuta mara mtu anakuja anabadilisha, mtu anakuja anafanya anavyotaka yeye hivyo sivyo. Matokeo ya Rais yakapelekwe kwa Jecha Salum Jecha ndio yatangazwe, mtu wa jimbo hahusiki hata kuyagusa ayapeleke moja kwa moja kwa Mhe. Jecha Salum Jecha mwana Mapinduzi, mtetezi wa wakwezi na wakulima.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika kifungu cha 127. Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hiki ni marufuku kwa mgombea, chama cha siasa, taasisi au mtu mwengine yeyote kutangaza matokeo ya uchaguzi kwa njia yoyote ya mawasiliano kabla ya kutangazwa rasmi na tume. Hicho ni kifungu cha 127(1).

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 127(2) kinasema, mgombea wa chama cha siasa, taasisi au mtu mwengine yeyote atakayetangaza matokeo ya uchaguzi au kuitaka tume kutangaza matokeo kabla ya kuisha kwa muda wa kutangaza matokeo uliopangwa, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atapata moja kati ya adhabu zifuatazo.

Sawa, ashatangaza na hapa alitangazwa, kuna mtu alifanya kazi ya tume, alifanya kazi ya Mheshimiwa mwana Mapinduzi Jecha Salum Jecha, lakini hakuna hata mtu mmoja aliyekwenda kumshtaki. Hakushtakiwa, polisi haikumshataki, tume haikumshtaki wala raia mwema hakutokea kwenda kumshtaki.

Hivyo nchi ya kimapinduzi mtu kayakashifu mapinduzi kenda kujitangaza, amefanya kazi ya tume, kazi ya kutumwa anakwenda kujitangaza yeye Rais katika nchi hii. Nchi nyengine ananyongwa. Juzi kaambiwa Odinga, kaambiwa wazi wazi na Mwanasheria Mkuu wa Kenya kwamba kama utajitangaza na utaapishwa kura Rais usisahau Katiba ya Kenya iko *very clear* tunakunyonga, basi mpaka leo kaingia mitini hathubutu tena kufanya chochote. Kenya unanyongwa, Iran unauliwa kwa risasi na *firing squad* ndio sheria yao, Uganda unanyongwa na nchi nyengine zote unanyongwa. Lakini hapa Zanzibar *okay* kosa tulilolifanya kwamba kulikuwa hakuna mwenyewe, hakuna mtu wa kwenda kumshtaki. Polisi hawakumshtaki wanasema si kazi yao ni kazi ya tume, hakuna raia mwema aliyekwenda kumshtaki kila mtu kanawa, nini si kazi yake ni kazi ya nani?

Mhe. Mwenyekiti, na Mhe. Waziri hii ni nchi ni ya kimapinduzi naomba kiongezwe kitu kifuatacho.

Naomb akiongewe kiwe nambari kiseme hivi:

"Tume au mtu mwengine yeyote atakayeona kama masharti ya kifungu kidogo cha 1 na cha 2 yamevunjwa atatoa taarifa kwa kituo cha polisi ili hatua za kisheria zichukuliwe". Hiyo ndio *point* ya kuongeza, kwa sababu sasa tutakuwa tumempa nguvu mtu, tumempa mwenyewe. Mwenyewe ni tume au msamaria mwema mwana mapinduzi mtetezi wa wakwezi na wakulima atakwenda kushtaki fulani amevunja maadili ya nchi yetu kenda kujitangaza yeye ni Rais.Keshakwenda kumshtaki tena majaji wataamua tunyonge basi tutanyonga, tupige *firing squad* tutapiga kwa mujibu wa sheria hiyo ndio nchi ya kimapinduzi inavyoendeshwa dunia nzima ushafahamu, tunanyonga basi imekwisha tutakuta akhera hakuna tatizo, kama hivyo ndio nchi ya kimapinduzi inavyokwenda hatuwezi kwenda tu kila siku kizembe zembe.

Naomba kipengele hicho kama mtakikubali waheshimiwa kwa maslahi ya wakwezi na wakulima wana mapinduzi wa nchi hii baada ya kufanya utafiti mkubwa naona kinafaa. Sasa itakuwa tume tumempa mwenyewe, Tume tumeipa meno, Tume tumeipa nguvu akitamka tu hata kama hajajitangaza, akitaka tu kujitangaza mbio Tume ishakimbilia polisi kamkamateni kwenda kumshtaki au mimi au mtu yeyote msamaria mwema wa mapinduzi kama mimi nitakwenda kusema katika kituo cha polisi fulani kakiuka maadili tukamkamate, atakwenda kukamatwa. Lakini iliyopita kulikuwa hakuna mkamataji kwa sababu hakuna mwenyewe, naomba kipengele hiki kwa heshima kubwa na taadhima

kubwa najua wazi waziri wa wizara hii ni mwana Mapinduzi, Mwanasheria Mkuu mwana mapinduzi na Naibu Waziri Mihayo ni mwana Mapinduzi hamtokataa hili. Kama mtakataa hili sijui mtakuwa mnawaweka wapi wana Mapinduzi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naomba niende katika kukata majimbo. Katiba 124(4) inatupa meno, katika kipindi cha miaka 8 kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984 kila mtu akamate Katiba asome. Katika kipindi cha miaka 8 hadi 10 au wakati wowote tume itachunguza idadi ya mipaka na majimbo hayo kwa kiwango kile ambacho inahisi ni wajibu kuangalia upya inaweza kwa kutoa tangazo kubadili idadi, mipaka na majina ya majimbo hayo. Kumbe tuna uwezo kikatiba sio lazima tusubiri miaka minane, kumi au mingapi aah, pana neno "au" wakati wowote tume itachunguza idadi kiunganishi au kinatupa nguvu kwa mujibu wa Katiba.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema aliyekata majimbo, yalivyokatwa majimbo tumefanya makosa, lazima majimbo hakuna haja ya kubadilisha Katiba wala sheria kwa mujibu wa Katiba hii, pana neno au wakati wowote. Kwa hivyo, kumbe Katiba inatupa uwezo mimi si mwanasheria lakini naona na ninafahamu akili yangu iko imara mimi ni *Diaspora* kwa hivyo *I know most of the things*. Kwa hivyo, madhali pana neno au hapa tunao uwezo wa kukata majimbo hata kesho tukiamua kwa mujibu wa Katiba. Kwa hivyo, majimbo haya tuyatizame upya na tukayakate upya atakayekuja na hoja tushindane kwa nguvu ya hoja kwa mujibu wa Katiba. Mimi niko tayari tusomeshane katiba asiyeijua katiba madhali pana neno au nafikiri Mwanasheria Mkuu kwa hili hutokataa wala hutobisha kwa hili kwa sababu katiba unayo mbele na pana neno au.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana lazima majimbo tu-*review* tena na tuyakate tena.

Mhe. Mwenyekiti, najua unataka kuniambia nisimame lakini muda wangu umebakia dakika nne na ninaziona vizuri, kwa hiyo naomba nizimalize dakika zangu nne.

Mhe. Mwenyekiti, ukitoka hapo tuna *observers* (waangalizi). Mimi nilipata bahati ya kuwa mwangalizi wa kimataifa katika uchaguzi wa Kenya wa tarehe 8 na uchaguzi wa marudio. Lakini ile ni nchi waliyopata uhuru kwa bendera shusha, bendera pachika kutoka kwa Muingereza, sisi ni nchi tuliopata uhuru kwa kupindua hatukupata uhuru wetu sisi kwa kushusha bendera huku na kutia saini aah! Sisi watu tuliwapiga mawe, mikuki, mishale mpaka tukapata hii nchi, ndio maana nchi yetu tunaiita nchi ya Kimapinduzi, Revolution government of Zaznzibar ziko sita Zanzibar ikiwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mwangalizi anaekuja kuangalia uchaguzi wa nchi ya kimapinduzi lazima iwe wa aina yake, sio aje tu na ushawishi wake huko Kenya sisi tuliwekewa vikwazo chungu nzima navijua vyote. Aje hapa alipe *fee*, akitaka kuangalia uchaguzi hapa muangalizi wa kimataifa alipe *fee* lakini pia apangiwe utakwenda kuangalia huku. Mimi nilipangiwa kuangalia Siaya, Kisumu ndio nilikopelekwa asubuhi nikapewa ndege na timu yangu tukenda Kisumu, tumepangiwa. Lakini hapa apangiwe asipange yeye na pia alipe fee ikiwa kuchukua fomu ya uwakilishi unalipa, fomu ya udiwani unalipa, fomu ya uraisi unalipa kwa nini yeye asilipe atoke kwao Uingerea, Marekani au Canada aje

hapa kwenye nchi ya kimapinduzi aangalie tu, haiwezekani. Mhe. Mwenyekiti, lazima alipe *fee* naomba sana na naamini kwa hili hamtolikataa waheshimiwa kulipa *fee*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia naamini mswada huu wa sheria uko vizuri lakini utakuwa vizuri zaidi kama tutazingatia marekebisho ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuliyoyaleta kwani sote tunajenga nyumba moja, sote tuna nia moja ya kuiona nchi ya Zanzibar inaendelea, ya kuona Mapinduzi Matukufu ya Januari, 1964 yanalindwa na kuona wakwezi na wakulima wa nchi hii wanapata maslahi yale yale yaliyokusudiwa kunako mapinduzi matukufu ya 1964. Mimi Hassan Khamis Hafidh, Mwakilishi wa Jimbo la Welezo (*Diaspora*) napenda sana kuunga mkono mswada huu na marekebisho yake kwa asilimia zote mia moja, kwani ni mswada wa kimapinduzi umesheheni lakini naomba marekebisho tuliyoyatoa yazingatiwe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja ya mswada na marekebisho yake. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hassan (*Diaspora*) kwa mchango sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma atafuatiwa na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi ajiandae.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kuweza kunipa nafasi hii nikaweza kuzungumzia hoja muhimu sana ya mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uchaguzi ya 2011 ya 1984 na kutunga Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 2017 pamoja na mambo mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningelishangaa sana tena ningelishangaa kweli kweli kama serikali wasingeweza kutuletea mswada huu wa marekebisho ya sheria ya uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, kila jambo lina historia yake, Zanzibar wenzangu walishazungumza historia ya uchaguzi ya Zanzibar ni tofauti na sehemu nyengine nyingi sana hapa duniani. Sasa waswahili wanasema “ukipigao ndio ukufunzao”. Mhe. Mwenyekiti, sote mashahidi tuliona vurugu, udanganyifu, ubabaishaji uliojitokeza katika uchaguzi wa mwanzo uliopita. Kwa kweli ilikuwa ni aibu kila mtu alikuwa anafanya anavyotaka katika lile eneo alilokuwepo utadhani serikali ilikuwa haipo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini baada ya kujiuliza na kutafakari na kuirudisha nchi yetu katika hali ya amani na utulivu tunaishukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Rais makini Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuweza kukaa na kutuletea mswada huu wa sheria ambao tukiupitisha sote kwa pamoja, pamoja na marekebisho yake utaweza sana kuondoa kasoro zote zile ambazo zilizojitokeza katika uchaguzi uliopita na chaguzi nyengine mbali mbali ili nchi yetu iweze kuwa na uchaguzi wa salama na amani.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja baada ya dibaji hiyo nilikuwa nataka niingie katika kuchangia mswada huu kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, mimi moja kwa moja nianze katika ukurasa wa 165 Kifungu cha 10 kinachozungumzia *marginal note* 'Uwezo wa Karani wa Uandikishaji'. Kifungu hiki kina karibu vifungu vidogo vitano (a) mpaka (e), lakini kitu ambacho nakusudia kukisema kwamba kifungu hiki kinasema 'Karani wa Uandikishaji atakuwa na dhamana ya shughuli za uandikishaji katika kituo na atakuwa na uwezo wa kufanya haya yafuatayo: Kumuamrisha Afisa Polisi, kumtoa katika kituo na kuhakikisha kuwepo kwa utiifu wa sheria na kufuatwa kwa maelekezo katika kituo cha kupigia kura".

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kifungu hiki ni muhimu sana, kwa sababu tumeshuhudia katika maeneo mbali mbali watu wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya ajabu mbele ya macho ya polisi.

Jana mwenzetu hapa Mhe. Waziri Asiye na Wizara Maalum alizungumzia ambaye ni Makamo Mwenyekiti wa Chama cha *ADC,*kwamba ilifika pahala kwa mujibu wa sheria za nchi kila chama na kila mgombea kinatakiwa kuweka mawakala wake, kwa bahati mbaya sana mawakala wa Chama cha *ADC* kama alivyosema yeye mwenyewe hasa katika Kisiwa cha Pemba kwa kweli walitolewa katika vituo kwa nguvu, wakapigwa, wakadhalilishwa barabarani na tuliona mpaka kwenye *clips* mbali mbali. Mtu mzima na heshima zake anavuliwa nguo anapitishwa barabarani anapigiwa ngoma. Kwa kweli ni jambo ambalo ni la fedheha katika nchi yetu ndio maana tukasema kwamba sheria hii lazima tuweze kuipitisha ili vitendo kama hivi visiweze kujirejea kwa mara ya pili. Kwa sababu kila chama kina haki yake ya kupiga kura lakini vile vile kupigiwa kura. Kwa hiyo, kama wewe umeshapiga kura basi usimbughudhi mwenzako.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nakuja katika kifungu hiki cha 12 kinachosema mtu atakuwa na sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura ikiwa ni Mzanzibari, lakini vile vile amefikia umri wa miaka 18. Vile vile ataonesha kitambulisho chake cha Mzanzibari Mkaazi kilichotolewa chini ya sheria zinazosimamia kitambulisho hicho.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo nataka niseme. Jana Mhe. Suleiman Sarahan Said alitoa mfano hai ambao aliuona yeye ndani ya jimbo lake, kwamba sheria inasema mtu ili awe na haki ya kupiga kura basi kwanza awe anakaa ndani ya jimbo si chini ya miaka mitatu (miezi 36) kwa mujibu wa sheria. Lakini vile vile aoneshe kitambulisho chake cha Mzanzibari na cha kupigia kura, leo kwa bahati mbaya sana maajabu yaliyokuwa yanafanyika mtu anakwenda na leseni eti leseni leo ndio mtu anaruhusiwa kupiga kura. Sasa mimi nadhani kupitia sheria hii tunayoipitisha na nashukuru sana huko mbele kuna kifungu ambacho nitakirejea baadae kilichoelezea kwamba sasa hivi vyombo vya ulinzi na usalama vitapewa nafasi kwa mujibu wa maelekezo ya Tume ya Uchaguzi kuweza kupiga kura mapema ili kuweza kusimamia sheria za nchi kila anaitekeleza wakati wa kupiga kura.

Kwa sababu tatizo linajitokeza kwamba askari wetu yuko katika kituo cha ulinzi matokeo yake anamwambia mwenzake hebu nishikie kidogo nakwenda kupiga kura, anakwenda kupiga kura anakaa karibu masaa sita ndio anarudi katika kituo chake cha kazi. Sasa mimi naamini ikiwa katika kila vituo vyetu kutakuwa na ulinzi wa kutosha ubabaishaji sasa itakuwa hakuna kila mwenye haki yake ataweza kupiga kura.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika mchango wangu nakuja katika ukurasa unaofuata wa 166 kifungu cha 14. Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki *marginal note* inasema, "sheha kuwa wakala uandikishaji kwa wadhifa wake". Kifungu cha 14(1) ambacho *marginal note* yake ndio nilioisoma kinasema: "Sheha kutokana na wadhifa wake atakuwa ni Wakala wa Uandikishaji wa Tume katika shehia yake.

Mhe. Mwenyekiti, ndio pale niliposema kwamba Waswahili wanasema "Ukupigao ndio ukufunzao". Uchaguzi uliopita moja ya jambo lililofanya watu wafanye uhuni katika vituo vya kupiga kura, watu kwenda katika vituo ambavyo hawahusiki kwenda kupiga kura; kwa sababu kulikuwa hakuna mtu au kiongozi ambaye yeye ndiye anawatambua wakaazi husika katika eneo lile.

Mhe. Mwenyekiti, kumrejesha sheha kuwa ni wakala wa tume katika kituo cha uchaguzi kitaweza sana kutusaidia kwa wale wababaishaji na mamluki, ambao wanatolewa sehemu mbali mbali kuja kupiga kura katika visiwa vyetu ili kutuchagulia watu halafu wao baadae wakaondoka. Kwa sababu tunavyojua kwamba mtu anamchagua kiongozi ili amshughulikie maendeleo yake na shida zao katika majimbo yao, lakini sasa leo mtu anakaa Mtwara, Singida miaka kumi leo anakuja hapa anakuja kuandikisha na leseni yake ya udereva anapiga kura anaondoka. Mimi nadhani kumrejesha sheha kupitia sheria hii itaweza kusaidia kutunza nidhamu ndani ya vituo vyetu vya uchaguzi na vile vile kuwapunguzia kazi maafisa wa Tume ya Uchaguzi kwa sababu maafisa wa Tume ya Uchaguzi wanaajiriwa kwa muda katika maeneo yale, lakini wao wanakuwa hawajui wale hasa wakaazi katika maeneo yale. Kwa hiyo, hii itaweza kutusaidia sana kutuondolea fujo katika maeneo yetu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika kifungu cha 15 ukurasa wa 167 kinaelezea Wakala wa Uandikishaji. Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri lakini vile vile watendaji wa Tume ya Uchaguzi. Kifungu hiki kinasema kwamba, kila chama cha siasa kinaweza kwa wakati wa uandikishaji kuteuwa mwanachama wake mmoja ambaye ameandikishwa kama ana sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura kwa wakala katika kuandikishwa .

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia katika uchaguzi uliopita uchaguzi wa mwanzo, ambao uligubikwa na ulaghai na vurugu nyingi tuliona vijana ambao walihama Zanzibar zaidi ya miaka 10 wako Uingereza lakini matokeo yake walikuja kupewa vitambulisho wakawa mawakala. Sasa hili mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti kwa sababu kuna masuala ya sheria lakini na uajibikaji wa Tume ya Uchaguzi. Tunaomba mawakala hawa waletwe na vyama, picha zao lakini vile vile tupate *background* kumbukumbu au tusiletewe mamluki. Mtu anaishi Uingereza eti anakuja kukaa uwakala hapa. Hii mimi nafikiri sio haki wala sio demokrasia. Kwa hivyo, tunaomba pamoja na sheria lakini vile vile na utafiti wa kutosha hasa hawa mawakala waliokuja kusimamia haki ndani ya maeneo yetu ya uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kifungu cha 16, hapa kwenye *marginal note* kinaeleza kwamba watu wanaoruhusiwa katika kituo cha uanhikishaji kwa ajili ya kuwasaidia yaani wale

watu ambao wanaruhusiwa katika kituo cha uandikishaji. Hapa kifungu kidogo (f) cha 16 kinasema "mtu anaemsaidia muombaji mwenye mahitaji maalum.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa vurugu na fujo zilizojitokeza hasa katika Kisiwa cha Pemba Mheshimiwa watu wengi walikuwa wananyimwa haki yao kwa kuambiwa kwamba sema sijui kuoma na kuandika. sema sioni wanachukuliwa katika maeneo kenye foleni wanakwenda kupigishwa kura zao kwa nguvu, maana yake ile inakuwa sio hiyari.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana suala hili Tume ya Uchaguzi iweze kulizingatia na kwa kuwa kutakuwa na masheha. Mimi nadhani katika vitu wajaribu sana kuangalia ujanja wa watu hawa ambao wanawatoa watu kwenye foleni kwa kisingiizio, wengine wanasingizia haoni wakati mtu madhali anajulikana kwamba anaona anakwenda sokoni, anateka maji, anafanya shughuli zake, lakini siku ya uchaguzi eti anaambiwa ukienda pale kituoni sema sioni ili apate kupigiwa kura.

Mhe. Mwenyekiti, masuala haya mimi nadhani katika kipindi hiki kinachokuja hasa baada ya kupitisha sheria hii naomba watendaji waweze kuyasimamia kwa ukamilifu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika kifungu cha 25 kinachosema Ukaguzi wa Daftari. Mheshimiwa hapa pana kitu nataka kukisisitiza ambacho kinasema kwamba mtu yeyote aliyejiandikisha kuwa mpiga kura kwa maombi yaliyofanywa kwa afisa uandikishaji anaweza kukagua daftari. Sasa hili mimi ninaomba, hiki kifungu kidogo cha (2) kinasema, "utaratibu wa kukagua daftari utakuwa kama ulivyoelezewa katika kanuni zilizotayarishwa kwa mujibu wa sheria hii". Hapa kuna kitu nilikuwa nataka kusisitiza, tunajua kanuni zipo lakini kwa kuwa tunapitisha sheria hii namuomba sana Mhe. Waziri hiyo kanuni iliyopo lazima itakuwa na marekebisho baada ya kupitishwa sheria hii. Sasa kitu ninachokiomba nakisisitiza Mhe. Mwenyekiti, kwamba kanuni iweze kufanyiwa marekebisho ya haraka ili kuweza kuingiza na yale ambayo tumepitisha katika sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja ukurasa wa 172 kifungu cha 34 ambacho kinasema:

"Kwa mujibu wa masharti ya Katiba, kutakuwa na Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar ambao utafanyika kila baada ya miaka mitano".

Mhe. Mwenyekiti, mimi bado naendelea kusisitiza na nitaendelea kusisitiza, iko haja ya kufanya marekebisho ya katiba kuangaliwa. Kwa sababu Mheshimiwa chaguzi ni moja katika njia ya fitina, chaguzi ni fitina, watu wataelewana, watashirikiana, lakini unapofika mwaka wa uchaguzi zinaanza chuki, fitina, majungu, lakini vile vile kuhujumiana. Sasa nchi yetu ni changa tunahitaji maendeleo. Mimi nadhani bado tuangalie kwenye marekebisho ya katiba, nimeshaleta hoja yangu ya kutaka kufanya marekebisho ya katiba, lakini kuna jambo bado naliona iko haja na huenda nikaliongeza, suala la muda wa uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani muda wa uchaguzi tufanye marekebisho ya katiba iwe miaka saba baada ya miaka mitano na hoja zangu ninazo. Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani

serikali kodi ya wananchi, wananchi wanahangaika, wanavua dagaa, wanafanya kila kitu wanachangia serikali kila baada ya miaka mitano pesa zile zinakwenda kwenye uchaguzi. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia bajeti ya uchaguzi una uwezo wa kujenga skuli za sekondari zaidi ya 20 kwa uchaguzi mmoja, kwa nini kila baada ya miaka mitano tuendelee kupoteza pesa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tukienda kwenye miaka saba, najua kwenye sheria haiwezi kuingia kwa sababu hili ni suala la kikatiba, lakini kama nilivyosema bado iko haja serikali yetu kuangalia na wengine wanasema kwa sababu tuliwahi ku-*raise* hoja hii, wakasema aa, maana yake sisi uchaguzi wetu tunafanya pamoja na Bara. Nawaambia *is not issue,* kwa sababu Wabunge Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kule wana katiba yao na Zanzibar tuna katiba yetu na mfano mzuri tunaweza kufanya chaguzi katika nyakati mbili tofauti wala sio *issue*.

Kwa hiyo, hili bado naendelea kulisisitiza ili wananchi wetu kwa sababu Rais wetu anafanya kazi miaka mitatu tu katika miaka mitano. Mwaka wa mwanzo anaweka sawa mazogozogo ya uchaguzi, miaka mitatu anafanya kazi ya kuendesha serikali mwaka mmoja wa mwisho anaandaa mazingira ya uchaguzi, ukiangalia ukiigawa ile miaka unamkuta Rais anafanya kazi miaka mitatu badala ya mitano. Sasa mimi nadhani miaka miwili, mmoja, arekebishe mazagazaga ya uchaguzi, miaka mitano afanye kazi, mwaka wa mwisho aandae uchaguzi tuangalie maendeleo kama hayatofikiwa kwa haraka sana. Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, iko haja suala hili kikatiba baadae kuliangalia na kulirekebisha.

Mhe. mwenyekiti, nakwenda haraka haraka usinitizame, kifungu cha 37 kinazungumzia mipaka ya majimbo. Hili nafikiri Mhe. Hassan Khamis Hafidh amelieleza, Katiba kifungu 120 sina haja ya kukirejea kinasema kwamba, tume wakati wowote wanaweza wakaangalia kama kuna kasoro yoyote katika mipaka kuangalia kuweza kukata upya majimbo.

Hapa mimi naomba sana kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu vile vile tuangalie sisi katika majimbo pia wakati mwengine kuna ukanganyaji katika utekelezaji wa shughuli zetu. Leo uwakilishi tuna majimbo 54, wabunge tuna majimbo 50 ndani ya nchi moja. Sasa mimi nadhani hili ni jambo la kuweza kulizingatia, naomba Tume ya Uchaguzi na ukiangalia hata safari hii yale majimbo jinsi yalivyokatwa yaani utafikiri labda kuna chochoro utafikiri labda kile kisiwa cha Pemba. Kuna mkono umeingia, kuna mkono umetoka. Mimi nadhani iko haja mipaka ya majimbo kuweza kurekebishwa na kuweza kutangazwa upya ili tuweze kufanya kazi vizuri kwa utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 41 kinasema 'Uchaguzi wa marudio". Mhe. Mwenyekiti, pale ambapo tume itaridhika kabla ya kutangaza matokeo ya uchaguzi, kwamba kulikuwa na kutokufuatwa kwa taratibu za matumizi mabaya ya ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi. Hapa kifungu kidogo cha pili kinasema, pale ambapo kura za mgombea waliopata idadi ya kura sawa zimelingana. Sasa kuna kitu kimoja hapa Mheshimiwa ni muhimu, hakikuingizwa na mimi naomba kifungu cha 41 kiongezwe kifungu kidogo cha (4).

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu suala la kurejea uchaguzi kuna suala muhimu sana ambalo Chama cha Mapinduzi hasa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli anasisitiza suala zima la rushwa, leo hapa iwe uchaguzi urejewe kwa sababu watu wamefungana kura tu, lakini lile suala muhimu kama kuna mtu amegundulikana ameshinda kwa ghilba na dhulma na kutoa rushwa uchaguzi ule ushindwe kurejewa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi naomba kifungu kidogo cha (4) kiongezwe liongezwe na suala la rushwa, ikionekana mtu ametoa rushwa katika uchaguzi basi uchaguzi uweze kurejewa tena watu watangazwe tena, waombe nafasi jimbo uchaguzi urejewe. Hili mimi nashukuru chama ambacho mpaka sasa hivi kinachoonesha dalili ya kupiga vita rushwa ni Chama cha Mapinduzi peke yake, kwa sababu bila ya kusubiri mtu kwenye Uchaguzi Mkuu kama yale mazingira yake anataka kuingia kwenye uchaguzi ametoa rushwa basi pale pale anadhibitiwa. Lakini leo chama chetu kinasisitiza suala la rushwa lakini kwenye sheria ya uchaguzi hatujataja suala la rushwa. Mimi nafikiri tatakuwa bado hatujaweza kuunga mkono jitihada za kuondoa rushwa katika nchi. Kwa hiyo, naomba kifungu kidogo cha (4) moja katika sababu ya kurejewa uchaguzi suala la rushwa na hapa Mhe. Mwenyekiti nitakuja kupiga buti kweli kweli, hapa lazima tuoneshe na sisi ndani ya sheria kwamba tunapiga vita rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, maana yake hata hivi sasa tena hili namuomba sana Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais amwambie Mhe. Makamu wa Pili kwamba hivi sasa tayari kuna watu wanaanza kunyapia nyapia katika majimbo ya watu, mimi kwangu hawaji maana wananiogopa. Leo mtendaji wa serikali amepewa dhamana maana najua uwezo wa kuhonga kwa pesa zake za mfukoni hana, anadokoa serikalini anakwenda kunyapia nyapia kwenye majimbo. Kwanza sasa hivi utaratibu unaambiwa ile ukitamka tu kama wakati bado umekwenda na maji. Sasa mimi nadhani miongoni mwa rushwa ni hii, mtu kutumia ofisi yake vibaya kwa ajili ya kutaka kumuondoa mtu aliyeko madarakani wakati muda haujafika. Mimi nadhani suala la rushwa lazima tulioneshe ndani ya sheria hii ili tuonekane kwamba sasa hivi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejiandaa kupambana na mtu yeyote mwenye nguvu ya kipesa, ukiwa ubabe, lakini kama katoa rushwa akae nje ya uwanja.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda haraka haraka kifungu cha 43 kinasema kwa kuzingatia sifa za mgombea Urais. Hapa maneno yapo. Mhe. Mwenyekiti, bado iko haja ya kufanya marekebisho ya katiba kwamba sifa za kugombea urais, Katiba yetu inasema awe na miaka 40, lakini mimi bado ninaamini tuna vijana wazuri, wamekomaa ambao wana umri wa wa miaka 35 wana uwezo wa kushika nchi na wakaendesha. Tumeshaona katika nchi mbali mbali tumeona Congo, Burundi, vijana wadogo wanaendesha nchi na mambo yanakwenda. Vile vile kama unaweka umri lazima uweke wa chini lakini vile vile uweke wa juu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napendekeza na ninapendekeza katika sheria hii, lakini vile vile na kwenye katiba. Mimi nadhani suala la umri liwe kuanzia miaka 35 ingawa katiba haisemi hivyo lakini na kwenda mbele asizidi miaka 75. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini sheria ya Utumishi wa Umma imeweka umri wa miaka 60 mpaka 65 kustaafu. Sasa leo mtu keshastaafu halafu unataka kuja kumbebesha majukumu mengine. Mimi nadhani akili inahitaji kupumzishwa tuwatengenezee pencheni nzuri ili wapumzike kwa salama.

Lakini Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nataka kuongeza na kifungu kidogo hapo katika eneo hili hichi kimemalizia (d) naomba kiwe (e), yaani wagombea ngazi ya uraisi ni kubwa lazima wapimwe afya. Mhe. Mwenyekiti, watu wapime afya waangaliwe uwezo wao nguvu zao kama alivyosema Mhe. Hassan Khamis Hafidh. Leo unamchagua mtu mgombea uraisi kila miezi 6 China, kila miezi 6 Uingereza yaani hiyo gharama ya kumtibu mtu wakati kuna watu wazima wenye afya zao wana uwezo wa kuongoza nchi.

Kwa hiyo, mimi Mhe. Mwenyekiti, nitakuja kungangana tena katika kifungu hichi nataka tuongezee (e) kwamba....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma muda wako umemalizika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie dakika mbili, tatu.

Mhe. Mwenyekiti: Nimeshakuongeza dakika mbili za kiti nne. Kwa hiyo, naomba umalizie

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, basi mengine nitapeleka kwa maandishi ili nije nipate ufafanuzi kwenye kupiga buti.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka nimalizie hili la mwisho kabisa mengine nitapeleka kwa maandishi suala la Kifungu cha 62 kinachozungumzia suala zima la mkutano wa mwisho wa kampeni lakini vile vile na mikutano ya kampeni.

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na mazoea mabaya na mazoea haya yameonekana kama imeshakuwa ni sheria kwamba watu wanaposimama kwenye majukwaa baada ya kuzungumza sera, baada ya kuzungumza nini watafanya, wao kazi yao ni matusi kuwatukana viongozi tena kwa bahati mbaya viongozi wengine wanakuwa viongozi wa kitaifa. Sasa suala hili limekuwa kama halina mwenyewe.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, na mwenzangu Mhe. Hassan Khamis Hafidh nitaunganisha hapa hapa alizungumzia suala la mtu kujitangazia kushinda nafasi ya uraisi. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kusema kwamba lazima ajitokeze mtu wa kwenda kutoa ushahidi. Mimi nataka tutumie mfano wa Jeshi la Polisi, Jamhuri ya Muungano Tanzania. Leo mtu sio kwamba anazungumzia masuala la uchaguzi ambayo ni hatarishi anakwenda tu anazungumza masuala ya uchochezi hajamaliza kutukana maana yake sio kuzungumza hajamaliza kutukana tayari Jeshi la Polisi linamteremsha kwenye kiriri na anafunguliwa mashtaka.

Kwa hivyo, Jeshi la Polisi lisitafute visingizio kamanda sijui nani hajapeleka ushahidi kwamba mtu anatukana anazungumza maneno hayastahili kwenye kiriri anateremshwa anakwenda kupelekwa pahala panapohusika, pahala ambapo panapostahiki. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache kama nilivyosema *hansard* yangu sijamaliza nitamalizia katika maandishi siungi mkono hoja hii mpaka yale mapendekezo ya kuongeza vile vifungu nilivyovitaka mimi nikubaliwe ndio nitaruhusu mswada huu upite kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Dr Mwinyihaji Makame Mwadini atafuatiwa na Mhe. Dr Makame Ali Ussi na Mhe. Miraji Mussa Khamis ajiandae.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa wasaa kuchangia hoja hii muhimu sana kwa nchi yetu sheria hii au mswada huu wa kufuta sheria ya uchaguzi namba 11 ya mwaka 1984 na kutunga sheria ya uchaguzi ya mwaka 2017.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nianze kwanza kabisa kazi za watu hawa wawili au mmoja niseme ni Mkurugenzi ambaye yeye anaongoza kitengo cha watendaji yaani Sekretarieti ya Tume ili tume yenyewe, Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nikasema hivyo, nimejaribu kusoma sana nione humu hadudi rejea za Mkurugenzi zikoje na za Tume zikoje. Kwa bahati mbaya sikuziona na mizozo ndio inaanza hapo. Mkurugenzi katika tafsiri katajwa humu kama ni mkurugenzi wa uchaguzi alieteuliwa kwa mujibu wa masharti ya sheria ya Afisi ya Tume ya uchaguzi sawa, nini kazi zake.

Haya tuende kwenye tume, tume nayo inetajwa hivyo hivyo maana yake ni Tume ya Uchaguzi iliyaonzishwa chini ya masharti ya Katiba. Lakini Mwenyekiti baadhi ya matatizo mengi sana yanatokana na baadhi ya Wajumbe wa Tume ku-*challenge* mamlaka ya mkurugenzi. Mkurugenzi kwa tume ni kama Katibu Mkuu ana mandate yake ana majukumu yake yamewekwa wazi 1-4. Na tume nao wana mandate yao 1-4, sasa kumuingilia Mkurungenzi, kuingilia Sekretarieti naona ni kosa kubwa sana na hili ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, hizi hadidu rejea ziwekwe hasa zifatute kipengele mahala zitajwe kazi za Mkurugenzi 1,2,3 na yeye ndie kiongozi wa Sekretarieti na yeye ndie mtendaji mkuu kuna mashirikiano kama waziri na Katibu Mkuu.

Lakini kuna mambo kama mambo ya masuuli waziri hawezi kumuamrisha Katibu Mkuu fanya hiki na hichi. Sasa ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, jambo hili liwe *spade out* kwa uwazi kabisa kujaribu kuondoa baadhi ya migongano ambayo haistahiki.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kwenye ukurasa wa 163 kifungu cha 5(3) daftari litahifadhiwa Makao Makuu wa Tume sawa, huko ndiko litahifadhiwa. Lakini daftari hilo hilo tumesema kwamba litaweka katika kila wilaya nakala ya daftari la wapiga kura kwa kila jimbo la wilaya husika na tumeambiwa huko watu watajiandikisha. Lakini la

kuhifadhiwa ni Makao Makuu. Sasa wasiwasi wangu au *point* yangu Mhe. Mwenyekiti, huku Makao Makuu watu wa fedha wenyewe wanaita ndio *strong room* yaani *strong room* Mhe. Mwenyekiti, ndio mapesa yote yanakohifadhiwa huko kuna ufunguo kule kama mkono na huwa anabakia nao mtu mmoja tu wala si wawili. Sasa huku wengine wilayani unaambiwa nao watakuwa wanatia *data*.

Sasa nataka kujua Mhe. Waziri aniwekee wazi ili *accessibility* kuingia kule *strong room* kule anayo nani maana naweka kwenye (*strong room)* unifahamu, *strong room* ndio tunakohifadhi hizo *data* zote za daftari, huko nako kumekuwa na mchezo kunaingiliwa sana na *strong room* ya Tume ni *zero*. *Strong room* ya benki *is very strong* kweli haingii mtu Mhe. Mwenyekiti, kuna udhu wake kule kuna ufunguo mmoja hapewi mtu anaingia nao mwenyewe tu yuko mama mmoja hapo PBZ Mazizini *very strong women* na yeye zile funguo hata akipanda gari hampi mtu nisaidie begi.

Sasa Mheshimiwa nataka kusisitiza tumesikia matatizo mengi sana watu wana-*tamp* na *data* kwenye huko tulikoambiwa kwamba kunakohifadhiwa, ndio pale nilipozungumzia hadudi rejea, wale Wajumbe Waheshimiwa wengine wanajifanya wao wana-*tamp* na *data* kule wanacheza nazo mwisho tunakujaambia kwamba daftari limeingia *virus.* Kweli maana leo unaingia na *diskette* hii, kesho hii, lisiingie *virus* na *virus* wengine tunawajua *virus* gani. Mhe. Mwenyekiti, unafahamu lugha hiyo ninayoizungumza.

Sasa ningeomba sana unajua kuna baadhi ya *data* haidhuru hao wa wilayani wapi waingize. Lakini zile bado ni *raw data* hazijafanyia *analysis* mpaka ziwe *data* kweli zilizofanyiwa *analysis* ndio ziingie kwenye daftari. Mhe. Mwenyekiti, lazima hiyo iwekwe wazi kama si hivyo, haidhuru huko Wilayani tunatia *data* kila mmoja anavyotia nafikiri hatutofika na mizozo haitoondoka.

Naomba niunganishe hapo hapo Mheshimiwa kuna baadhi ya majimbo akilini haiingii kwamba pale wanajiandikisha watu elfu saba elfu tisa, kwa macho tu unalijua baadhi ya jimbo hili na watu wenyewe unawajua watu wa aina gani waliokuwepo pale. Leo unakuja kusikia siku ya kura Jimbo lile watu 9750 wametokea wapi. Sasa ndio hayo ninayozungumza ku-*verify point* yangu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee kwa Bwana Sheha mimi naipongeza sana Tume, naipongeza sana Tume kwa kumrudishia heshima yake Mhe. Sheha, hapa kati tulikuwa tunamuangusha heshima yake yeye ndio *governor* katika Shehia yake, yeye ndie anaejua watu wanaohamia, wanaokaa, wanaoondoka. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kumrudishia heshima yake kwamba yeye ndie atakuwa wakala wa uandikishaji katika eneo lile ni jambo muhimu sana na litatusaidia na wanaompinga Sheha hao ndio wanampinga kwa maslahi yao wenyewe.

Sasa naomba niunganishe nisije nikasahau hiyo *role* ya Sheha. Naomba niruke niende mbali sana lakini kwa hiyo hiyo nisimrudie tena Sheha kwenye kifungu cha 77, kifugu 77 Mheshimiwa ukurasa wa 188 kwa hii *version* niliyonayo wameorodheshwa watu wanaoruhisiwa kuwemo katika kituo cha kupiga kura Sheha hayumo. Kwenye uandikishaji yumo lakini kwenye kupiga kura hayumo. Sasa nataka kupendekeza kwenye

kifungu cha 77(i) imetajwa mtu mwengine yoyote atakaeidhinishwa kwa maandishi na Tume.

Lakini kabla ya hapo tuseme Sheha nae awemo Sheha au mtu mwengine yoyote atakaeidhinishwa kwa maandishi na Tume. Kwenye kujiandikisha yumo hakuna mjadala, lakini kwenye kupiga kura kaachwa nje aa na yeye awepo au mtu yoyote atakaeidhinishwa kwa maandishi na Tume. Ningemomba nyongeza hiyo Mhe. Mwenyekiti, tuiongeze.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende ukurasa wa 182 kifungu cha 63 kinazungumza suala la mikutano ya hadhara. Mhe. Mwenyekiti, utakubaliana na mimi kwamba wakati wa kampeni Tume inakaa na vyama na wanakubaliana mikutano ya hadhara chama gani kiende wapi, kiwanja gani. Lakini kumejitokeza matatizo kwamba baadhi ya viwanja wenyewe wana miko yao, nao wape wale waliopo wenyewe sisi hapa tuliopo ni watu wa aina fulani. Sasa wanakuja watu mfano wanakuja kucheza ngoma au wanakuja kuzungumza maneno aah sie hatuyaafiki. Kwa hiyo, unasema aa kiwanja changu mimi sitaki, mimi ndie mwenye kiwanja changu.

a) Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba tuiweke kwenye sheria kabisa maana tuondoe ule mgogoro kwamba aaah popote kuna right mtu akifanya mkutano, yule kama yeye ndie mwenye kiwanja chake ana miko yake pale ana taratibu zake, ana silka zake basi lazima tumfate mwenye anavyotaka, yeye ndio *owner* pale. Sasa hii naomba sana kwamba kiwanja cha kampeni idhini itoke kwa mwenye kiwanja, mwenye *site*, mwenye *venue,* tusiende tu tukavamia tukafanya mambo kidogo halafu mnaondoka nyinyi mnawatisha watoto wale wanapata shida miezi inakwenda.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana hili jambo kuondoa ule mgogoro *verbal confrontation* wakati mwengine si *verbal* tu lakini mpaka *physical confrontation* inatokezea tuliondoe tuliweke wazi kabisa kwenye sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 197 kifungu 94 kinazungumzia maswala ya wasimamizi au watu wanaoruhusiwa kuwemo katika chumba cha majumuisho, mbali ya majumuisho lakini hata wakati wa kupiga kura. Sasa nakusudia kuna wasimamizi wale wetu wa hapa hapa wenyeji, wao utakuta katika kila chumba kuna *organization* yao wamem-*station* yule msimamizi wao yumo kila chumba. Sasa msimamizi sisi tunajua awe *mobile* sio awe *station* kaganda pale kama ofisa. Sasa yule chanzo cha matatizo maana yake yule anachukuwa *data* pale yeye anatoa amri ana-*dictate* anagombana na wale wasimamizi, maofisa waliopo pale. Hiyo nayo Mheshimiwa ningeomba sana tuliangalie na tulirekebishe kama waziri atalitia humu kwenye sheria au *by-law* iwekwe kwamba wasimamizi mimi sizungumzi hao wa nje, lakini hao hao wa *local*. Utakuta kila chumba kawekwa mtu msimamizi yeye na chama fulani, wenyewe wanasema ni msimamizi wa *organization* lakini unajua hasa Unguja yetu ni ndogo. Unajua hasa huyu fulani huyu yuko hapa kwa maslahi ya chama ya chama fulani.

Kwa hiyo, mimi naishauri sana Mheshimiwa hili nalo tulisimamie kama wasimamizi awe *mobile*, dakika 5 yuko hapa 10 yuko chumba chengine lakini sio agande pale pale kama ofisa yeye wa Tume haipendezi.

Mhe. Mwenyekiti, nimezungumza tayari suala la wajibu wa Wajumbe wa Tume na Mkurugenzi. Naomba nizungumzie suala la jumla sasa dogo tu. Mhe. Mwenyekiti, kwa maoni yangu Tume iwe na meno kumchukulia hatua mtendaji wake yoyote au hata tuweke humu hata Mjumbe sijui kama atakuwa na *mandate* hiyo kwa sababu mwenyewe kateuliwa na Mhe. Rais lakini waweze kumshauri na hiyo iwe ni zoezi linaloendelea sio unamuona huyo mtendaji hafai anatuharibia tunakwenda nae tu mpaka tunafika 2020 huko tunaingia tena kwenye zahma ile bado unae, wapewe meno Mkurugenzi apewe meno haidhuru hana mamlaka ya kufanya haya na haya lakini alau yeye ndie mwenye *mandate* pale anamuoana mtendaji wangu huyu mbovu hana maadili haendi ipasavyo aweze kupendekeza aondoke na tusiwaweke.

Sasa Mhe. Waziri hili lako kama mkurugenzi anakuletea unaambiwa bwana kwenye kuandisha fulani tushamuona hafai wewe unasema aah! nitamzungumza, tutakwenda nae, ngoja kidogo atarekebishika *no that wrong* Mhe. Mwenyekiti, umeshamuona mtendaji usharipotiwa umeshaambiwa, Mkuu wa Wilaya kakwambia, mkuu wa mkoa kakwambia, maafisa wengine wamekwambia huyu hafai anatupotosha kwenye uandikishaji anasema tutamrekebisha lazima tuwe na *prompt action* tukishamuona huyu bwana hatufai aondoke Mheshimiwa hili ni lako Mhe. Waziri tunakuomba sana, samahani naku-*address* wewe kwa sababu mswada ndio wako huu.

Mhe. Mwenyekiti, yale kwa Wajumbe wa Tume nao sijui kikatiba Mhe. Rais sina uhakika kipengele kile kinasemaje kwa sababu yeye ndie anaeteuwa. Lakini pili nae kwa *mandate* yake akimuona Mjumbe wa Tume anahatarisha maisha ya Tume anakwenda kinyume na Tume maadili hana na yeye asimuweke. Nasema hizi ni kazi za Mhe. Rais hatumuingii lakini sie kazi yetu kushauri kwa sababu tukimuweka tunakwenda nae hao ndio wanakuja mwisho tena kutupa matatizo zaidi.

Sasa "udongo upate ulimaji" huku huku anaanza anatenda onyo la kwanza, onyo la pili, la tatu tusingoje bahati mbaya sana tunaambiwa kwamba wako baadhi ya wajumbe wanayo tabia hiyo mpaka mwenyewe mwenyekiti alisema wajumbe walifika kupigana kweli wajumbe wa Tume wafike kupigana haiingii akilini.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa hili tena namrudia Mhe. Waziri Mhe. Mwenyekiti, hiki chombo ni kizito sana, chombo hiki hakiendi peke yake, hiki ni chombo kiende na nguvu za dola. Tunazungumza *state organs*, watu tunazo habari wanafanya hujuma, wanafanya fujo, kidogo kidogo, kidogo kidogo unaripotiwa. Kwa nini hachukui hatua, ndio yale nazungumza. Tunangoja, tunangoja, tunangoja mpaka tena mambo yanafurutu ada, sivyo. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri lazima tuwe wakali kwa hili, tumeshaona hiki chombo sio cha kuchezewa lakini watu wanakichezea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sipendi kutoa mfano wa Rais Uhuru Kenyatta juzi hapa hotuba yake baada ya uchaguzi wa mwanzo kuharibika. Anasema watu milioni 40

wameshamchagua wanayemtaka, lakini watu wachache tu wanatuchezea wanaharibu kila kitu. Akatumia neno moja silisahau *"I am going to fix them"*. Haikupaswa Rais mzima aje aviambie vyombo vyake namna ile au akamwambie ofisa wake namna ile kwamba *I am going to fix him.* Aaa haikupendeza, lakini sasa inamaanisha nini, ile *seriousness* chombo hiki ioneshe kwa nchi. Tusiwe na watu wanatuchezea chezea, au wanaichezea chezea. Watu wanatamka matamshi ya ovyo hata onyo hawapewi, wengine wanafanya kabisa sheria zinakataza dola tunawaachia. Kwanini? Mhe. Mwenyekiti, lazima tunapozungumza sheria tuzifanyie kazi, leo tunapitisha sheria tuifanyie kazi, tusimheshimu mtu kwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, wengine tulipata kuona uchaguzi wa 1963 ndio mimi napata akili pale nipo darasa la tano. Nipo Matarumbeta pale nikaona uchaguzi wa mwaka 1963 jinsi ulivyokuwa watu walivyopigwa marungu damu zikamwagika mpaka timu ya *African Riffles* wakatoka Nairobi wakaletwa, tunaamka alfajiri majumbani mle Matarumbeta mtaani pale unakuta senyenge tu. Lazima dola i-*act* hivyo, yaani *act promptly* usingoje, tatizo limeshatokezea hapo hapo haidhuru tushauriane, tuelekezane, lakini lazima tuwe na maamuzi. Mhe. Mwenyekiti, tusiwe na kigugumizi kwenye maamuzi. Watu wanashauri, wanaelekeza, yapime Waziri haya ninayoshauriwa ndio yanafaa, lakini tusingoje, tusiwe na ajizi.

Mhe. Mwenyekiti, wasia wangu kwamba chombo hiki tukipe meno, tukipe *mandate* na tukilinde na wa kuilinda ni dola, yeye mwenyewe hawezi huyu. Lakini dola lazima ikilinde hiki chombo kifanye kazi na tusiwe na msalie Mtume na maofisa wanaotuchezea, ikiwa maofisa wetu, ikiwa maofisa wa Tume, ikiwa na vyombo vya usalama, kuna habari kwamba kuna baadhi ya maofisa wa vyombo vya usalama walikuwa nao wanatuchezea tusingoje. Mhe. Mwenyekiti, kazungumza vizuri humu Mhe. Hassan Khamis Hafidh (*Diaspora*) kwamba nchi nyengine watu kama hawa hukumu yao risasi tu, hilo ni kosa la jinai, ni risasi tu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja pamoja na marekebisho haya waliyozungumza wenzangu tuyatilie maanani chombo chetu hiki kifanye kazi kwa maadili tusiogope mtu wala kivuli chake, twende kwa mujibu wa taratibu zinavyofanya. Kama taratibu hazifuati tusione tabu bwana hata kumpiga *lock up* akakaa ndani huko. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, atafuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa, na Mhe. Salma Mussa Bilal ajiandae.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi niingie katika *list* ya wachangiaji wa mswada huu muhimu sana wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya 1984 na kutunga Sheria Mpya ya Uchaguzi ya mwaka 2017.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Serikali inastahiki sana pongezi, na Tume nayo inastahiki sana pongezi kwa kuleta mswada wa aina hii. Ni vizuri kuwe na miswada, mara hii katika

Baraza letu hili mara nyingi tumekuwa na miswada mingi sana tumefanya marekebisho na hii ndio inavyotakiwa. Tunaambiwa siku zote tusiende kwa mazoea tubadilike, haya ndio mambo yatakayotufanya tubadilike. Kwa hivyo, narudia kumpongeza sana Mhe. Rais, Tume ya Uchaguzi, Mwanasheria Mkuu kwa kuleta mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza kwa historia fupi tu, nitakwenda kwa ufupi ufupi pengine hata muda huo nisipitilize kwa sababu wenzangu wengi wameshachangia mambo mengi kwa hiyo naona nisirudie yale yale.

Mhe. Mwenyekiti, tukianza na historia mara baada ya Mapinduzi kipindi chote kabla ya vyama vingi kuanza mwaka 1992 nadhani tulikuwa tunaongozana au tunakwenda kwa mujibu wa *ethics* za kupendana katika nchi yetu. Kulikuwa hakuna malumbano sana, malumbano yaliyokuwepo ni ndani ya wenyewe kwa wenyewe ambayo yalikuwa yanasawazishwa mara moja. Uchaguzi wa viongozi ulikuwa unafanyika kwa kufuata taratibu, ama tukio fulani limetokea anabadilika kiongozi anakuwa fulani. Tumeshuhudia viongozi wasiopungua wanne kwa mfano alikuwepo Mhe. Abeid Amani Karume aliyeanza, kaja Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, kaingia Mhe. Ali Hassan Mwinyi, hatimaye Mhe. Idris Abdul-Wakil, baadaye Dkt. Salmin Amour Juma, tumekwenda Dkt. Amani Abeid Karume, tumekwenda hapa na Dkt. Ali Mohamed Shein sasa hivi. Kwa kweli ni mabadiliko ambayo tunakwenda nayo kwa mujibu wa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, mara baada ya kuanza vyama vingi mizozo mingi sana imeanza kutokezea. Tunajua madhumuni ya chama chochote cha siasa kashiriki katika uchaguzi na kadhalika, madhumuni yake makubwa ni kupata ushindi aongoze dola. Hii wataalam wa *political science* wanasema ni ku-*struggle for power.*

.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza rafiki yangu hapa Mhe. Said Soud Said ni mtu mwenye msimamo. Yeye ni kiongozi wa chama, ana chama chake na ni Mwenyekiti wa Chama Taifa anagombea Urais lakini anajua kuna Mungu, kushinda na kushindwa ni matokeo, ni majaaliwa ya Mungu. Kwa hiyo, yupo anaendelea na kujenga taifa letu hili kwa mashirikiano makubwa sana. Naomba na wale wengine nao wafuate mfano kama huu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema katika nchi yoyote ya demokrasia, ikiwemo hii Zanzibar ambayo demokrasia yake inaongozwa na Mapinduzi kama walivyosema wenzangu hapa. Tunaposhindana tunajua kwamba kuna mshindi na mshindwa na lazima tukubali hayo, lazima tuyakubali, tukianza kufanya chuki basi tutakuwa tunakwenda kinyume na hata taratibu za Tume, taratibu za nchi na kadhalika. Katika chaguzi zetu hizi kumejitokeza mambo mengi sana, kumekuwa na chuki. Waingereza au wataalam wanasema zile *deeply embedded habitual tendency,* ule undani wa watu umejitokeza mwingi sana, umetokea ubaguzi watu wanabaguana hata kwenye biashara huyu nani asiuziwe, huyu afanye nini, huu asifanye nini, hata kuzikana watu wamekuwa wakigomea. Sababu tu ya wachache ambao wanalazimisha lazima washinde, hata kama itakwenda kinyume na taratibu na sheria zilizowekwa lazima washinde wao na kujitangaza kwamba wao wameshinda matokeo yake ndio yanakuja haya.

Katika chuki hizo zinakuja mtu anataka alipize kisasi kwa kosa hajafanyiwa, wazungu wanaita *procrastination* nafikiri Mwanasheria Mkuu analifahamu hilo pengine ataninong'oneza kwamba pale ulikosea. Lakini kulipiza kisasi kwa kosa hujafanyiwa wazungu wanaita *procrastination* na katika sheria ipo. Kuzibena sheria kuzibatilisha vile ilivyo ukweli umeshawekwa, kama ni Rais ameshatangazwa, kila kitu kimeshatangazwa, viongozi wote wameshateuliwa, halafu wewe ukenda kinyume ukatangaza vyengine. Maana yake kama huko Mahkamani kuna kifungu cha hukumu kinaitwa *conspiracy to the cause of justice,* yaani unabatilisha, unaubena ukweli unataka kufanya ukweli wako uonekane uongo wakati ambapo haiwezekani kabisa kufanyika jambo kama hilo. Unasababisha chuki, dharau, ubinafsi ndani yake na kadhalika. Masuala haya kwa kweli ndio maana tumeleta mswada huu ili kuweka mikakati ambayo itasaidia hizi chuki, hii kudanganya danganya iondoke. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeupitia mswada huu wote nimeuangalia nimeona katika sura ya kwanza hapa kipengele cha 3 kuna tafsiri, naona kuna maneno karibu 46 hapa yametafsiriwa na tafsiri zimekuja vizuri tu. Lakini katika mambo yote haya lazima kunakuwa na upungufu fulani, na hilo linaweza likarekebishwa sasa hivi au baadae. Nathubutu kusema kwamba humu mote sura ya kwanza nimepitia hizi *definition* nimeona kwamba kuna neno uchaguzi limetafsiriwa hapa kwa maana ya uchaguzi unaofanyika kuchagua viongozi. Lakini nimeona lingetafsiriwa kwanza lile neno, *translation* ya lile neno uchaguzi lenyewe likabainishwa pale halafu tena ukaja uchaguzi wa viongozi wa Rais, uchaguzi wa Madiwani, lingekwenda vizuri zaidi na ikafahamika vizuri zaidi kwenye sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nikaingia kwenye sura ya pili nikaona kwamba kuna daftari hili la kupiga kura, hapa limeelezwa daftari halafu imeelezwa kwamba litakuwa na jina kamili, litakuwa na picha. Sasa kama ni daftari litakuwa na majina si jina moja tu. Sasa nilikuwa napendekeza basi isemwe kwamba daftari hili litakuwa na majina ya wapiga kura, picha zao pamoja na tarehe zao za kuzaliwa na kadhalika. Hilo ni daftari la watu wengi kama linavyo-*qualify* hapa kwamba ni daftari la jina la mtu mmoja. Ingawa inafahamika lakini ni vizuri ikasomeka hivyo. Kuna mengine mengi ambayo yamesemwa na wenzangu nayakubali kabisa na nayaunga mkono. Niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kabla sijafunga mjadala wangu.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuondosha haya matatizo nimesema tuwe tunafanya *amendment* ya hii Sheria ya Uchaguzi. Pia kuna kufanyiwa *amendment,* kwa hiyo *Election Commission Act* kwa sababu hii tunasema kwamba ni *Independent Electoral Commission* ambayo kwa kweli inajitegemea. Hakuna tena mtu aliye juu ya *commission* hii kama walivyosema wenzangu ambaye anaweza akenda akajitangaza kwamba yeye ni mshindi wakati *commission* hiyo ipo. Kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba hata hiyo *act* yenyewe basi irekebishwe, lakini irekebishwe kwa kufanya utafiti wa kutosha kuona mapungufu yaliyojitokeza katika *establishment* ya hii *commission* yenyewe, tuone mambo ya *membership* ya *commission,* tuone hata hizi *office accomodation* za *commission* zikiwemo ofisi za huko Wilayani, Mikoani na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, pia tuangalie ukweli kwamba *commission* haiwezi kuingiliwa na mtu yeyote na hiyo pia iingizwe na ielezwe wazi wazi katika *act* hiyo. Halafu *member of commission* wale, hiyo *study* yenyewe iangalie halafu ipendekeze *member of commission* ambao wapo katika ofisi na pengine wanapaswa wawe *disqualified* kwa mambo gani ambayo yatawapasa wawe *disqualified* wasiwe *member of commission*. Inawezekana pengine kutokana na *discipline* yao, inawezekana kutokana na ugonjwa na kadhalika. Nakumbuka kama sikosei katika *commission* hii hii imeshatokea watu kupigana ngumi ndani ya ofisi kwa sababu ya kupingana huyu ana msimamo huu, na huyu ana msimamo huu wakaanza kuzozana. Kwa hiyo, hiyo nayo ikiingia katika *research* halafu ikawa *documented* kwenye *Act* basi itasaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, halafu tuiangalie na ile *commission,* wale *staff* wa *commission* kama wapo *appropriate* na maendeleo ya sera za uchaguzi. Halafu kama kuna *saving* na *transfer* zozote, *liability* zozote za Tume basi nazo pia ziainishwe katika *Act* hiyo. Halafu tena tutakuwa na mengineyo *(miscellaneous)* ambayo yatahusu *interpretation* kama hivi tulivyosema mwanzo. Hapa nimesema hivyo kwa sababu naona hii *independent electoral commission* inaitwa kwa ufupi tu *electoral commission,* unahisi neno muhimu sana *independent*. Sasa kuna mwengine akisikia *electoral commission* anajua hii *independent*. Kwa hiyo, likiingizwa hilo neno *independent electoral commission* nafikiri mtu ataweka heshima yake sawa sawa atajua lipi la kulizungumza lipo sawa na miongozo ya *commission*, na lipi la kuacha kuzungumza halipo sawa na miongozo ya *commission*.

Mhe. Mwenyekiti, maana ya kusema hayo, ni kwamba vitendo kama vile vilivyojitokeza vya uvunjaji wa haki za binaadam wakati wa uchaguzi kwa baadhi ya wagombea kununua vitambulisho vya watu kuwakosesha haki yao ya kwenda kupiga kura, hii ni uvunjifu wa haki za kibinaadam, wanaweza kushtakiwa hata kimataifa. Kwa hivyo, katika marekebisho haya nadhani na hiyo iingie *specific* kwamba mtu yeyote atakayenunua kitambulisho cha mwenzake kwa madhumuni ya kukitumia au asiende kupiga kura tu na ikithibitika, basi huyo achukuliwe hatua zinazostahiki tena apewe adhabu kali sana kwa sababu huyo ni muhalifu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudia tena nilisema mimi sitotumia muda mrefu kwa sababu wenzangu wamezungumza vizuri sana hapa kimapinduzi na ki-*socialist* sijui, kwa hiyo mimi sitaki niharibu uzuri wa mambo yote haya. Najua hii itakwenda itatumika na baadae itakuja kurudi tena japo si miaka hii lakini miaka ya mbele itarekebishwa tena, huo ndio msimamo kwamba hakuna kitu kinachokuwa *perfect hundred percent* kikawa kipo sawa maisha yake kikatumika hivyo. Kitakwenda na wakati kitabadilika, kitabadilika mpaka dunia itakwisha.

Mhe. Mwenyekiti, narudia kuwapongeza sana watu wa Tume ya Uchaguzi akiwemo Mwenyekiti, Mkurugenzi na watendaji wote kwa kuendesha uchaguzi wa marudio kwa ufanisi zaidi. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuwa miongoni mwa wachangiaji wa mswada huu uliokuwepo mbele yetu. Lakini kwanza niwapongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Wakurugenzi na watendaji wake wote wa Tume ya Uchaguzi kwa kazi kubwa ambayo wameileta mbele yetu. Wamefanya kazi nzuri na imeturahisishia mambo mengi sana. Lakini kabla ya kuelekea huko Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia vile vipengele ambavyo wenzangu wamenibakishia maana vingi wamevisemea vizuri na sitarejea huko.

Niwaambie tu wenzetu Mhe. Waziri katika jambo moja kubwa sana ambalo tunawaweka rehani wenzetu hawa wa Tume ya Uchaguzi ni kuwawekea Tume ambayo inatupa mashaka sana katika nchi yetu. Tume moja ambayo inaingiliwa na vyama vya siasa sio Tume rafiki. Haya mazuri tunayoyapitisha leo na tutakayoyapitisha siku za mbele, kwa tume tuliyonayo ile ambayo inatoa fursa kwa vyama vya siasa hasa vikubwa vile viwili haitatufikisha. Lazima tutafute Tume huru itakayokuwa inatoa ufanisi mzuri, lakini inakwenda kufanya kazi zake bila ya ushabiki kwa vyama vyao vya siasa. Lakini hapa haya tunayoyatunga leo na tunayoyapitisha leo watayatekeleza vizuri. Lakini kinyume chake tukirudi na Tume ile ambayo haina uhuru wa kutekeleza kazi zake,ushabiki utaendelea kutokea lakini na wenzetu tutakuwa tunawaweka rehani, wakati fulani tunaweza tukafika pahala tukawalaumu kwa mambo ambayo sio ya msingi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba kuchangia kwenye tafsiri. Tafsiri zimetolewa katika maeneo mengi, lakini kuna neno huku mbele katika kifungu cha 12(3)(a) imejitokeza Idara Maalum haikutolewa tafsiri. Katika moja ya taasisi zetu zinazoleta mitihani hasa ukifika wakati wa uchaguzi na suala la Idara Maalum limo. Sasa tafsiri katika sheria hii ningeomba sana ikatolewa maana yake, au ikaandikwa tu kwa mujibu wa utaratibu ambao uko humu Idara Maalum kama inavyosomeka katika Katiba ya Zanzibar, basi pia inaweza aidha, tafsiri au isomeke, hayo ni mapendekezo yangu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika kifungu hicho hicho cha 12(2)(a), kuna neno hapo ameolewa na anaishi katika jimbo hilo mradi mwenza wake wa ndoa ni mkaazi wa kudumu wa eneo hilo. Tumempa *favour* mwanamke maana ndiye anayeolewa kwa mujibu wa kumbukumbu zangu, hao wengine siwatambui. Lakini wanaume pia na wao huowa wakakaa kwa wake zao, kwa hivyo katika fursa ya kijamii zaidi tumemuona mmoja. Sasa ilikuwa mapendekezo yangu tuweke tu ameolewa au ameowa, sasa hayo maelezo ya mbele yabaki kama yalivyo, sasa fursa zitakuwa kwa pande zote mbili, maana sio mara nyingi. Sasa hivi wanawake huwa wanaolewa lakini wako wanaoolewa pia na wanaume wakawafuata wanawake na wakaishi pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika hiyo hiyo 12(3) niliyochangia ile tafsiri, lakini 12(3)(a) nikasema maelezo yote lakini ndani yake tumeisahau taasisi moja ya uhamiaji ni taasisi ambayo tunashirikiana nayo. Kuna taasisi zimetajwa kama Afisa Usalama wa Taifa, Jeshi la Polisi, Idara Maalum na Jeshi la Wananchi. Lakini uhamiaji tumeiwacha na wao hawa ni sehemu pia katika utekelezaji wa majukumu yetu, kwa sababu wanaingia hata katika hizo Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya zetu kwa mule mwahala mwingine. Sasa wana waajiriwa ambao tunakaa nao pia kwa muda mrefu, kwa hivyo tukiwataja hawa na wale wengine tukawaacha katika kuwasema katika sheria yetu

wakapata haki ya msingi kama walivyopata wenzao itakuwa sio jambo la busara, ndio nikasema tuongeze tu na Uhamiaji. Kama Mhe. Waziri atakubaliana na wazo langu basi tuongeze, hatukukubaliana basi tutaona mbele ya safari.

Naomba niende sasa Mhe. Mwenyekiti, katika kipengele cha 15(1), ambacho kinazungumzia Wakala wa Uandikishaji. Mimi naomba niungane na wenzangu, wako wenzangu wawili nilikuwa nawasikiliza kwa makini. Walisema tuwaondowe kabisa hawa na tunawaondoa kwa dhamira pia na malengo mahususi na ikifika pahala kwa ujumla wetu tukarudi kwenye Katiba ya Zanzibar, tukaanza kifungu cha 6(2) tukakinukuu. Mimi naomba nikinukuu.

Kifungu cha 6(2)

> "Kila Mzanzibari kwa misingi ya katiba hii ataweza kufaidi haki na fursa zote anazostahiki Mzanzibari na atapaswa kutekeleza wajibu wa majukumu na dhamana za Mzanzibari kama ilivyo kwenye katiba hii au kwenye sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi".

Lakini kipengele cha 7(1) pia naomba nikinukuu kwa kujenga hoja ya huku ninakoelekea. Kwa hivyo, kila Mzanzibari anayetimiza umri wa miaka 18 anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Zanzibar.

Sasa hoja yangu iko wapi Mhe. Mwenyekiti, fursa hii kapewa Mzanzibari hakupewa mwanachama wa chama cha siasa. Sasa leo huku tunawajadili wanachama kuwa ndio wanaokwenda kujiandikisha hatuwajadili Wazanzibari. Sasa tukiwajadili Wazanzibari kuwawekea wakala sio vyema, na sio utaratibu ambao Wazanzibari tunakwenda kuwawekea wakala wanaotokana na vyama vya siasa.

Kwa hivyo, haki hii ya kikatiba ameipata na tumeitunga wenyewe katiba ya Zanzibar. Lakini leo tunatunga sheria haki yake ile ya kuwa Mzanzibari na kwenda kupiga kura anapotimiza umri wa miaka 18, tunamuingiza sasa kwenye uwanachama wa chama cha siasa na ndio maana mnamuwekea wakala. Sasa kwa nini kama wewe umeshakuwa na haki ya kupiga kura, yaani haki ya kujiandikisha ili uwe mpiga kura, lakini wako wenye haki hawana hata hicho chama cha siasa. Leo hapa mnawapeleka wakala, wakala watimie wa vyama 14, sasa yeye kama hana hata kimoja na umemuwekea wakala atasaidiwa na nani kuipata haki yake.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kimsingi hiki hakileti tija na hakina maana hapa kamili ya kuwa ule uandikishaji pia tunaupeleka wakala kwenye haki ya msingi ya Mzanzibari, tumezungumza katika katiba yeye apate kupiga kura akishatimiza umri wa miaka 18. Lakini hakuambiwa ana haki ya kuwa mwanachama wa chama cha siasa, sasa leo mnawapeleka watu wa vyama vya siasa wakawe wakala wa kwenda kumnyima yeye wakati mwengine haki. Maana kama hawakumtambua wao, utaratibu wa vyama hivi 14, maana kuna watu wa kundi la 15 hawana chama hata kimoja na ndio hoja yangu. Tukiwacha vile vyama 14 tulivyonavyo na kuvisajili kama wewe huna chama maana wewe wakala wako huna. Sasa hapa ndio tunapeleka kwenye ushabiki, suala la

uandikishaji tulitowe kwenye ushabiki wa vyama vya siasa, tuiwachie serikali na tume tuliyoiweka. Kwa hivyo, eneo hili tuondowe wakala wakati wa uandikishaji. Mimi sina tatizo wa kuweka wakala wakati huo wa kupiga kura, huyu wakati haki yake keshaipata huko nje ya kupata kadi ya mpiga kura atakwenda tu kupiga kura, lakini pale mwanzo wa kuingia kwa nini tufike pahala hapa.

Hapa Mhe. Waziri kwa mantiki hiyo mimi buti langu la mwanzo naweka hapa, mimi hapa naweka shilingi kabisa maana yake sina maelezo yatakayokuwa rafiki nitakayopingana na kutafuta haki ya msingi ya kuandikishwa kwa mpiga kura unapotimia umri wa miaka 18 kesha ukawekewe wakala wa chama cha siasa wakati katiba haikueleza hivyo. Kwa hivyo, mimi nasema kifungu hiki kiondoshwe na kikiondoshwa kwa maana ya kifungu cha 16(d) kiondoshwe.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba kukazia hapa, leo hii Tume ya Uchaguzi ina ofisi zake mpaka mawilayani na inafanyakazi kila siku maana ndio dhamira ya kufungua ofisi. Leo hii kazi hii tukaiweka siku maalum na utaratibu wa kwenda wewe ukaandikishe maana yake inakuwa siku maalum kesha utoke na mawakala kuwepo na kuwafunza na vitu vingine. Hii kazi tunaiweka ni kazi ya operesheni. Sasa tume itakuwa kazi yake kila siku kwenye eneo hili wakafanye kazi ya operesheni haiwezekani, iwe ndio kazi yao ya kawaida kama ambavyo wanafanyakazi ya Uzanzibari Mkaazi, umetimiza sifa unakwenda unaandikwa unaondoka. Lakini leo tunaweka urafiki wa vyama vya siasa hata ile dhamira na ukuaji wa Tume kwenda katika malengo mazuru unaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye kifungu 17(5) hapa nimezungumza vya kutosha. Mimi nina marekebisho kidogo, sentensi ya 17(5) inasema uamuzi wa Tume juu ya masuala ya uandikishaji uliofanywa chini ya kifungu hiki, utakuwa wa mwisho na neno limekosewa hapa, hili neno "hautojadiliwa" lirekebishwe. Lakini pia naongeza maneno kuwa "hautajadiliwa na mtu au taasisi yoyote", lazima tuifunge katika misingi hiyo, tusiiweke kama hivyo ilivyo itatosheleza. Nakuomba sana Mhe. Waziri kwenye jambo hilo, baada ya hayo marekebisho pia unikubalie na hilo ninaloongeza utafanya busara sana, na kwa sababu wewe ni mzee wa busara katika Baraza hili naamini busara zako zitatuelekeza kwenye kukubaliana na hili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kifungu cha 35(3) na hapa pia nina marekebisho kidogo tu. Naomba niyakariri ili marekebisho yake tuyapate vizuri.

> "Tume kwa kupitia kanuni zilizotayarishwa chini ya sheria hii inaweza kutoa maelekezo na kuweka mazingira ambayo mtu kwa uchaguzi".

Sasa tafsiri ya sheria hii hakuna neno "mtu". Tafsiri ya sheria hii kuna neno "mpiga kura", kwa hivyo mtu aondoke isomeke mpiga kura, kwa sababu ndio tuliyomzunguza na tumetoa tafsiri katika sheria hii. Lakini mbele baada ya koma hiyo, kuruhusiwa kupiga kura huku, imeandikwa "mbali na kituo ambacho amepigiwa kura". Sawa hii naomba kukubaliana nayo haina tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika kifungu cha 36(3) na 36(5). Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki pia kina marekebisho kidogo 36(3) kinasema;

Kifungu cha 36(3)

"Msimamizi wa uchaguzi anaweza kulingana neno "kulingana" "litoke halileti maana. Hata ukienda kwenye *version* ya Kiingereza pia linatofautiana. Kwa hivyo, tukirudi katika uhalisia basi naomba na kufuatana na ile *version* ya Kiingereza, Msimamizi wa Uchaguzi anaweza kwa maelekezo ya Mkurugenzi kuteua lakini pia iongezwe, kuteua na kuajiri watendaji wa vituo vya kupigia kura kutokana, "baada ya kulingana" pia nalo litoke. Nimetoa kulingana ya mwanzo halafu nimetoa kulingana ya pili.

Sasa kulingana ya pili badala ya kulingana basi iwe kutokana na mahitaji ya kuweza kusimamia uchaguzi katika jambo hilo. Naomba nirejee Mhe. Waziri. Msimamizi wa Uchaguzi anaweza, hapa imeandikwa kulingana siafikiani nayo haileti mantiki na haileti sura na inapingana na *version* ya Kiingereza. Ukiisoma ya Kiingereza basi tafsiri yake Msimamizi wa Uchaguzi anaweza kwa maelekezo ya Mkurugenzi iendelee hivyo. Lakini naongeza kuteuwa lipo, lakini kuteuwa na kuajiri watendaji wa vituo vya kupigia kura, kulingana itoke iwe kutokana na mahitaji ya kuweza kusimamia uchaguzi katika jambo hilo.

Mhe. Waziri tumeleta ushauri huo kwa mantiki ya kutengeneza sheria nzuri. Tafsiri ya Kiingereza au ile *version* ya Kiingereza ukiisoma inapingana na hii, ili iwekwe sawa na yale maneno niliyoongeza hayo marekebisho yake basi nilikuwa naomba yakae kama nilivyosema.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye kifungu cha 36(5) kuna sura ya kiapo hapa, kiapo cha kutunza siri. Mimi naongeza tu kiapo cha kutunza siri na uadilifu, katika kazi hii tunayowapa wenzetu lazima hivi viapo viende na hatua mbili, kiapo cha kutunza siri na uadilifu kiingie hapo nimeongeza marekebisho madogo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika kifungu cha 44. Kile kifungu cha 43 wenzangu wamekichangia vizuri, lakini mimi niungane na sheria hii pale kwenye miaka ya 40 sitaki kurudi nyuma, tunaendelea 40 kwa sababu hata Mtume Mohammad (*SWA*) alianzia hapa uongozi wake, kwa hivyo na mimi sina tatizo, kurudi nyuma sirudi lakini wacha twende mbele kutoka 40, kwa sababu hata na mimi mwenyewe ndio nimeshafikia naweza kugombea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba niende kwenye kifungu cha 44, ambacho mimi nina tatizo kidogo Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, nina tatizo kidogo kwenye kifungu cha 44(a) kwenye sifa hizo za hawa waliogombea uwakilishi wawe Wazanzibari. Kule kwa mgombea wa Urais awe Mzanzibari wa kuzaliwa, kwa hivyo na mimi nina hoja katika eneo hili kwa sababu hawa ndio wasaidizi wa Rais na wasaidizi wa Rais lazima tuwapeleke kwenye kuwa na sifa ya Mzanzibari, lakini wawe na sifa ya kuzaliwa kwao ndio wanapokuwa wazalendo wa nchi hii. Lakini pia na nyinyi viongozi mlio kuwepo mbele huko mtapunguza kwenda kuwazaa watoto wenu Uingereza, kisha baadae

wakapata makole ya kule wakaja kutuongoza sisi. Sasa hili pia tutajenga utaratibu wa kuonekana basi kwenye nafasi zile za msingi za kumtafuta Rais lakini na zile za kufika pahala tukatafuta wasaidizi watakaomsaidia Rais, basi wawe na *criteria* sawa.

Mhe. Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu nataka ule uzalendo wa nchi yetu, angalau huu udiwani tunaweza tukawaachia, japokuwa atakuwa anakuja kuandaa Meya, pengine Meya atakua sio mzalendo, lakini kwenye sura ya uwakilishi, tunaandaa mawaziri, viongozi wakubwa pengine na humu ndani ya kundi hili la kuwa mwakilishi kuna Makamu wa Pili wa Rais. Sasa tutakapofika pahala huku kwenye Urais kuna Mzanzibari wa kuzaliwa, lakini huku kwenye wasaidizi wa Rais kuna Mzanzibari tu, kwa maana hiyo hata yule wa kuandikishwa anaingia hapa, hatuwezi kutoa fursa zote kwenye maeneo muhimu na moja ya eneo muhimu ni hili, lakini pia litawashajihisha na nyie nasema viongozi mliokuwepo mbele watoto wenu msiwazae Uingereza sana, muwazae hapa na wajenge uzalendo wa hapa, wasome hapa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika kifungu cha 48(1)(a) na hapa nataka niweke nyongeza kidogo Mhe. Waziri;

Kifungu cha 48(1)(a)

> "Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar iwapo atadhaminiwa na wapiga kura wasiopungua 200 ambao ni wanachama wa chama chake kutoka kila mkoa kati ya mikoa mitano ya Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, sentensi nakubaliana nayo lakini naomba niongeze tu, mwisho baada ya mikoa mitano ya Zanzibar "ambao ni wapiga kura". Hatuwezi kwenda kum-*support* Rais kuwa mwanachama tu wa chama chake, lakini usiwe tu mpiga kura maana yake wa kumsaidia huyo Rais mwenyewe. Maana unaweza kuwa na wanachama 200 ambao hata ndani ya daftari hawamo tumewaweka katika sheria wakam-*support* siku moja Rais anapata kura moja, haiwezekani. Kwa hivyo, angalau wale wanaomdhamini basi pia wawe ni wapiga kura katika daftari la kudumu. Kwa hivyo, naongeza tu maelezo yawe vile vile wanachama wa chama chako cha siasa, lakini pia mwisho tunaongeza ambao ni wapiga kura.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende sasa katika kifungu cha 53(1) ambacho kimezungumza kuwa kutakuwa na viti maalum vya wanawake katika Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 67. Kwanza hicho kifungu cha 67 kiwe ni 67(1) la mwanzo kwa sababu ndio hakuna 67 tupu. Kwa hivyo, katika Katiba kuna kifungu cha 67(1) lakini na maelezo ukenda katika kifungu cha 67(1) kwa tafsiri maana yake ukiyavuta yanashabihiana, lakini ni vyema yale maelezo yaliyokuwemo kwenye Katiba basi na hapa iwe, naomba kupendekeza kama ifuatavyo:

"Kuwa kutakuwa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanawake kwa idadi ya asilimia 40 ya idadi ya wapiga kura wote wale waliochaguliwa, kama kilivyozungumza kifungu cha 67(1). Lakini hoja yangu ya mwanzo kifungu cha 67 basi iwe kifungu cha 67(1), na ya pili ndio hayo marekebisho ambayo nimeyasema kama tutakubaliana".

Hapa sina buti ni maelezo tu ya kuwa tunapofika pahala tukaelekezana, kama na mwenzako atakuelekeza vizuri unakubaliana naye, lakini hoja yangu ya msingi hapa ni hiyo.

Naomba nimalizie Mhe. Mwenyekiti, kwa kifungu 127(a),(b) na (c). Katika kifungu hiki kimeeleza adhabu na adhabu hizi hapa ndio pana mustakabali wa nchi. Maana nchi inapoingia katika uchaguzi basi inakuwa katika hali ngumu kweli. Sasa kuna watu hapa wakijitangazia huku maana yake unakuja kukuta faini katika kipengele cha (a) ni shilingi milioni 50. Hawa wenzetu wa milioni 50 maana yake ni kidogo, kwanza ile adhabu ya miaka 5 mimi sikubaliani nayo, kwanza mimi nitapiga buti hapa ni lazima tuweke miaka 10 angalau vipindi viwili vya uchaguzi.

Kwa hivyo, mapendekezo yangu mimi hapa nitapiga buti, *logic* ya miaka mitano sikubaliani nayo, lazima tuweke vipindi viwili vya uchaguzi, maana yake miaka 10 lakini na adhabu yake alau, kwa sababu kwenye jambo hili ile *tension* ya nchi maana yake unakuja kuiharibu kwa wakati mmoja, unamuwekea milioni 50 mtu wa aina hiyo. Kwa hivyo, kifungu (a) miaka 10 lakini na milioni 200, tuondoke kwenye milioni 50 twende kwenye milioni 200 maana tusiwe na majaribu katika nchi yetu, tukitunga sheria maana yake tutunge sheria itakayo heshimika.

Lakini kifungu cha (b) huyu mwanachama wa chama cha siasa ambaye atakwenda huko kufanya tatizo kama lililozungumzwa katika kifungu cha 127(1), hapa pia adhabu yake iliwekwa hapa milioni 100. Milioni 100 huyu kidogo kachukua dhima ya chama chake, yeye na chama chake maana yake napendekeza milioni 500 alau iwe ndio adhabu yake, yeye na chama chake maana wote wawili kwa pamoja. Lakini na chama pia ni lazima tukiwekee misingi ya kukizuwia kutoshiriki uchaguzi kwa vipindi viwili, tutizame namna sheria ya vyama vya siasa inavyoelekeza, lakini lazima sisi sheria yetu ielekee huko tusiwe tuna majaribu.

Kifungu cha (c) mtu mwengine. Hapa hatujui mtu gani, lakini tunakwenda na tafsiri hiyo hiyo, hapa kawekewa adhabu ya miezi 18 ni kidogo. Huyo mtu mwengine utakayemtafuta kwa niaba akafanye kazi kama ambavyo wanafanya wenziwe, huyu angalau mapendekezo yangu yawe kwa miaka mitano.

Lakini mapendekezo yangu ya mwisho ya kuongeza kifungu haya yote yanayofanyika chama cha siasa kipo, huyu mgombea yupo. Lakini matangazo hayawezi kwenda kama hakuna mtu wa chombo cha habari, lazima tumdhibiti kwenye eneo hilo. Kwa hivyo, kifungu cha (d) tuongeze tu, chombo cha habari kitakachotumika kutangaza matokeo, lazima nacho tukipige faini ya shilingi milioni 100, nidhamu iwepo kwa maeneo yote. Sasa tukiwabana hawa toka hayo maeneo matatu, lakini eneo ambalo naliongeza ni la chombo cha habari, maana hawezi kujitangazia kawaida huyu lazima atatumia chombo cha habari. Kwa hivyo, chombo cha habari kitakachojihusisha na hili basi tukiainishe kiwe ni miongoni mwa vile vyombo ambavyo tunavipa adhabu.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu ulikuwa ni mdogo kwa sababu maeneo mengi waliyasema wenzangu na nilisema niseme machache tu, lakini yenye

manufaa. Haya maeneo mawili mimi Mhe. Waziri nakamata shilingi ya mswada wako, lile nililolisema na hili eneo la adhabu ni lazima tukubaliane na tuweke nidhamu katika nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa mchango wako, Waheshimiwa Wajumbe, muda tuliokuwa nao ni karibu nusu saa lakini naomba kabla sijaahirisha nimuachie Mhe. Mwanasheria Mkuu atumie kanuni ya kutengua muda, ili tuliahirishe Baraza hili kwa muda huu kwa kumpa nafasi Mhe. Waziri na watendaji wake, ili waje watuletee majumuisho kwa hoja mbali mbali zilizotolewa na wajumbe. Mhe. Mwanasheria Mkuu.

KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kutenga kando kanuni ya muda, kanuni ya 23 ili tumpe fursa Mhe. Waziri kwenda kujitayarisha na kuja kufanya majumuisho jioni baada ya michango mingi iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe.

Kwa msingi huo Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ya kutenga kando kanuni ya muda ya 23, ili tukiahirishe kikao hiki sasa hivi mpaka saa 11 jioni. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo. Wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nikiahirishe kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 6:23 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, asubuhi tulikuwa tumebakisha watu wawili, lakini walikuwa hawapo na hivi sasa pia naona hawapo. Kwahivyo, naomba nimuite Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kuniruhusu, lakini nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa utukufu na mwenye rehema kutujaalia uzima na afya ya kuweza tena

kutukutanisha hapa leo katika Baraza lako hili tukufu, wakati tunahitimisha Mswada wa kufuta Sheria ya Uchaguzi No. 11 ya Mwaka 1984 na kutunga Sheria mpya ya Uchaguzi ya mwaka 2017.

Aidha, niendelee kumshukuru sana Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa imani yake, busara zake na hikima zake za kuongoza nchi yetu. Vilevile, nimshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa uongozi wake na namna anavyomsaidia Mhe. Rais katika kutekeleza majukumu yake. Mhe. Spika, uniruhusu niishukuru sana na kuipongeza Kamati yetu ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mhe. Omar Seif Abeid. Kamati hii siku zote imekuwa karibu na sisi, lakini katika suala hili la mswada huu iliuchambua na kuujadili na kutoa mapendekezo ya manufaa yaliyotuwezesha kufikia hatua hii ambayo imetufikia. *(Makofi)*

Lakini shukurani zangu maalum ziende kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia hoja hii. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba niwatambue.

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk kwa niaba ya kamati
2. Mhe. Ali Suleiman Ali
3. Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
4. Mhe. Rashid Makame Shamsi
5. Mhe. Husein Ibrahim Makungu
6. Mhe. Simai Mohammed Said
7. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali
8. Mhe. Asha Abdalla Mussa
9. Mhe. Suleiman Sarahan Said
10. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
11. Mhe. Suleiman Makame Ali
12. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
13. Mhe. Hamza Hassan Juma
14. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
15. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
16. Mhe. Miraji Khamis Mussa

Mhe. Spika, hawa ni waliochangia moja kwa moja na wale waliochangia kwa maandishi Mhe. Spika, naomba pia uniruhusu niwataje.

1. Mhe. Mohammed Said Mohammed
2. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
3. Mhe. Saada Ramadhani Mwenda
4. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
5. Mhe. Waziri Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
6. Mhe. Ussi Yahaya Haji
7. Mhe. Hamza Hassan Juma

Mhe. Spika, baada ya kuwashukuru wajumbe wetu hawa kwa michango yao ya kina, naamini imetuwezesha kufikia hatima nzuri ya mswada huu wa sheria, michango yao

Mhe. Spika, inaonyesha wazi itajenga katika kuimarisha sheria yetu hii. Historia ya Uchaguzi kama nilivyokwisha eleza imeanza muda mrefu hapa Zanzibar tokea katika miaka ya 50, na wakati wote huo katika shughuli zetu za uchaguzi tumekuwa tukifanya marekebisho ya mara kwa mara katika Sheria za Uchaguzi, kwa ajili ya kurekebisha kasoro zinazojitokeza, ili tuendane na wakati na dhamira ni kutoa fursa kwa wananchi wetu kuweza kuitumia vizuri demokrasia yao.

Mhe. Spika, katika nchi yetu tumefanya marekebisho ya sheria mara nyingi baada ya Mapinduzi matukufu tokea katika mfumo wa chama kimoja, na katika mfumo wa vyama vingi vya siasa. Nia na dhamira ni kuondoa kasoro na kurekebisha, ili kuboresha kuwe na sheria bora. Mhe. Spika, nataka niseme leo, hayo ndio yaliyokuwa madhumuni makubwa na malengo ya sheria hii, kuondosha kasoro zilizokuwepo na kuweka sheria iliyo bora zaidi itakayoondoa manung'uniko na malalamiko mbalimbali yaliyojitokeza na hiyo inatokana na ripoti mbalimbali Mhe. Spika, zilizofanywa na Tume yetu ya Uchaguzi kwa kusikiliza wadau mbalimbali wanaohusiana na vyama vya siasa na wananchi wengine na matokeo yake yanayojitokeza katika chaguzi mbalimbali zilizofanyika.

Ndio maana kutokana na mapendekezo yao serikali, ikaona upo umuhimu wa kufanya marekebisho makubwa ya sheria na kufuta sheria iliyokuwepo na kuanzisha sheria mpya, na si kwa maana nyengine yoyote zaidi ya kuwa na sheria bora inayotoa demokrasia zaidi, inayotoa nafasi kwa wananchi wa Zanzibar kuchagua viongozi wao wanaowataka. Mengine yote yatakuwa ni maneno ya wanayoona wao lakini hayo ndio madhumuni ya serikali kuleta sheria hii na naamini Baraza lako tukufu limeuona umuhimu huo na ndio maana ikauchangia na kufanya marekebisho yaliyowezekana kufanyika.

Mhe. Spika, michango katika Baraza lako tukufu iliyotolewa na Wajumbe iligusa maeneo matatu makubwa eneo moja la utendaji, eneo moja linahusu masuala ya Katiba na eneo la tatu linalohusu sheria yenyewe. Yale yanayohusu masuala ya kiutendaji nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba watakwenda kuyafanyia kazi na yale yote wajumbe waliyoshauri tunayachukua tukayafanyie kazi vizuri, ili utekelezaji uwe mzuri na lile lengo na madhumuni ya kuanzisha sheria mpya liweze kufikiwa.

Kwa upande wa yale yanayohusu mambo ya kikatiba kwa upande wetu tunayachukua na pale, ambapo itaamuliwa kutoka mabadiliko ya kikatiba nadhani mambo haya kwa wingi wake na umuhimu wake yatapewa umuhimu wake, kwasababu mwisho wa siku tutakapofanya mabadiliko yoyote ya kikatiba Mhe. Spika, yanakuja kwenye Baraza hili ninavyoamini maoni ya wajumbe ndio yataendelea kupewa nafasi yake.

Mhe. Spika, yanayohusu sheria hii nitajaribu kuyatolea ufafanuzi kwa kadri itakavyowezekana. Lakini niseme kabla ya kuendelea kwamba Katiba ndio sheria mama na haiwezekani sheria ikawa na nguvu mbele ya Katiba, kwa mujibu wa kifungu cha nne cha Katiba yetu ya Zanzibar kimeeleza wazi na naomba ninukuu.

Kifungu cha nne kinasema hivi:

> "Katiba hii ni Katiba ya Zanzibar na itakuwa na nguvu za kisheria nchini kote, na isipokuwa kutokana na kifungu cha 80 ikiwa sheria yoyote inatofautiana na

Katiba hii basi Katiba hii ndio itakuwa na nguvu na sheria hiyo itakuwa batili kwa kiwango kile ambacho kinahitilafiana".

Kwahivyo, suala lolote ambalo linahusu Katiba hatuwezi kuliingiza katika sheria hii bado katiba itasimama na itakuwa na nguvu kuliko sheria.

Mhe. Spika, katika sheria mambo yaliyozungumziwa sana yalikuwa yanahusu.;

1. Kujitangazia matokeo ya uchaguzi
2. Sifa za kugombea hasa umri
3. Suala la waangalizi wa uchaguzi kulipia ada wanapokubaliwa
4. Masuala ya adhabu na makosa pamoja na mengine mbalimbali ambayo tutajitahidi tuyajibu kadiri itakavyowezekana.

Mhe. Spika, nikianza na hili la kujitangazia matokeo Mhe. Ali Suleima Ali alianza kulisema hili na waheshimiwa wengine mbalimbali walilizungumzia hili akiwemo Mhe. Simai Mohammed Said, Mhe. Hassan Khamis Hafidh, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) na Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) walizungumzia sana suala la kujitangazia matokeo ya uchaguzi.

Bahati nzuri Mhe. Spika, Sheria hii katika kifungu 127(1) cha Sheria hii kinapiga marufuku kwa mgombea, Chama cha Siasa, Taasisi, au mtu mwengine yeyote kutangaza matokeo ya uchaguzi kwa njia yoyote ile ya mawasiliano kabla ya kutangazwa rasmi na Tume. Sasa pale ambapo tunaposema mawasiliano kuna baadhi ya wenzetu walisema kwanini tusitaje redio na *television* na kadhalika. Mawasiliano ina maana pana sana ni pamoja na redio, TV, mitando ya kijamii na aina yoyote ya mawasiliano hata hii ninayosema mimi na wewe ukisikia ndio mawasiliano kwa hivyo hii ina maana pana zaidi, na hata katika tafsiri imeonesha upeo wa maana hii kwa msingi huo neno mawasiliano ni vizuri likabaki kwa sababu linatoa maana kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika kifungu cha 27(2) (a) mpaka (c) kinaonyesha adhabu za wale ambao watajitangazia matokeo. Kwa mfano, kwa mgombea ana adhabu ya kifungo kisichopungua miaka mitano na faini isiyopungua shilingi 50,000,000/=, kwahivyo ukiwa mgombea na ukajitangazia matokeo basi ujue una kifungo kisichopungua miaka mitano, na faini isiyopungua milioni hamsini. Kwa chama cha siasa kitakachojitangazia matokeo kitapata adhabu ya faini isiyopungua milioni mia moja na kwa mtu mwengine wa kawaida anayejisemea semea lazima tuwe na hadhari ana kifungu cha miezi 18. Kwahivyo, usije ukajitokea tu ukatangaza matokeo mitaani huko ukafikiri unasema maneno maneno, unayo adhabu hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakubaliane na adhabu hizi, kwasababu sheria ya nyuma adhabu ilikuwa ndogo, naamini kwa adhabu hii kwa wale wenye mtindo wa kufanya makosa haya watapata adhabu ya kutosha itakayowapa stahili ya kuacha kufanya makosa hayo. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Spika, lilikuja shauri hapa kwasababu ilionekana kwamba mara nyingi utekelezaji unakuwa mdogo kutokana na makosa haya kutokufika mahakamani na adhabu ikatafsiriwa, kwa hivyo likaja shauri lililozungumzwa na Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Hassan Khamis Hafidh, kwamba lazima lipewe nguvu suala la utekelezaji na sheria isimamiwe vizuri. Kutokana na hali hiyo, likatoka shauri kwamba basi kiongezwe kifungu chengine cha tatu kinachosema, "tume au mtu mwengine yoyote atakayeyaona masharti ya kifungu cha 27(1) na 27(2) yamevunjwa atatoa taarifa katika kituo cha Polisi, ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya mgombea mtu au taasisi iliyovunja masharti haya".

Maana yake yeyote katika raia wa nchi hii au mtu yeyote atakayeona sheria hiyo ya kujitangazia imevunjwa mtu huyo ana haki ya kwenda kituo cha Polisi na kutoa taarifa, na sasa Polisi wachukue hatua zinazofaa. Mhe. Spika, kupitia Baraza lako tukufu napenda nimuagize Kamishna wa Polisi ahakikishe kwamba wale wanaovunja sheria wahalifu wanapelekwa katika vyombo vya sheria, uchunguzi unafanywa ushahidi unakamilika kwa taratibu zilizopo za kisheria watu hao wapelekwe kwenye vyombo vya sheria bila ya kujali mtu huyo ni nani. *(Makofi)*

Suala jengine ambalo limezungumzwa sana Mhe.Spika, ni suala la sifa za kugombea na hasa kwenye masuala ya umri Waheshimiwa Wajumbe wengi wamechangia kwenye eneo hili, na wakielezea hasa kwamba wale wananchi waliofikia zaidi ya umri wa miaka 70 na kuendelea wasipewe haki ya kugombea nafasi ya urais. Mhe. Spika, kwa kuwa sifa za kugombea nafasi ya urais na nafasi nyengine za uwakilishi zimo ndani ya Katiba kifungu 26(1) cha Katiba yetu (a) mpaka (d) kinaelezea sifa za mtu ambae atakuwa Rais wa Zanzibar. Vilevile, katika sheria yetu hii kifungu cha 43 kimezichukua kama zilivyo katika katiba sifa zile zikaiweka katika sheria hii. Sasa kwasababu sheria haina nguvu mbele ya Katiba hatuwezi kuongeza mengine wala kupunguza kutokana na utaratibu ule wa Kikatiba uliomo katika kifungu cha 26(1).

Kwa msingi huo ni pale tu ambapo tukihitaji kuongeza sifa inatubidi tufanye mabadiliko katika Katiba ndipo tutakapoweza kurekebisha kwenye utaratibu wa sheria, kwa sasa sheria inatufunga na imeeleza wazi sifa za mgombea urais. Kwahiyo, kwa sasa ni umri wa miaka 40 kuanzia na miaka yoyote utakayokuwa nayo alimradi una uwezo wa kwenda kuchukua fomu ruksa chama chako kitatizama je, mtu mwenye umri huu kwa leo tena anatufaa hayo ni maamuzi ya vyama vya siasa watajijua, lakini sifa hizo zimo kwa mujibu wa Katiba.

Kuhusu kuwa Mzanzibari wa kuzaliwa ndio upate nafasi ya kugombea uwakilishi bado vilevile Sheria No. 5 ya mwaka 1985 imeeleza na imeweka masharti ya nani Mzanzibari upatikanaji wake na upoteaji wake na hivyo ndivyo anavyopatikana Mzanzibari. Lakini kifungu cha 6(a) cha Katiba kinatambua kuwepo kwa Mzanzibari na ndicho kilichoelekeza kutungwa kwa Sheria ya Mzanzibari

Mhe. Spika, sifa za Mwakilishi zinaelezwa wazi katika kifungu cha 68 cha Katiba yetu. Kwahivyo, kwetu sisi sifa zile ambazo zinatoa kuwa Mwakilishi ni sifa za Kikatiba

zimeelezwa ndani ya Katiba. Sasa kama tunataka kufanya maamuzi yeyote ya kubadilisha sifa ya mwakilishi inabidi twende tukafanye mabadiliko ya Kikatiba, hilo ni jukumu lenu Waheshimiwa Wawakilishi.

Sasa hapa tunachosimamia ni kwamba lazima matakwa ya Katiba yaheshimiwe, kwasababu hakuna sheria itakayokuwa na nguvu mbele ya Katiba hata tukikiweka hicho kifungu kitakuwa batili kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, pia katika eneo hili kulitajwa suala la afya ya mtu. Mimi nataka niseme hakuna mmoja wetu mwenye dhamana ya afya. Afya zetu sote mwenye dhamana ni Mwenyezi Mungu, unaweza ukaamka leo mzima kesho ukaumwa. Mtu mwenyewe atajijua kwamba afya yangu hainuruhusu kuingia kugombea katika kinyang'anyiro cha kugombea nafasi hizi kubwa hususan za urahisi. Asiyejijua huyo hata wananchi maisha hawatampa kura watakapomuona kwamba mtu huyu kwa hali yake sasa ilivyo, afya yake, na umri umeshapitilia sana, basi ni tatizo. Kusema kweli dunia ya leo watu ni wajuzi wa mambo, wanachambua mambo, wataamua wenyewe watakavyoona inafaa. Lakini suala la afya mimi nadhani tusiliingize katika sheria yetu hii, leo unaweza ukawa mzima kesho hujui utaamka vipi.

Mhe. Spika, pia tulipata maoni ya kamati. Kamati katika mapendekezo mengi kulikuwa kuna mapendekezo mawili makubwa. Moja ilikuwa pendekezo la kututaka taasisi za kidini sizishirikishwe katika uangalizi wa uchaguzi. Sisi tumeona wazo hili zuri, viongozi wetu wa dini na watu wa dini wao wende wakahamasishe amani, utulivu, ummoja wa nchi itakuwa vizuri zaidi wakati wa uchaguzi kuliko kuwa wao ni sehemu ya kuangalia uchaguzi, hasa kwa mazingira yetu ya Zanzibar. Kwahiyo, sisi tumekubaliana sana na wazo hili, hivyo tunakubali kuongeza katika kifungu kile cha 100 kifungu cha tano ambacho kitaweka bayana kukataza taasisi za kidini kuwa waangalizi wa uchaguzi. *(Makofi)*

Hivyo, tunakubaliana na mawazo ambayo yametolewa katika eneo hili na kamati yetu na tutaongeza kifungu cha 5 katika kifungu cha 100 cha sheria hii, ili taasisi za kidini zisiwe waangalizi wa uchaguzi. Hivyo itawekwa vizuri na Mwanasheria Mkuu kwa utaratibu wa kisheria ili haya maneno yasomeke kwa vizuri.

Pendekezo la pili nalo kubwa la Kamati walitaka mashauri ya migogoro yanapotokea kwa Uwakilishi na Udiwani yasipelekwe Mahakamani, badala yake yamalizwe na Tume ya Uchaguzi. Jambo hili nalo linagongana na msingi wa Kikatiba. Maana Katiba ndiyo iliyotoa maelekezo ya uwezo kuwa Tume ifanye nini. Pendekezo hilo linapingana na Katiba kifungu cha 72(1) cha Katiba inayoelekeza Tume namna ya kufanya kwa mujibu wa Katiba.

Mhe. Spika, Kifungu cha 72(1) kinaeleza kwamba "Mahakama Kuu ya Zanzibar ndiyo pekee yenye mamlaka na uwezo wa kusikiliza na kuamua mashauri yote yanayohusiana na uchaguzi Zanzibar". Isipokuwa Katiba hiyo hiyo imetoa nafasi katika kifungu cha 34(7) "maamuzi ya Tume kwamba Tume inapomtangaza Rais hakuna Mahakama yoyote itayokuwa na mamlaka ya kuchunguza kuchaguliwa kwake". Kwahiyo, kwa upande wa

Wawakilishi na Madiwani malalamiko yao ni lazima kwenda Mahakamani. Kwa upande wa nafasi ya urais hayo hakutokuwa na Mahakama itakayoweza kusikiliza malalamiko ya matokeo hayo.

Kwahiyo, kwa hili Kamati yangu ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa hatutoweza kuliingiza katika sheria kwasababu hata ukiliingiza litagongana na utaratibu wa Kikatiba, sheria hiyo haitokuwa na nguvu. Naomba tukubaliana na matakwa ya Katiba ya kifungu cha 4 cha Katiba yetu inayosema sheria haina nguvu mbele ya Katiba. Kwa msingi huo naomba kamati yangu tuendelee kukubaliana na mapendekezo kama yalivyo katika sheria hiyo.

Mhe. Spika, jengine kubwa lilizungumzwa kuhusu Muundo wa Tume, limezungumzwa sana na ndugu yangu MBM Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum), Mhe. Miraji Khamis Mussa na wengine, kuhusu muundo wa Tume. Nalo la Muundo wa Tume ni suala la Kikatiba, katika Katiba ya Zanzibar kifungu 119 (1) kinaeleze kuhusu Muundo wa Tume ya Uchaguzi. Ushauri ni mzuri, siyo vizuri kuwa na Tume yenye wajumbe wanaotokana na vyama vya siasa. Lakini sheria haiwezi kuiongoza Katiba kwenye hili itabidi Wajumbe tutafakari namna ya kubadilisha Katiba yetu ndipo tuwe na uwezo sasa wa kubadili muundo wa Tume, kwa sasa Katiba ina nguvu mbele ya sheria.

Mhe. Spika, mawazo ni mazuri pale itakapotokezea kujadili suala la Katiba hapo tutaweza kulizungumza jambo hili. Tumeona uzoefu uliotokea kwa kuwemo wajumbe wanaotokana na vyama vya siasa katika Tume ya Uchaguzi mara nyingi wanakuwa kila mmoja anasimamia kuvutia upande wa chama chake. Ni vizuri sana jambo hili huko mbele tukafikiria uwezo wa kuchagua wajumbe wa Tume uwe mikononi wa Rais wetu. Lakini hilo hatuwezi kufanya mpaka pale tutakapofanya mabadiliko ya Katiba.

Mhe. Spika, vile vile katika hili rafiki yangu wa siku nyingi sana, mzoefu katika Baraza hili Mhe. Hamza Hassan Juma yeye alikuja na wazo kwamba kipindi hichi cha uchaguzi kisiwe miaka mitano bali tuwe miaka 7. Wazo ni zuri sana na uzuri wake halina mpaka, lakini kifungu cha Katiba 28(3) kinaelezea muda wa Urais ni vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Ndio kikwazo chetu hapa. Kweli miaka saba ni muda mzuri wa kufanya shughuli zetu hasa kwa nchi masikini kama zetu, kufanya chaguzi mara kwa mara miaka mitano mitano lina tatizo lake, lakini miaka saba inakuwa ni muda mrefu kwa kufikiria vizuri, kwa kupanga mambo vizuri na matokeo mazuri kwa wananchi, kuliko kila baada ya miaka mitano kuwabebesha wananchi uzito. Hususan kwa Zanzibar kila tunapofanya uchaguzi tunavuna vutana.

Ndio maana Mzee Karume alisema uchaguzi baada ya miaka 50 alijua kuna mivutano katika masuala haya. Lakini sasa hivi kwa sababu dunia hii ni ya kidemokrasia na kadhalika, mambo haya yanakwenda kwa taratibu za Kikatiba na lazima tuheshimu Katiba yetu. Katiba yetu inasema miaka mitano, kwa vyovyote vile itabadi kwa sasa iwe miaka mitano. Lakini pale Baraza hili tukufu litakapoona mawazo mazuri ya Mhe. Hamza Hassan Juma ya kuwa hiyo miaka saba, basi tutakapofikiri kubadili Katiba ndipo pale hayo yanaweza kufanyika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumzia sana suala la rushwa katika sheria hii. Nakubaliana sana kwasababu sasa hivi ni wakati wa mapambano dhidi ya rushwa. Lakini sheria yetu kifungu 130 tokea namba 1–5 katika sheria hii kinazungumzia sana mpambano dhidi ya rushwa na ipo *fine* kwa wale ambao watatoa rushwa au watapokea rushwa isiyozidi milioni 5 au kifungo vilevile kisichozidi cha mwaka mmoja na kisichopungua miezi 6. Lakini sheria ya zamani ilikuwa ina adhabu ndogo ya hii.

Mhe. Spika, mimi namuomba Mhe. Hamza Hassan tukubaliane kwamba adhabu iliyokuwepo sasa inakidhi haja na zipo sheria nyengine mbali mbali zinazosimamia mapambano dhidi ya rushwa na mwisho wa siku wale watakaotuhumiwa na rushwa watakwenda Mahakamani watapewa adhabu stahili kutokana na rushwa waliyoifanya. Nimuombe Mhe. Hamza Hassan kwamba ushauri wake ni mzuri na sote tunakubaliana tupambene dhidi ya rushwa lakini mwisho wa siku kutokana na sheria zetu zile zile ndizo atakazopelekwa mtu Mahakamani akapewa adhabu kwa mujibu wa sheria zilivyowekwa.

Mhe. Spika, kuhusu la waangalizi wa uchaguzi. Waangalizi wa uchaguzi wa ndani na nje ni kweli walikuwa na mtindo hususan kutoka nje wanapokuja wanakusanyika katika eneo la Mkoa wa Mjini Magharibi na sana sana sehemu za Mijini. Hawakuwa na utaratibu wa kwenda kuangalia sehemu nyengine ambapo uchaguzi vile vile ulikuwa unaendelea. Hata huu uchaguzi uliomalizika waangalizi wa nje wote walijikusanya hapa Mjini Magharibi, Pemba kule hakukuwa na muangalizi wa uchaguzi kama walikuwepo ni mmoja au wawili, lakini hapa walikuwepo wengi sana.

Kutokana na uzoefu huu sasa sheria hii imeona upo umuhimu wa kuwekea taratibu za kisheria waangalizi wa uchaguzi. Kwahivyo, tume kwa mujibu wa sheria hii katika kifungu 102 kinaeleza vizuri namna ya waangalizi watakavyopewa majukumu yao ya kusimamia au kuangalia uchaguzi. Kimeeleza vizuri katika kifungu 101 – 105 kinaeleza vizuri namna ya utekelezaji wanavyotakiwa kufanya waangalizi wa uchaguzi wanapokuja kuangalia uchaguzi kwetu. Watapangiwa maeneo yao, watapewa kibali maalum na watakapokwenda eneo jengine atavunja sheria, atanyang'anywa kibali hicho na kadhalika. Hivyo, kwenye eneo hili sasa limepangiwa vizuri.

Mhe. Spika, ulikuwepo ushauri kwenye sheria tumesema uwepo uzoefu wa miaka mitatu, lakini tukapewa ushauri kwamba waangalizi iwe kwa vipindi vitatu, ushauri ule sisi tunaupokea, tunaukubali. Kwa msingi huo utatengenezea utaratibu mzuri wa kimaandishi ya kisheria, ili iwe ni vipindi vitatu badala ya miaka mitatu. Ushauri tunaupokea na Mwanasheria Mkuu ananisikiliza vizuri atakuwa na maneno mazuri ya kuyasema badala ya hii ya miaka mitatu.

Vilevile, kutakuwa na kitambulisho maalum utakachopewa kutokana na eneo lako kwa wilaya uliyopangiwa, ikiwa wilaya hii rangi yake ni kijani kitambulisho chake kitakuwa ni kijani, wilaya ile rangi yake nyeusi, kitambulisho chake kitakuwa cheusi, ile nyeupe kitambulisho chake kitakuwa cheupe, kila wilaya na kitambulisho chake. Kutokuwa muangalizi sio ikawa unafanya unavyotaka weye kwa mujibu wa sheria hii, sheria inakuongoza namna ya kufanya na kibali chako utaangikiwa na ni lazima ulete maombi ukubaliwe. Tukiona muangalizi huyu mkorofi anakwenda kinyume na utaratibu na haleti

ripoti hapo nyuma alizotakiwa aziandikie azilete kwa tume, huyo hatufai na hatopewa kibali hicho. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia Waheshimiwa Wajumbe walikuwa na ushauri kwamba tutoze ada kwa hawa wanaokuja kuangalia. Waheshimiwa Wajumbe, hili tuachieni tulipange liwe kwenye Kanuni, tuwaachie tume waone ni ada gani watatoza kwa wanaokuja kuangalia uchaguzi. Lakini wengi huwa tunawaalika kwasababu unamualika na unamtoza tena tutajua kwa mujibu wa kanuni tutakazoziweka.

Kuhusu kufutwa kifungu cha 73 cha sheria hii. Tunaomba Waheshimiwa Wajumbe, kifungu hichi kibaki. Kifungu hichi kinatilia mkazo masharti yaliyowekwa na kifungu cha 71 cha sheria kuhusu ununuzi wa vifaa vya uchaguzi. Kifungu cha 73 kinaweka vizuri masharti ya ununuzi huwo. Kwahiyo, naomba sana tukiachie kifungu cha 73.

Mhe. Spika, kuhusu Matumizi ya Tume kwa kuwa Sheria hii sana inaonesha namna na uendeshaji uchaguzi, lakini ile sheria tuliyoipitisha hapa Nam. 1 ya mwaka 2007, Sheria ya Afisi ya Tume, ile ndiyo imeonesha namna ya matumizi ya Tume ya Uchaguzi. Licha ya kuwa Sheria ile kuonesha namna ya matumizi ya Tume ya Uchaguzi pia tunayo Sheria Kuu inayohusiana na mambo ya Fedha ya Mwaka 2016 ile ni dira ya matumizi yote ya Taasisi za Umma. Pamoja na Sheria ya Ununuzi na Uhaulishaji, sheria zote hizo tatu bado zinasimama katika kusimamia matumizi bora ya serikali. Kwa msingi huwo sheria hii itasimamiwa kupitia sheria hizo na matumizi ya tume yatakwenda kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, jambo jengine limezungumzwa sana ni kuhusu mabango, *posters* na machapisho. Bahati nzuri Sheria hiyo katika kifungu cha 64(1) – (5) kinaelezea vizuri kuhusu mabango, *posters* na machapisho ya uchaguzi au wakati wa kampeni. Moja ambalo lilikuwa linafanyika na Waheshimiwa Wajumbe wamelisema sana ni ile kuja ukaona nyumba yako umebandikiwa bango ambalo hulitaki au picha ya mgombea ambaye humtaki, kuiyondosha ilikuwa ni mtihani kwa mujibu wa sheria. Kwa mujibu wa sheria hii inampa nguvu mmiliki wa eneo husika lazima kwanza ushauriane naye, atakapokubali akakupa idhini ndiyo utaweza kuweka makaratisi yako, ukimuwekea kinyume na hayo ni mkosa kwa mujibu wa sheria. Suala hili limeelezwa vizuri ndani ya sheria yetu hii ni lazima kupata idhini ya mwenye eneo husika ndiyo uweze kuweka mabango yako.

Vilevile, katika sheria hii tumeweka utaratibu wa kuweka vifaa vya uchaguzi katika maeneo mbali ya umma na namna ya kuviharibu baada ya uchaguzi. Kwahiyo, mambo yote yapo hayo, kwasababu wapo watu wanoharibu pia mabango ambayo yameshaweka kwa mujibu wa sheria na yashapata idhini ya wahusika na wakatokea kuyachana ama kuyaondoa, kufanya hivyo ni kosa na kwa mujibu wa sheria hii utapewa adhabu. *(Makofi)*

Kuhusu ukataji wa mipaka jambo hili liko wazi kikatiba Tume ya Uchaguzi imepewa uwezo kwa mujibu wa Katiba kifungu 124 kinaweza kufanya mapitio ya mipaka na

majina ya majimbo katika kipindi kati ya miaka minane na kumi, lakini inaweza kufanya hivyo wakati wowote inakapoona inafaa.

Kwahivyo, si lazima miaka minane na kumi kama kumeonekana kuna makosa katika mipaka ya majimbo tume ina uwezo wa kufanya hivyo. Mhe. Spika, ni vyema tuiwachie tume uwezo upo kama tunaona yapo majimbo yana kasoro tutawaeleza tume, na tume kwa mujibu wa katiba hii wanao uwezo wakati wowote, pale tume itakapoona kuchunguza idadi ya mipaka na majina ya majimbo hayo inaweza kufanya hivyo kwa hivyo tunaweza kurekebisha bila ya matatizo. Eneo hili limeoneka limelalamikiwa sana na Waheshimiwa Wajumbe, inaonekana yapo mapungufu, kwahiyo sasa ni wajibu wa tume wamesikia kilio cha wajumbe waanze kazi ya kufuatilia jambo hili.

Mhe. Spika, kuhusu wakala wa vyama vya siasa wakati wa uandikishaji Waheshimiwa Wajumbe hususan Mhe. Hussein Ibrahim Makungu alishauri tuondoshe kifungu hiki kinachotowa wakala wa vyama vya siasa katika uandikishaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, wazo hili lazima tulifikirie kwa upana wake maana kura ni mchakato na hasa hasa uchaguzi ni uandikishaji tukishafeli katika uandikishaji huna turufu tena masuala mazima ni kwenye uandiklishaji. Kwahiyo, kwa kukuza demokrasia na kuweka uwiano wa ushindani ulio sawa suala la kukataa mawakala wakati wa uandikishaji wa vyama ni gumu sana, linaweza kuletea mtihani mkubwa na maneno mengi. Mhe. Spika, nashauri Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tukubaliane na wakala wa vyama wawepo wakati wa uandikishaji, ni sawa sawa wakati wa kupiga kura hauna tafauti, lazima tuliomo humu ndani tuelewe umuhimu wa jambo hili ili nchi yetu iendelee katika hali ya usalama, utulivu na umoja.

Kuhusu kupiga kura mapema kuna kifungu pale 82 (1) tume imepewa uwezo itaweka utaratibu mzuri utakaoruhusu upigaji kura mapema, kwa ajili ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sote ni mashahidi kwamba vijana wetu au askari wetu walikuwa mara nyingi wamekosa kupiga kura, kwasababu ikifika wakati wa kupiga kura wanapangiwa maeneo nje ya maeneo yao ya kupiga kura na wanakwenda huko kwasababu ya kusimamia masuala ya ulinzi na usalama kwa manufaa yetu sote. Kutokana na utaratibu huu na kwasababu imetokana mara nyingi kukosa fursa hizo sasa tume itaweka utaratibu utakaoruhusu upigaji kura mapema, ili vyombo vyetu vya ulinzi na usalama viweze kupiga kura na baada ya hapo viweze kufanya kazi yake ya ulinzi na usalama, wapi watapiga kura watapangiwa na tume wenyewe kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Sheha kuwa wakala wa tume katika sheria hii sheha atakuwa wakala wa tume kifungu 14 (1) cha sheria hii kinamtambua sheha kuwa wakala wa Tume ya Uchaguzi wakati wa uandikishaji atakuwepo pale. Mhe. Spika, kwasababu tumepata ushauri na ushauri huu tumeuona ni mzuri wajumbe hapa walitaka pia sheha apate fursa wakati wa upigaji kura. Kwahiyo, tumeona tuongeza kifungu pale tuongeze maneno pale kwenye kifungu 77 (1) kitakachosema alikieleza vizuri Dkt. Mwinyi alitoa ushauri huo na akaeleza akasema hivi

'Sheha au mtu mwengine yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi na tume ataweza kuwepo kwenye kituo chza kupigia kura'. *(Makofi)*

Kwahivyo, hayo tunayoruhusiwa wakati wa kupiga kura na sheha atakuwemo naona hili ni wazo zuri litasaidia, kwasababu masheha wanawajua watu wetu wanawafahamu na ndio maana kwenye uandikishaji yupo na kwenye kupiga kura atakuwepo, ili kunusuru wajanja ambao hawana sifa za kupiga kura wasipige kura.

Vilevile, Mhe. Hamza Hassan Juma pia aliuliza swali kuhusu yale matokeo ya uchaguzi yanayo bandikwa kwenye vituo vya uchaguzi yatakuwemo na matokeo ya uraisi, ndiyo kwasababu yanahesabiwa yote ya uraisi yanahisabiwa, mwakilishi yanahisabiwa na diwani yanahisabiwa kwahiyo yatabandikwa na matokeo ya Rais katika vituo vya kuhesabia kura. Lakini hata usipobandika, kwenye ile fomu kila mmoja anakuwa amepewa kopi yake wale mawakala wa vyama wanaokuja pale ana saini idadi ya kura ulizozipata katika kituo husika. Kwahiyo, tayari idadi inajulikana, hivyo sisi tunaona bado ni busara kuendelea kubandika matokeo kwenye vituo vile lakini bado Baraza letu tukufu linaweza kufikiria vyenginevyo inavyoona inafaa.

Lakini, ile inasaidia sana kufichuka uhalifu hasa kwenye vituo vya Pemba watu wanabadili sana matokeo, lakini inapobandikwa kwenye vitu baada ya kuhesabiwa yake matokeo yanasaidia, lakini Baraaza Tukufu ndilo linalofanya maamuzi ya mwisho ya sheria nikiona hamuonelei kubandikwa katika vituo mnaweza kupendekeza vyenginevyo.

Mhe. Spika, pia Mhe. Hamza Hassan Juma alishauri kuhusu marekebisho ya *marginal note* katika kifungu cha 113 kuhusu malalamiko ya uchaguzi, akataka tuongeze maneno pale yaongezeke maneno ya mwakilishi na diwani. Kwakweli, kama nilivyosema awali kwakuwa kifungu 72(1) ndicho kinachoeleza kilichopita tume uwezo wa malamimiko yetu kwenda mahakamani kwa msingi huo vile kilivyomo kwenye sheria ndio kilopatikana kwenye katiba 72 (1) kwa hivyo kilivyopo kwenye sheria kipo sahihi hatuwezi kuongeza zaidi ya pale.

Baada ya maelezo hayo yako maelezo mengine ya makosa ya kiuandishi ambayo Waheshimiwa Wajumbe walishauri katika kifungu 12 (2), kifungu 15 (1) na kifungu 28 (9). Maoni yao yamepokelewa na yatafanyiwa kazi, ili kufanya marekebisho kwa ufupi tunakubaliana na marekebisho hayo. Vilevile, makosa ya kiundishi tunakubaliana kufanya marekebisho katika kifungu cha 3, kifungu cha 31(2)(a) na kifungu 33 lakini kifungu cha 43 tunashauri kibakie kama kilivyo kwasababu Sheria ya Vyama vya Siasa inaweza kubadilika wakati wowote.

Mhe. Spika, kifungu cha 47 (4) kuongeza neno katika kanuni za tume tumekubaliana kuongeza neno katika Kanuni za Tume, kama ilivyopendekezwa ni kusema katika Kanuni za Tume, kifungu 71 (1) kuongeza neno na penye ubora tumekubaliana kuongeza neno na vyenye ubora kama ilivyopendekezwa.

Kuhusu kukifuta kifungu 73 tumeendelea kuwaomba waheshimiwa wajumbe kifungu kile kibaki kwasababu kama nilivyosema kinatilia mkazo kila kifungu cha 71. Kifungu

74 (2 b) wajumbe walishauri kiondoshwe. Tunaomba Waheshimiwa Wajumbe kifungu hiki kibaki kwani, kinalinda misingi ya usiri wa kura katika uchanguzi za kidemokrasia.

Kifungu cha 102 (d) kama nilivyosema mapema tunakubaliana na pendekezo kuhusu adhabu kuhusiana na elimu ya wapiga kura iongezwe. Waheshimiwa Wajumbe tunaomba hii ibaki kama ilivyo katika sheria masharti ya fedha nimeeleza, kuhusu kifungu 15 kifutwe tunashauri kifungu kibaki kama kilivyo sasa kwasababu kinaboresha mfumo wa demokrasia ambao unatoa fursa za ushirikishaji wa wadau.

Kifungu cha (13) eneo la soko lisiruhusiwe kubandika mabango ya kampeni kifungu hiki tunashauri kibaki kama kilivyo kwasababu eneo la soko ni moja kati ya maeneo ya umma ambalo linakusanya watu wenye mitizamo tofauti. Ulinzi katika vituo uongezwe tunalipokea tutahakikisha ulinzi unaongezwa katika vituo vyetu, hatua zote zinachukuliwa hizi za kupiga kura siku moja kabla ni kwasababu za kuimarisha ulinzi katika vituo vyetu vya kupigia kura.

Kuhusu sheria haijaweka mipaka ya kazi za Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi, Sheria ya kuanzisha Ofisi ya Tume ya Uchaguzi imefafanua na kuweka ufafanuzi huo ya mwaka 2017 sheria namba 1 ya 2017 inaelezea vizuri jambo hili.

Kuhusu tafsiri ya neno Mzanzibari na Idara Maalum yatafsiriwe pendekezo hili tunalikubali. Kifungu cha 17 (5) mapendekezo yamekubaliwa. Kifungu cha 35 (3) neno mtu lisomeke mpiga kura maapendekezo yamekubaliwa. Kifungu 36 (3) neno kulingana katika mstari wa mwanzo lisomeke kwa na neno kulingana katika mstari wa pili lisomeke kutokana mapendekezo yamekubaliwa. Kifungu 36 (5) liongezwe neno uwadilifu mara baada ya neo siri mapendekezo yamekubakubaliwa na la mwisho kifungu cha 100 (2 d) turekebishe baina ya neno masuala la uangalizi iwe neno ya badala ya wa.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika nataka nirudie tena nikushukuru wewe, kuwashukuru wajumbe kwa namna walivyochangia sheria hii, naamini watakapoipitisha sheria hii itasaidia sana kufanya chaguzi zetu vizuri kwa uadilifu, kwa uwazi na uhuru naamini itajenga misingi ya kufanya nchi yetu kuwa hali ya amani na utulivu mkubwa.

Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana naomba kutowa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono naomba niwahoji wale wote wanokubaliana na hoja ya mheshimiwa wanyanyuwe mikono, wanaokataa walokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kupitia mswada huu kifungu kwa kifungu, Mhe. Spika naomba kutowa hoja.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa sababu ya ukubwa wa Mswada wenyewe tunakuwa tunahoji kwa sehemu, kwa hiyo vile vifungu ambavyo waheshimiwa watataka wanyanyuke ile sehemu ikitajwa kama kile kifungu kimo mule ndani mheshimiwa ataweza kuonyesha *interest* kwa buti.

Mswada wa Sheria ya Uchaguzi, 2017

SURA YA KWANZA

Masharti ya Utangulizi

Kifungu 1 - 4 Pamoja na marekebisho yake

SURA YA PILI

Sehemu ya Kwanza

Daftari la Kudumu la Wapigakura

Kifungu 5 - 10 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Pili

Uandikishaji wa Wapigakura

Kifungu 11 - 24

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti nilichangia kifungu cha namba 15 (1) na nikatowa maelezo ya kina sana juu ya kuondoshwa kwa wakala wa vyama vya siasa. Lakini nililolipata kwa waziri anakuja na kauli za ku-*compromise* katika sheria za nchi kitu ambacho kimenisikitisha sana. Hoja yangu na nilisoma kifungu cha Katiba 7(1) kwa kila Mzanzibari aliyetimiza umri wa miaka kumi na nane (18) ana haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu inaanzia hapo ukiangalia kifungu cha Katiba kinamtaja Mzanzibari na wala hakimtaji mwanachama wa chama cha siasa, tunapokuja kutunga sheria Mzanzibari huyu ukamtilia wakala wa vyama vya siasa katika uandikishaji maana hata huo mstakabali wa kupingina na Katiba tunauanzia hapo. Wakala ambaye sisi tulikuwa tumemuona ni yule wakala wa serikali na lile daftari la serikali ni sheha. Hoja

yangu tukasema kifungu hiki kifutwe, kwasababu kinakwenda katika kushabikia na kuondoa ile taswira nzima. Maana hapa tukamtia wakala wa vyama vya siasa.

Lakini hapo hapo Mhe. Mwenyekiti ukifungua kifungu mbele tu, katika utaratibu huo huo wa 17(5) uamuzi wa tume juu ya masuala ya uandikishaji uliofanywa chini ya kifungu hiki utakuwa wa mwisho na hautajadiliwa na mtu au taasisi yoyote. Huyu wakala tunayemuingiza hapa wa chama cha siasa na mwisho tunatoa wiki moja ya kuangalia ile taswira ya kuonekana kama wewe una tatizo una lalamika. Wakala huyu wajibu wake ni nini kwenda pale, maana lazima tutizame ukweli wajibu wake ni nini maana hana nafasi ya kusema chochote anakwenda kukiangalia nini na ripoti yake anampekea nani.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea kusimamia hoja yangu na kwenye hii Mhe. Mwenyekiti mimi bora niwe mmoja, lakini kwasababu mzalendo wa nchi hii nitapigisha kura, haki yangu unipe. Naomba majibu ya ziada kwenye hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, anayosema Mhe. Miraji Khamis Mussa nimeyasikia, lakini kama nilivyosema uchaguzi una mchakato na mwazo wake ni uandikishaji. Kama ile haki ya wakala anayokuwepo kwenye kupiga kura, ndio haki hiyo hiyo ya wakala anayokuwepo katika uandikishaji. Madhumuni yake ni yale yale na asiyekuwa na chama yeye vile vile wapo wakala wa vyama wakati wa kupiga kura.

Kwahivyo, haimzuii asiyekuwa na chama asiweze kuandikisha, lakini hawa wenye vyama vyao wanaona wakati mwengine hakuna uadilifu katika uandikishaji. Ile kuhakikisha kila kitu kimekwenda sawa, hakuna maneno kila mmoja ameridhika nchi kuibakisha katika hali ya utulivu lazima mawaka wawepo, huo ndio msingi wake. Vyenginevyo tungelichukua lile daftari tukaliandika tu lakini chama kinataka kujiridhisha watu wetu hawa wanayo haki wanakuwepo pale. Hivyo, ukasema tuandikishe bila ya wakala Mhe. Mwenyekiti ni tatizo, tunaweza kuanzisha tatizo kubwa katika nchi bila ya sababu. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, leo ndio napata taswira ya kutunga sheria inayosimamiwa bila ya wazalendo wa nchi hii, ndio nataka kuwaona mmoja baada ya mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii hii inasema huku mwisho kifungu hicho hicho cha 15 mwisho kabisa, kinasema isipokuwa kwamba kutokuwepo kwa wakala wa uandikishaji katika kituo hakutasimamisha kazi ya uandishaji. Dhahiri maana yake hawa waliotuletea mswada huu wanatupa picha kama huyu mtu hakuwa wa lazima, wanaendelea tu ndio hilo nasema wanatuletea mswada lakini huku huku wanakwenda ku-*compromise*.

Haiwezekani kupunguza *resource* za nchi hii, hawa ukawa ule mlo tu wa siku wawe kila kituo tu kwa mujibu wa taratibu tuliotoka nao watu wawili, vituo vya nchi hii tumepoteza hela kubwa sana ya walipa kodi wa nchi hii. Mhe. Mwenyekiti, hakuna maana lakini pia naomba unisikilize kwa sababu unisimamie hoja yangu, tunatoa wiki moja ya watu kulalamika, wakati huyu wakala alikuwepo. Hiyo wiki moja tunaitoa ya nini na wakala

wako wewe alikuwepo kwenye daftari, maana vitu vyote ukivichanganya huoni maana na waziri iwe kanijibu mimi awe anawatendea haki wananchi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kifungu hiki kiondoke na hiyo ndio mara yangu ya pili bado mara yangu ya tatu kama hakunijibu tupigishe kura.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, *point* yako hasa unajua unazunguka sana, *point* yako vipi abaki sheha tu kwamba ndio anatosha au vipi?

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, *point* yangu niliisema mwanzo wakala wa serikali siwezi kumuondoa sheha. Wakala wa vyama vya siasa namuondoa kwasababu hii haki ya Katiba maana yeye alinukuu Katiba. Katiba inampa haki mwananchi wa nchi hii, haimpi haki mwanachama wa chama cha siasa. Kwanini leo tutunge sheria ikisha yeye akasimamiwe na chama cha siasa katika kuangaliwa. Hiyo ndio hoja yangu, mimi sina tatizo siku ya kupiga kura kwa sababu kuna mgombea wako Miraji kagombea kamsimamie haki yake.

Lakini hapa ninapozungumza mimi hapana uwakala wa chama cha siasa kwasababu haendi kupigiwa kura mtu, tunaenda kumuingiza mtu kwenye daftari, ndio hoja yangu. Sasa mimi sheha nambakisha kuwa ni wakala wa kubaki, lakini wakala wa chama cha siasa mimi namuondoa…

Mhe. Mwenyekiti: Ushafahamika Mhe. Mjumbe, naomba ukae …

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ikifika pahala serikali haitaki tupige kura, ndio faida ya *backbencher*…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba ukae. Mhe. Waziri tafadhali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kiwango cha uzalendo hakipimwi kwa maneno, kiwango cha uzalendo katika nchi hii ni wananchi wa nchi hii watatupima sote kwa kitendo cha kila mmoja wapo. Kwahivyo, suala la kudharauliana kwenye uzalendo pengine mimi nina uzalendo mkubwa kuliko yeye sio tuelewane. *(Makofi)*

Lakini la msingi hapa tuna hoja ya kubakisha suala ambalo tutajenga misingi ya utulivu wa nchi na amani ya nchi, na halazimishwi chama cha siasa kuleta wakala, kama hataki ndio hataki lakini utaratibu wa kuweka wakala ni *best practice* na pia ni suala ambalo litakuwa linatuliza nchi wakati huo wa uandikishaji.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakubaliana kabisa tupige kura wajumbe wengi waamue. *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mara yangu ya tatu, mimi sitaki kuishi kuishi kwa *best practice* katika kutunga sheria, naam Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nataka nipigishe kura…

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Nilikuwa nasema sitaki kuishi na *best practice* ambayo yeye mwenyewe ukimuuliza na uzalendo aliosema wa nchi hii haujui umeanzia nchi gani…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kwenye suala la uzalendo tusiende huko, naomba…

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Aaa! Kwenye uzalendo mimi nimeacha, nakuja na *best practice* aliyoisema alau angesema tu Kenya wanatumia, Uganda wanatumia ndio *best practice,* maana tunazungumza nchi na zinavyotunga sheria. Kwa hivyo, kwenye *best practice* mimi naondoka kabisa, ninachosimamia kuwa hili zoezi ni zoezi la serikali, sheha sina tatizo naye kuwaingiza vyama vya siasa maana yake ni kutuingizia kwenye majaribu ya hatua ya awali.

Nataka sote tuwe *free* kama mimi natoka CCM nitakuwa *free*, kama mwenzangu anatoka TADEA atakuwa *free* watu waende tu na hatujadili wanachama wa chama cha siasa. Tunajadili wananchi waliozungumzwa kwenye Katiba kifungu cha 7(1) na ndio ninao watetea, tusiwaekee watu wakenda kuwapinga ambao hawana msingi wa kisheria ya kuwapinga tusiwaingize humo. Hoja yangu ni hiyo kifungu kiondoshwe kama mwenzangu hataki tuende kupiga kura.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba tukipigie kura lakini kabla ya hapo ningewaomba wale wataalamu wa Mhe. Waziri wateremke huku chini, ili waweze kumpa msaada wa karibu ikitokezea kama kuna tatizo, shukeni hapa chini tu.

UPIGAJI WA KURA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, twendeni kwenye kura waheshimiwa nitahoji wale wote ambao wanaunga mkono serikali kwamba kifungu hiki kibaki kama kilivyo wanyanyue mikono. Waheshimiwa inaonekana hamjafahamu nitasema tena. Serikali inataka kibaki kama kilivyo, Mhe. Miraji Khamis Mussa yeye anasema kitoke. Mimi ninachohoji wale wote ambao wanaunga mkono serikali kukibakisha kama kilivyo wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe)*

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tunaomba hesabu

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, upigaji kura kidogo naona wengine hawakuwa na msimamo, kwa hiyo naomba bora tusimamishe mmoja mmoja apige kura. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Sawa, Waheshimiwa unajua kuna baadhi ya watu hawakupiga kabisa hii kura yaani, serikali iliponyanyua mikono baadhi ya watu walibaki hawakunyanyua tuliposema wale wanaokataa, yaani hawakukubali wala kukataa. Sisi tulihesabu kura tu zile ambazo…

Waheshimiwa Wajumbe, naomba tuendelee, naomba tuendelee, Waheshimiwa naomba tuendelee kwasababu kuna watu wengine ndio kwanza wameingia sasa hivi wao walikuwa hawamo hatuwezi kuipiga tena hii kura. Tunaendelea. (*Makofi*)

Sehemu ya Pili

Uandikishaji wa Wapiga Kura

Kifungu 11-24 Pamoja na Marekebisho yake

Sehemu ya Tatu

Ukaguzi wa Daftari

Kifungu 25-28 Pamoja na Marekebisho yake

Sehemu ya Nne

Uendelezaji wa Daftari

Kifungu 29-33 Pamoja na Marekebisho yake

SURA YA TATU

Sehemu ya Kwanza

Uchaguzi Mkuu

Kifungu 34-41

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kusimamia vizuri upigaji wa kura. Lakini, hoja yangu Mhe. Mwenyekiti katika sehemu hii ya tatu nilikuwa nina maeneo kama matatu ambayo yote nimekusudia kuyapigia buti kama nilivyoeleza mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, nilivyokuwa naelezea au katika mchango wangu kifungu cha 34. Kwanza nashukuru kwa maelezo ya Mhe. Waziri lakini pia naomba avumilie kwa *disturbance* ambayo iliyotokezea kwa namna tulivyokuwa tukizungumzia hapa Barazani. Kwakweli, tunampa pole lakini nitaomba Mhe. Mwenyekiti kwenye *hansard* tuje tumuombe mwenzetu arekebisho kidogo ile lugha yake, maana yake uzalendo hauna

kipimo. Kwahiyo, hili tutakuomba Mhe. Mwenyekiti baadae tuje tumuombe mwenzetu aeke sawa *hansard* yake ili kumbukumbu ziende vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye hoja yangu ya kifungu cha 34 kuhusu suala la uchaguzi mkuu. Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa masharti ya Katiba kutakuwa na Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar ambao utafanyika kila baada ya miaka mitano.

Mhe. Mwenyekiti, nilieleza *concern* yangu najua kwamba Katiba ndio sheria mama na Katiba yetu inaeleza kutafanyika uchaguzi kila baada ya miaka mitano. Lakini bado tunaendelea kusisitiza kwasababu Mhe. Waziri alivyokuwa akieleza kuna hoja zetu nyingi alikuwa aki-*quote* Katiba, kwamba Katiba inazuia, Katiba hairuhusu. Kwahiyo, nadhani kupitia maneno yake mwenyewe Mhe. Waziri sasa hivi iko haja serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kama Katiba inavyosema kwamba aidha Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi anayo haki ya kuleta kufanya marekebisho ya Katiba au serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani bado naendelea kusimamia ule msimamo wangu kwamba tunajua kwenye sheria huwezi ukaingiza, lakini lazima tufanye marekebisho ya Katiba, tuangalie sasa je ni miaka mingapi ambayo baada ya kupita katika demokrasia na kuangalia umuhimu wa maendeleo na matumizi mazuri ya *resource* za serikali. Miaka saba nadhani ni wakati muafaka kwa kufanya uchaguzi kila baada ya miaka mitano. Sasa hoja yangu hii nilikuwa naomba Mhe. Waziri atakaposiamama kunijibu anieleze je serikali wako tayari kufanya marekebisho ya Katiba au kama hawajakuwa tayari, basi sisi wenyewe ambao tuko tayari tuweze kuleta marekebisho ya Katiba ili yaendane vizuri na sheria ambazo tunazozitunga. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwa kuwa hatuendi kwa vifungu tunaenda kwa sura, nilikuwa naomba mwongozo wako aidha vile vifungu vyengine niende navyo kabisa au nisubiri baadae kidogo. Lakini kama itakuwa niende kifungu kimoja kimoja naomba nipate ufafanuzi wa kifungu hiki, halafu baadaye niendelee na vifungu vyengine viwili. Kama tulivyosema kuwa tunaenda kwa sura na sura ina vifungu vingi nadhani nije nipate tena haki ya…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nitakuruhusu tena kwasababu sitaki kumchanganya waziri nataka tumpe kitu kimoja kimoja aweze kujibu halafu nitakupa tena nafasi nyengine.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sawa ahsante, basi naomba ufafanuzi kwa hilo. Mhe. Mwanasheria Mkuu pia akusaidie hapo kama kuna chochote.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwasababu kwenye sehemu hii kama nilivyosema lile la miaka linahusu mambo ya Katiba na hapa kwenye sehemu yote hii vifungu vya sheria ambavyo hatuwezi kukiuka utaratibu wa Katiba. Kwahiyo, inakuwa vigumu…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri nadhani hayo anayaelewa isipokuwa alikuwa anachotaka yeye lini au mko tayari serikali kuleta mabadiliko ya Katiba au mtawaruhusu wajumbe walete wao binafsi waweze kuvirekebisha hivyo vifungu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hili jambo linahitaji ushauri kwa sababu suala la Katiba hii mheshimiwa na namna ya kuendesha mfumo mzima wa uendeshaji wa nchi, kwasababu hapa tunafanya pamoja na wenzetu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni mambo ambayo yanahitaji mashauriano na tunakubaliana ni utaratibu gani mzuri tuufanye, tunabadilisha nini katika Jamhuri yetu ya Muungano. Kwahivyo, suala la Katiba ni suala tabu mimi kulitolea maamuzi moja kwa moja, lakini kwangu ni kuupokea ushauri na nitauwasilisha serikalini na namna itakavyoonekana inafaa ndio tutapewa maelekezo, naweza kusema hivyo tu mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu atusaidie, kwa sababu tuna chaguzi mbili tofauti na hata Tume za Uchaguzi tuna tume mbili tofauti. Tuna Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (*NEC*) na tuna Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (*ZEC*). Kwahiyo, bado Katiba ya Jamhuri ya Muungano haitufungi kufanya marekebisho ya Katiba kwa yale mambo ambayo tunahisi yana maslahi ya Zanzibar kwa kuona kwamba lazima iende sambamba na marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Hivyo, bado naendelea na msisitizo wangu Mhe. Mwanasheria Mkuu tuambie kwasababu kama nilivyosema vifungu vya sheria hivi vingi vinatubana kwenye katiba, maana sheria hapa huwezi ukatia mkono wakati Katiba tayari imebana, ndio maana nikauliza je, serikali iko tayari kufanya marekebisho ya katiba, ili sheria zetu nyingi tunazozipitisha ziende sambamba? Au sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tujiandae kufanya marekebisho ya katiba tuyalete ili tuweze kuyajadili kwa maslahi ya Zanzibar?

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, *of course* kama alivyosema Mhe. Waziri hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma inajadilika na hoja hiyo inakwenda sambamba na kifungu cha 28(4), ambacho ndio kimeweka muda wa urais. Lakini pia inakwenda na kifungu cha 92 cha katiba ambacho pia kimeweka muda wa maisha ya Baraza la Wawakilishi ambayo ni miaka mitano. Kwahiyo, sio muda wa uchaguzi wa urais peke yake tu, lakini pia hata muda wa uchaguzi wa Baraza la Wawakilishi nayo ni miaka mitano.

Sasa tunapozungumza hoja hizi tujue tunazungumza hoja zote mbili. Hoja yake inazungumzika kama alivyosema Mhe. Waziri na hii katiba sio ya serikali, katiba ni ya Zanzibar maana yake ni yetu sote, ina maslahi ya Wazanzibari wote. Kwahiyo, fatwa ya kusema tunachukua na tutarekebisha hayo sio maamuzi ambayo tutayatoa leo. Lakini namwambia Mhe. Hamza Hassan Juma hoja yake inazungumzika utaratibu upi utafanywa hayo ni mambo ambayo yataamuliwa hapo baadaye, ama na serikali ama na Baraza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, sitaki twende kwenye kupiga kura, lakini namalizia kwa kumshauri sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. Sasa hivi nadhani sote tunajua kwamba serikali zetu zote mbili zinafanya jitihada za kubana matumizi, lakini vile vile kufanya matumizi mazuri ya serikali kwa kuleta maendeleo ya wananchi.

Nafikiri hoja yangu ukiangalia kiuchumi ina tija kubwa sana, kwa sababu kama ninavyosema chaguzi kila baada ya miaka mitano tunatumia fedha nyingi sana, lakini pia tunakaribisha ugomvi mwingi sana. Sasa mimi nadhani kama alivyosema linazungumzika basi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanasheia Mkuu aturuhusu sasa tuanze mjadala wa ndani nje ya Baraza katika vikao vyetu vya ndani kuangalia ni maeneo gani ya Katiba yetu ya Zanzibar tuweze kuyafanyia marekebisho ili kuleta maslahi kwa wananchi wa Zanzibar. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, sasa Mhe. Hamza Hassan Juma unyanyuke, kwa ajili ya vile vyengine ulivyosema kinachofuata hicho kimepita.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, katika hoja yangu nyengine ambayo nilizungumzia ilikuwa kifungu cha 43. Kifungu hiki kama nilivyosema Mhe. Waziri namshukuru sana alitoa ufafanuzi mzuri sana kinazungumzia sifa za mgombea urais. Niliendelea kusisitiza kwamba bado Katiba yetu ya Zanzibar inambana kijana kuchukua nafasi ya uraisi wa Zanzibar, yaani katiba yetu inasema umri wa kuchukua uraisi anatakiwa awe miaka 40. Lakini sasa hivi tuna vijana wamesoma, weledi...

Mhe. Mwenyekiti: Hicho ni kifungu cha 43 Mheshimiwa?

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ndio, sifa za kugombea uraisi.

Mhe. Mwenyekiti: Hatujafika huko mwisho 41 hii tunayohoji.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mimi nilifikiri tunakwenda kwa sura kumbe kwa sehemu. Kwa sababu sura bado ni sura ya...

Mhe. Mwenyekiti: Kwa sehemu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Aah, *okay* ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Basi naomba nihoji kwa hiyo sehemu, ngoja isomwe tena hapa.

Sehemu ya Kwanza

Uchaguzi Mkuu

Kifungu 34 - 41

Mhe. Hamza Hassan Juma: Samahani Mhe. Mwenyekiti, bado kuna hoja nyengine katika sehemu hii, katika sura hii kifungu cha 41. Kifungu hiki Mheshimiwa nilielezea kuhusu kwamba kuongezwa kifungu kidogo cha (4), hapa kimeeleza uchaguzi wa marudio, zimeelezwa hapa kwamba pale ambapo tume itaridhika kabla ya kutangaza matokeo ya uchaguzi kwamba kulikuwa na kutofuatwa kwa taratibu za matumizi mabaya na ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi, au kifungu kidogo cha (2) kinaeleza pale ambapo kura za wagombea zimefungana. Sasa kuna kifungu kimoja ambacho mimi nimependekeza kiongezwe kwamba "uchaguzi utarudiwa iwapo itabainika kwamba kulifanyika vitendo vya ubadhirifu" yaani, nimekusudia suala zima la rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ukiangalia moja katika matumizi mabaya au ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi suala la rushwa limo. Sasa hapa ingawa Mhe. Waziri aliniambia kwamba ziko sheria nyengine ambazo zinazungumzia masuala ya rushwa na mtu akipatikana atakwenda Mahakamani. Lakini je, kama mfano akienda Mahakamani na tunajua kwamba kesi ya rushwa inaanzia miezi sita na kuendelea, wakati mtu mwenye sifa ya kugombea akifungwa kwa muda wa miezi sita ina maana tayari anakuwa *disqualified,* hawezikuwa Mbunge au hapa tunazungumzia uwakilishi hawezi kuwa Mwakilishi au Diwani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa nadhani kifungu hiki cha (4) kinaingia, kwasababu kama alivyosema Mhe. Waziri sheria inasema kwamba mtu akikamatwa na rushwa Mahakama ikimthibitisha atafungwa kifungo kinachoanzia miezi sita, ina maana kama kuanzia miezi sita ameshakuwa *disqualified* kuwa mwakilishi. Sasa kwa nini kifungu hiki kishindwe kuingia hapa?

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimefahamu hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma, ukikisoma kifungu namna ambavyo kimeandikwa *of course* moja ya maeneo ambayo tume itazingatia ni maeneo haya ambayo yanatokea wakati wa uchaguzi ikiwemo ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi, rushwa. Kifungu cha 130 ndio kimeeleza karibu kifungu kizima namna gani rushwa inakatazwa ndani ya sheria hii. Sasa mimi nadhani Mhe. Mjumbe kama ana hoja kwenye adhabu labda tukifika kwenye kifungu cha 130 ndio aombe yeye hoja yake ya adhabu.

Lakini kwa namna kilivyo hapa, nadhani maeneo yote ambayo ya ukiukwaji wa taratibu yakibainika maana yake tume imepewa uwezo wa ama kuakhirisha au kusitisha huo uchaguzi. Sasa kama hoja yake ni kwenye adhabu basi tusubiri kifungu cha 130 tutapojadili ile adhabu, ile hoja yake atasema kama adhabu izidishwe au ipunguzwe iwe ndogo zaidi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia *marginal note* inazungumzia uchaguzi wa marudio. Kwahiyo, ina maana tume ikija ikigundua kwamba mtu ameshinda uchaguzi lakini alitumia njia ya rushwa uchaguzi si utarudiwa, ina maana kama uchaguzi utarudiwa basi *marginal note* hapa ndio inavyosema. Kwa maana hiyo, hata mtu akipewa adhabu, adhabu yenyewe ina maana ni uchaguzi ule kufutwa na kurudiwa, sasa *marginal note* ndio inavyosema. *Marginal note* inasema uchaguzi wa marudio.

Mhe. Mwenyekiti, labda *terminology* za kisheria unajua mimi nilisoma *college* ya Kwamtipura lakini tafsiri ya kule kwetu naona kama ndio inazungumzia hivyo. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Na mimi nimeshakuelewa Mheshimiwa tumsikilize Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani hoja ya Mhe. Mjumbe anachosema ni kwamba kama huyu mtu amekamatwa na ametiwa hatiani hoja yake kama atakosa sifa wakati wa uchaguzi wa marudio.

Kwakweli, nasema moja ya eneo ambalo linamkosesha mtu sifa ya kuchaguliwa ni kutiwa hatiani kwa kosa la jinai. Sasa wakati haya yanatendeka na kama huyu mtu alikuwa ni mgombea na tume ikathibitisha na Mahakama kama ametiwa hatiani kwa kosa la rushwa, maana yake mtu huyu amekosa sifa za kuwa ni mgombea. Kwahiyo, kwenye ule uchaguzi wa marudio maana yake huyo tayari ameshakuwa ametiwa hatiani na hatakuwa ni sehemu ya uchaguzi ule wa marejeo, ndio hivyo ilivyo kisheria. Hatokuwa sehemu ya uchaguzi ule wa marejeo kwasababu atakuwa tayari ameshatiwa hatiani.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu nitachukua ushauri wake nitasubiri kule katika kifungu cha 130. Kwasababu bado hoja yangu lazima tusisitize suala zima la rushwa, tunalipiga vita katika sheria hii. Ahsante.

Sehemu ya Kwanza

Uchaguzi Mkuu

Kifungu 34 - 41

Sehemu ya Pili
Uteuzi wa Wagombea

Kifngu 42 - 61

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa tena hii nafasi, nazungumzia tena kifungu cha 43 na hoja yangu naendelea kusisitiza umuhimu wa kufanya marekebisho ya katiba kwa sababu kifungu hiki pia tunabanwa na Katiba ya Zanzibar. Nilizungumzia suala zima la umri, kwamba sheria inasema kuwa kifungu 43(b) ametimia umri wa miaka 40, yaani mtu anapaswa kugombea uraisi awe ametimia miaka 40. Lakini kama nilivyosema sasa hivi tumeshuhudia kuna vijana wadogo kuanzia miaka 35 wengine wanakuwa Wakurugenzi wanaendesha mashirika makubwa, lakini hata serikali inawapa dhamana kubwa na wanafanya vizuri.

Kwahivyo, bado katiba inatubana katika suala zima la umri na hoja yangu ilikuwa kwa kuwa katiba inabana huku chini, yaani kuanzia miaka 40 miaka 35 inabana. Lakini kwa kuwa katiba iko wazi haijazungumzia kikomo mimi nafikiri kwenye sheria hapa bado

nilikuwa napendekeza kwamba kuanzia miaka 40 lakini asizidi miaka 75. Sasa hii bado nilikuwa naendelea kuisisitiza kama nilivyosema kwa sababu lazima tuangalie matumizi mazima ya *resource*.

Vilevile, katika kifungu hiki nilipendekeza kwamba kiongezwe kifungu ambacho mgombea wa nafasi kubwa ya uraisi lazima ahakikishwe anapimwa afya na madaktari wathibitishe kuwa anaweza kushiriki katika harakati za kuongoza nchi kwa muda wa miaka mitano bila ya matatizo yoyote. Kama alivyosema Mhe. Waziri mtu unaweza kuwa kijana lakini ukaumwa, tunazungumzia suala zima la afya. Afya kuna *background*, tunajua mtu yeyote ambaye anapima afya anakuwa na *background*, kama madaktari watathibitisha kwamba huyu mtu afya yake itakuwa kila baada ya miezi sita kwenda kutibiwa nje ya nchi itakuwa ni matumizi mabaya ya fedha za serikali. Kwa hivyo kifungu hiki pia naomba kiongezwe suala zima la kupimwa afya.

Mhe. Mwenyekiti: Umeeleweka Mheshimiwa, Mhe. Mwanasheia Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Hamza Hassan Juma amefahamu sana hoja iliyokuwepo kwenye kifungu cha 43 ambayo inafanya rejea kwenye kifungu cha 26 cha katiba. Mhe. Waziri katika majumuisho yake amesema vizuri, kwamba sheria yoyote ambayo itakwenda kinyume na masharti yaliyomo kwenye katiba sheria hiyo itakuwa batili na itatenguka.

Masharti yaliyokuwemo katika katiba na katiba haikutoa fursa, wakati mwengine Mhe. Mwenyekiti katiba inatoa fursa, inasema au jambo jengine lolote kama litaidhinishwa na sheria itayotungwa na Baraza la Wawakilishi. Katiba hapa imejifunga imetaja sifa na ikamaliza haikutoa nafasi kwa sheria nyengine kueleza sifa nyengine zaidi ya ambazo tayari zimeshatajwa kwenye katiba. Hoja yake ibaki kwenye katiba kifungu cha 26 kama hapo nchi itapokuwa tayari kufanya marekebisho ya katiba basi moja ya eneo iwe ni kifungu cha 26, lakini kwa tulivyo hapa hatuwezi Mhe. Mwenyekiti, kutia mkono juu ya kupunguza au kuzidisha sifa ambazo hazijaelezwa ndani ya katiba. Nashukuru Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, nafikiri na yeye pia amenielewa. Kwahiyo, ndio tunaona hapa jinsi tunavyoipitisha hii sheria katika mazingira magumu kwa sababu tumebanwa au tumefungwa na katiba. Hivyo, bado nitaendelea kusisitiza mazungumzo yetu ya ndani yaendelee ili tuone haya maeneo ambayo katiba inatubana yaweze kufanyiwa marekebisho. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikupongeze sana kwa umahiri wako kwa kukiongoza hiki kikao vizuri na naamini tutafika pahala pazuri. Lakini la pili naomba sana niondoe neno langu lile la uzalendo kwa kulifuta na huo ndio uungwana, pale ambapo unakwenda *speed* basi unapunguza *speed* unaomba radhi wenzako. Lakini hoja yangu niliyosimama nayo nina vifungu viwili, 44 na 53.

Kifungu 53 ni kidogo tu, katika kunukuu. Huku waliandika nambari 67 lakini mapendekezo yangu mimi nikasema yawe 67(1) na ndio katiba tukiitizama ni 67(1) sio 67 peke yake, ili waiweke. Hoja yangu hapo ndogo tu, sasa sijui Mwanasheria Mkuu na Mhe. Waziri mzalendo mwenzangu watasemaje.

Kifungu 44 nilichangia kuonekana wagombea wa uwakilishi awe ni Mzanzibari wa kuzaliwa na nikatoa maelezo kidogo, kuwa hawa ni sehemu kubwa sana kuwa ni wasaidizi wa Mhe. Rais, mana tunazungumza hapa ndani yake mna mawaziri na Makamu wa Pili wa Rais. Sasa tutapotoa fursa pana kabisa ambayo tuweke Mzanzibari tu asiwe Mzanzibari wa kuzaliwa tunaweza kuwakosa sasa wale watu wenye uchungu na nchi hii wakatufikisha pahala si pazuri.

Sasa Mhe. Waziri akaja akasema napingana na katiba, akasoma katiba kifungu cha 6(1), kila nikikiangalia hakiendi sambamba na yale niliyoyataka mimi mana hakinizuii ndio jibu lake. Sasa akiangalie kifungu 6(1) alichonijibu na hoja yangu niliyoitoa ili twende sambamba. Mimi hoja yangu awe Mzanzibari wa kuzaliwa kifungu 44(a) badala ya Mzanzibari mtupu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu cha 44 kama kilivyoanza kusoma kifungu cha 43 kwa kuzingatia masharti ya katiba na masharti yenyewe ni kifungu cha 68 cha Katiba ambacho ndio kinatoa sifa za mtu kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Sifa ya kwanza awe ni Mzanzibari na Mzanzibari ametajwa kwenye sheria nambari 5 ya mwaka 1985 ni nani Mzanzibari. Sasa hayo ndio masharti ya katiba na ndio masharti ya Sheria Nam. 5 ya mwaka 1985 ya nani Mzanzibari. Katiba haikusema kwenye kifungu cha 68 awe ni Mzanzibari wa kuzaliwa na haya masharti ndio yamechukuliwa kwenye kifungu cha 68.

Sasa niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe, sana Mhe. Mwenyekiti, kwenye vifungu ambavyo tutapitia na kwenye vifungu ambavyo vinafanya rejea kwenye katiba majibu ya upande wetu yawe ni haya, kwamba hatuwezi kutia mikono kwenye katiba tukaitungia sheria masharti ambayo yanakwenda kinyume na masharti ya katiba. Niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe, hoja zao ni nzuri lakini hoja zao zinapingana na masharti yaliyomo kwenye katiba. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mwanasheria Mkuu, ndio tunaiona faida ya kuja humu, pale maeneo ambayo hata Waheshimiwa Mawaziri wanapotujibu tofauti pengine na yale pengine anakuja kuyaweka sawa. Kwasababu alitunukuu kifungu 6(1) na mimi nikaiweka katika *bracket* 6(1) inasemaje. Lakini sasa hivi alipolipeleka kifungu cha 68 nimekubaliana naye, lakini kwenye hili tunaendelea ila katika yale ambayo ameshauri Mhe. Hamza Hassan Juma ya kuyazungumza kwa undani kabisa ili tuyalete kwa utaratibu na hili liwemo.

Mhe. Mwenyekiti: Huko usiende Mhe. Mjumbe.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Maana hii nchi inakoelekea siko. Nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nina marekebisho madogo kuhusu hansard, nilisema 6(1) inatambua kuwepo kwa Mzanzibari, 68 nimesema. Kifungu cha katiba ndicho kinatoa sifa za Mwakilishi. Napenda *hansard* ikae sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante.

Kifngu 42 - 61

Sehemu ya Tatu

Kampeni za Uchaguzi

Kifungu 62 - 66

Sehemu ya Nne

Matayarisho ya Upigaji Kura

Kifungu 67 - 77

Sehemu ya Tano

Upigaji Kura

Kifungu 78 - 85

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, mimi niko kwenye kifungu cha 80 Utaratibu wa Kupiga Kura. Mhe. Mwenyekiti, kifungu 8(a) kimesema 'kila mpigakura aliyeandikishwa ambaye ana nia ya kupiga kura atakwenda yeye mwenyewe katika kituo na atatoa kitambulisho chake cha kupigia kura kwa msimamizi wa kituo. Jana katika kuchangia nilisema kwamba kuna baadhi ya wengine wakati wa kupiga kura huchukuwa mpaka vyeti vya bibi zao waliokufa enzi za kunde nyingi huenda wakapiga kura. Hasa hapa nilitaka nijuwe kwasababu haipo kwamba ikiwa kama huna kile kitambulisho upige tu. Kwanza nilitaka kujua je, wale wale utakuwaje.

Mhe. Mwenyekiti: Sijui kama umemuelewa Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Bado sijaelewa ungeeleza vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Kuna watu baada ya kuchukuwa vyeti vya kupigia kura vile vipande wa kupigia kura wanakwenda na vyeti vya wazee wao si ndio.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ndio, Mhe. Mwenyekiti, yaani vile vyeti vya bibi zao nakusudia mpaka leseni za gari na vitu vyengine hata jana nilizungumza hivyo. Sasa nilitaka njiue hapa kwamba ruhusa hiyo itakuwa ipo au haipo kwasababu si kuna wengine vitambulisho huviuza halafu wakenda wakafanya fujo kule. Sasa kama huna kitambulisho usipige kura nilitaka nijue hapo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, akifungua kifungu cha 24 cha sheria hii ataona taratibu naomba nikisome.

Kifungu 24(i) kinasema hivi:

> "Pale ambapo kitambulisho cha mpigakura kimepotea kimechafuka au kuharibika mpigakura anaweza kuomba yeye mwenyewe kwa Afisa Uandikishaji kupatiwa kitambulisho kipya cha kupiga kura".

Kwahiyo, lazima tutakwenda na kitambulisho chako cha kupiga kura huwezi kwenda na kitambulisho cha bibi yako ukawa wewe mpigakura. Mpigakura anapiga kura kwa kitambulisho chake na kitakachopotea utaratibu ni huu wa kupata kitambulisho chengine ili apige kura.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kidogo niko kwenye kufahamu kwasababu kwamba kimepotea sawa nadhani kama kimepotea leo mfano Jumatano lakini uchaguzi ni Jumatano inayofuata ana uwezo wa kwenda hapo. Lakini sasa uchaguzi kesho, kesho kutwa au kesho tuseme leo keshakiuza pesa keshakwenda kununulia changu. Sasa ile ndio hoja yangu atakipata vipi na wakati keshakiuza na uchaguzi ni kesho asubuhi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Hapo umepoteza haki yako ya kupiga kura kitambulisho huna kama unacho kionekane. Kwa hivyo, huwezi kutumi cha bibi wala cha babu una kitambulisho chako utapeleka utapiga kura. Utaratibu wa kuomba kupata kitambulisho kipya upo dakika wa mwisho ukipoteza utashukuru Mungu. *(Makofi0*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nafikiri tumeelewana Mhe. Suleiman Makame Ali sehemu hii imekubaliwa,.

Kifungu 78 - 85

Sehemu ya Sita

Kuhesabu Kura na Kutangaza Matokeo

Kifungu 86- 99

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 93 (4) Mhe. Mwenyekiti, kifungu hichi nilikilalamikia suala zima la kubandika matokeo ya uraisi katika katika jimbo. Mhe. Mwenyekiti, hapa kifungu kidogo cha nne naomba kunukuu.

Kifungu cha 93(4) kinasema hivi:

> "Fomu za matokeo kwa kila jimbo au wadi ya kila uchaguzi chini ya kifungu hiki utasimamia na msimamizi wa uchaguzi wakala au mgombea na zitabandikwa nje ya kituo cha majumuisho".

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la uwakilishi na udiwani sina tatizo matokeo kubandikwa kwenye kituo, kwasababu yale ndio matokeo ya mwisho na pale ina maana msimamizi wa kituo anatangaza matokeo ya diwani alieshinda na Mwakilishi alieshinda. Sasa hoja yangu utakapobadika na matokeo ya uraisi sasa pale ina maana yule Mkuu wa Kituo cha Jimbo atatangaza kwamba pale rais gani alieshinda au mgombea gani wa uraisi alieshinda.

Hoja yangu, kwamba katika majimbo matokeo yabandikwe ya wale ambao wanatangazwa walioshinda pamoja na kura zao. Sasa wale ambao mawakala wa raisi kwa kila chama waendelee kuchukuwa matokeo yao mkononi, ili Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi yeye ndie mwenye haki ya kutangaza matokeo ya urais. (*Makofi*)

Sasa leo Mhe. Mwenyekiti, tutakapobandika matokeo katika majimbo ndio pale kila mmoja atakwenda na *WhatsApp* yake, kila mmoja atafanya hesabu zake matokezeo yake tutasababisha hiyo vurugu ya watu kufanya majumuisho kutangaza matokeo ya urais wakati hakuna haki hiyo. Sasa hoja yangu ni hiyo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe, umeeleweka. Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, pale huwa hatangazi matokeo ya uraisi. Lakini kweli wanabandika hesabu za matokeo na kama nilivyosema awali kwamba sisi tumeona utaratibu wa kubandika ni mzuri. Lakini kama Baraza lako tukufu litaona tubadili kwa kura za rais tusibadike matokeo pale yanapotokea kwa kura za urais tusibandike matoke pale lakini watakuwa na ile fomu ambayo....

Mhe. Mwenyekiti: Kwahiyo, serikali imeshalikubali hili au vipi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Hatuna pingamizi nalo.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante tunaendelea. Maana yake wamekubali kulibadilisha Mhe. Waziri.

Kifungu 86- 99 Pamoja na marekebisho yake.

SURA YA NANE

Sehemu ya kwanza

Uangalizi wa Uchaguzi

Kifungu 100- 105 Pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Pili

Elimu ya Wapigakura

Kifungu 106- 108 Pamoja na marekebisho yake

SURA YA TANO

Utatuzi wa Migogoro na Malalamiko ya Uchaguzi

Kifungu 109- 117

SURA YA SITA

Makosa

Kifungu 118-132

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi sina makubwa sana lakini nina ushauri tu nilitoa katika kuchangia kwangu nilisema tu katika utangazaji wa matokeo kinyume na sheria.

Mhe. Mwenyekiti, katika nchi nyingi duniani hapa ndio kwenye mgogoro unaosababishwa kwamba Mungu atuepushe mbali hata maafa yakifikia....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kifungu gani unachozungumzia.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 127 ukurasa wa 208. Madhumuni yangu nimesema kwamba, kifungu hichi kina mambo matatu, naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 127 kinasema hivi:

i. "Ni marufuku kwa mgombea wa chama cha siasa taasisi mtu mwengine yoyote kutanganza matokeo ya uchaguzi kwa njia yoyote ya mawasiliano kabla ya kutangazwa na tume rasmi.

ii. Mgombea wa chama cha siasa, taasisi au mtu mwengine yeyote atakayetangaza matokeo ya uchaguzi au kuitaka tume kutangaza matokeo kabla ya kuisha kwa muda wa kutangaza, matokeo yaliyopangwa atakuwa ametenda kosa na .....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nenda kwenye hoja yako moja kwa moja.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Hoja yangu katika vifungu a, b,c,d naongeza d maana a, kinasema kwamba mgombea anatumikia kifungo cha muda usiopungua miaka 5 na faini isiyopungua milioni hamsini sina tatizo. Ikiwa chama cha siasa taasisi adhabu isiyopungua milioni mia moja sina tatizo. Lakini c nasema tu ikiwa mtu mwengine atatumikia kifungo kisichopungua miezi 18 sina tatizo lakini iongezwe.

Mhe. Mwenyekiti, nyongeza yangu ya hapa nimesema tu iongezwe kifungu cha (d), mgombea huyu asigombee maisha yake katika nchi hii. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Suleiman Ali ametupa ushauri mzuri kwasababu zote hizo ni adhabu na namna ya kukataza watu wasifanye makosa. Kwahivyo, kama Baraza litaona kwamba mgombea asigombee ni vizuri lakini ni vizuri akatupa muda tuweze kushauriana vizuri. Ni hoja nzuri atuachie hili jambo kwasababu inakuwa kugumu kulifikia maamuzi lakini linaongeza uzito kukataza watu kufanya makosa. Hivyo, anachokisema kina msimamo upande mmoja na upande mwengine itabidi tufate ushauri wa kisheria kama inayumkinika tutaweza kufanya hivyo. Sijui Mwanasheria Mkuu unasemaje.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsnate Mhe. Mwanasheria Mkuu, nyongeza kwenye hilo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mwenyekiti, mimi sina nia ya kugombea. Kwahiyo, sijui nikijibu vipi. *(Kicheko)*

Ah! Mhe. Mwenyekiti, nadhani ile mantiki iliyokusudiwa kisheria imepatikana kwenye kifungu cha 127. Kwasababu adhabu tayari imeshatoka kwa wale wote ambao watakuwa wamekwenda kunyume na kifungu cha 127 iwe mgombea iwe chama chake iwe taasisi nyengine yoyote. Mhe. Mwenyekiti, nadhani adhabu hizi nimuombe sana Mhe. Ali Suleiman Ali atukubalie hivi zilivyo na tuendelee.

Lakini pili kuna marekebisho ambayo pia yamefanywa na Mhe. Simai Mohamed Said na Mhe. Hassan Khamis Hafidh ya kuongeza kifungu (iii) ambayo pia serikali imekubali. Kwahiyo, nafikiri hivi ilivyo Mhe. Mwenyekiti, ni bora ziadi kuliko ilivyokuwepo hapo awali. Nimuombe sana Mhe. Mjumbe atuachie na tuendelee nacho.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo. Lakini ili kulinda usalama na amani katika nchi yetu tuondoe hicho asigombee maisha yake baadaye agombee iwe kipindi cha miaka 10 asigombee katika nchi hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ameondoa maisha ameweka miaka 10 Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wangu mimi sina tatizo serikali ndio inayoweka utaratibu ambao utatoa adhabu watu wasifanye makosa ni jambo jema. Kwahiyo, sawa tunakubaliana naye.

Mhe. Mwenyekiti: Mnakubaliana nae siyo?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ndio tunakubaliana nae. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Haya Mhe. Hamza Hassan Juma nilikwita au Mhe. Hassan Khamis Hafidh au siyo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma hukunyanyuka.

TAARIFA

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilisema nitasimama kwenye kifungu cha 130 kwenye suala la rushwa. Sasa nilifikiri labda utakumbuka lakini ndio nakukumbusha.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsnate sana Mhe. Mwenyekiti, ingawaje Mhe. Mwanasheria Mkuu kasema hichi kifungu cha 127 ambacho kina kitoto (i) na (ii) amekubali kuongeza kifungu (iii) kama tulivyo *propose*. Tungemuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu au Mhe. Waziri akisema basi ili tukisikie nini kimeongezwa. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nilikitamka pale kwamba nilikuwa nasema:

> "Tume au mtu mwengine yoyote atakaeona masharti ya kifungu cha (i) na (ii) kimevunjwa basi mtu huyo atakwenda kutoa taarifa katika kituo cha polisi, ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa". Ndio nilivyosema pale mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti: Ndio nakumbuka Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwasababu kimekubaliwa nafikiri unaweza ukaa baadae na Mhe. Waziri mkaweka sawa. Kwasababu kakubali kwamba atakurekebishieni.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee nawaamini wote ni wazalengo, wote ni wana Mapinduzi.

Mhe. Miraji Khamis Musssa: Mhe. Mwenyekiti, niungane na Mhe. Hassan Khamis lakini na mimi katika kifungu cha 127(c) ikiwa mtu mwengine atatukimikia kifungo kisichopungua miezi 18.

Sasa hapa katika kuchangia nilisema miezi 18, maana yake hapa ni mwaka mmoja na nusu. Tunazungumzia suala zito la uchaguzi wa nchi hii na *tension* na ile siku ya uchaguzi na kutangaza matokeo. Mtu mwengine huyu maana yake kama si taasisi au

kama si chama cha siasa, mtu mwengine atakwenda kufanya hivi ni muda mdogo sana, nikapendekeza angalau basi iwe miaka 5.

Maana hii adhabu sawa sawa na mtu alieiba kuku tunakuja kwenye uchaguzi. Kwenye hili hebu jamani viongozi wenzangu tuongeze uadilifu maana uadilifu tunao. Mimi nilikuwa hoja yangu hiyo tu ni kuongeza miezi 18 itoke kifungo kisichopungua miaka 5. Lakini na huyo mtu mwengine yoyote na yeye alipe faini na nikaisema mimi milioni 15.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, mambo mengi hapa tulipa ushauri wa wanasheria na wataalamu ndio tunafikia maamuzi haya na huyo mtu mwengine yeyote anatumikia kifungo kisichopungua miezi 18. Sasa Mhe. Miraji Khamis Mussa anataka tumuongezee miaka 5. Sasa mimi sina utaalamu wa kisheria kuwa mtu wa namna hii labda tusikilize ushauri wa kisheria.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya kifungu cha 127 tunakwenda na ukweli wa uzito wa jambo lenyewe na uzito wa kwanza unatoka kwa yule ambaye ni mgombea na ndio maana adhabu kubwa imewekwa kwake. Lakini uzito wapili unatoka kwenye chama cheke ambacho anatoka na adhabu kubwa nayo ikwekwa.

Vilevile, ya tatu kwenye taasisi nyengine yoyote iwe chombo cha habari au taasisi nyengine yoyote nayo pia adhabu kubwa nayo iwekwa. Kwasababu hayo ni maeneo ambayo ndiyo yanabeba uzito mkubwa katika jambo hili.

Lakini kuna na wengine hawa wanaopenda kufanya fanya haya mambo ambao *magnitude* yake sio kubwa kama wale wawili na watatu ambao wametangulia, ndio maana na huyu akawekewa na yeye adhabu na adhabu ya miezi 18 sisi kwa upande wetu tumeona inatosha ya miezi 18. Miaka 5 ni sawa sawa kuweka adhabu ya mgombea na ambao uzito wake haulingani.

Sasa ushauri wangu Baraza litaamua, ushauri wangu mimi ni miezi 18 ambayo ipo nadhani inatosha. Lakini, kama Baraza linaona haifai basi Baraza liamue kwa namna ambavyo litakavyoona linafaa Baraza ndio haki ya kutunga hiyo sheria.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu, lakini kwenye hivi vyama hivi huwa kuna wasemaji huwa kuna makatibu waenezi. Sasa katika mazingira haya huyu mtu mwengine yoyote maana taasisi ikisema huko unapata tafsiri tafauti na ndio maana nikasema pia pana ukubwa wake.

Sasa kama ile miaka 5 aliyoisema Mhe. Mwanasheria Mkuu tutakuwa tumemshabihisha na mgombea mwenyewe basi huyu tumpe nusu yake. Maana alau yawe makosa yawe yanalingana mie sina tatizo tumpe nusu yake miaka miwili na nusu. Lakini na hyo milioni 15 pia tuiondoe. Basi tuiweke hata milioni kumi kwa sababu huku tumempa hamsini kwasababu huyu mtu mwengine yoyote katika eneo hili lazima tumpe adhabu alau inayolingane.

Mhe.Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ushafahamika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Lakini pia nafidia atoe asiinde aka- *provoke* tu baadaye iwe *free* kila kitu hakuna adhabu itakayomkamata.

Mhe.Mwenyekiti: Miaka miwili na nusu Mhe. Waziri mwenyewe.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Nakubaliana naye Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tena kunipa nafasi hii kama tulivyokubaliana na Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba suala la rushwa nisubiri kwenye kifungu chake maalum.

Sasa nimeangalia kifungu chote cha 1130 katika suala zima la rushwa halikuzungumzwa kumuhusu mgombea wa uchaguzi, imezungumziwa zaidi mtu ambaye anafanya ushawishi wa kuteuliwa yeye mwenyewe au kuajiriwa au kwenye karatasi za kura au kitambulisho haijamgusa moja kwa moja kama mgombea.

Kwahiyo, bado naendelea kupendekeza kwamba katika suala zima la rushwa kwamba iwapo itathibitika na mahakama kwamba mgombea alishinda kwa kupitia rushwa, basi uongozi wake au uwakilishi wake au udiwani wake ufutwe na turudi katika uchaguzi wa marudio. Kwakeli, kifungu hichi kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti, kimeelezea tu kwa watu wengine hakikimgusa moja kwa moja mgombea. Nafikiri sheria zetu sasa hivi kila moja tu katika suala zima la rushwa tuweke sheria au tuweke kifungu ambacho kitakachombana mtu.

Sasa napendekeza baada ya kifungu cha 30(i) na hizi a,b,c mpaka 5 tuongeze iwe kifungu cha 130 (ii) ambacho kitambana moja kwa moja mgombea katika hiyo nafasi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mheshimiwa hoja ya rushwa nchi yetu inaipiga vita sana na serikali zetu zote mbili hazipendelei kuona rushwa na hususan katika uchaguzi. Kwahiyo, nataka nikubaliane na Mhe. Hamza Hassan Juma, kwamba katika kifungu cha 130(5) kitakacho weka vizuri maelezo yake hayo na Mhe. Mwanasheria Mkuu ata-*draft* kitu kinachoweza kuoana kiendane na hiyo adhabu ameionesha. Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kwa mara nyengine tena ya kuchangia mswada huu muhimu. Mhe. Mwenyekiti, ni utaratibu wa baadhi ya vyama vya siasa hasa vya upinzani hasa katika nchi za Kiafrika, baada ya kuona kwamba zinakwenda katika ushindani wa uchaguzi vinashindwa kuunda mbinu na taratibu mbalimbali za kuzuia watu wasende kupiga kura. Mhe. Mwenyekiti, taratibu hizo zimetumika sana hapa visiwani, kama vile wanapiga mabomu, baruti ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, uko kwenye kifungu gani.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, niko kwenye kifungu 131.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, endelea.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, watu wanaweza kupiga mabomu watu, wanawanyang'anya vitambulisho vya kupiga kura, wanawapiga makofi yaani, kila uhalifu wanaufanya, ilimradi kuhakikisha mtu hendi kutumia haki yake ya kupiga kura. Mhe. Mwenyekiti, kama mimi ningeulizwa ningesema basi mtu yeyote anayemzuia mtu kwenda kupiga kura bora iwe kosa la jinai, lakini *ok* tusiipeleke kwenye kosa la jinai. Kwakweli, hili ni kosa kubwa kunizuia nisende kutumia haki yangu ya kumchagua kiongozi ninayemtaka, ambaye ataweza kuniongoza kwa miaka mitano ni kosa kubwa sana, kwasababu sijui niliyemtaka mwenyewe, wewe humtaki na atakayekuja nani ambaye mimi simtaki pengine.

Mhe. Mwenyekiti, kulingana na adhabu iliyowekwa haitoshi kifungu 131. Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

Kifungu 131 kinasema hivi:

"... faini isiyozidi shilingi milioni tano na isiyopungua shilingi laki tano au atatumikia kifungo cha kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote yaani, faini na kifungo".

Mhe. Mwenyekiti, hichi hakitoshi kwasababu haki ya kupiga kura ni haki kubwa kwa raia. Kutokana na hali hiyo, naomba kusema kwamba, mtu huyu kwa vile amewazuia watu na hizi ni taratibu ambazo zinafanyika katika nchi hii pamoja na nchi nyingi zinazoendelea. Kwahivyo, naomba kusema Mhe. Mwenyekiti kwamba hapa tubadilishe na tuseme hivi, "mtu huyo atatumikia kifungo kisichopungua miaka mitano na kulipa faini kuanzia milioni tano na kuendelea, ili iwe fundisho kwa wengine" yaani, awe hana sababu mtu ya kuzuia mtu kwenda kutumia haki yake ya kidemokrasia ya kumchagua mtu anayemtaka. Mhe. Mwenyekiti, kwa fedha hizi pamoja na adhabu hizi hazitoshi, watu wataona hapa wanapeta na watatufanyia vituko hasa katika visiwa hivi vya Zanzibar wale wapinga maendeleo na mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, sheria ni msumeno. Kwahiyo, maelezo yake aliyosema Mhe. Mjumbe nakubaliana nayo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri umekubaliana na pendekezo la Mhe. Mjumbe ndio.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ndio nakubaliana nalo.

Kifungu 118-132 Pamoja na marekebisho yake

SURA YA SABA

Sehemu ya Kwanza

Masharti ya Fedha

Kifungu 133 - 134

Sehemu ya Pili

Masharti Mengineyo

Kifungu 135 - 145 Pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wetu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Uchaguzi, 2017

(Kusomwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Kufuata Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984 na Kutunga Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2017 na masuala mengine yanayohusiana na hayo usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Ahsante. Waheshimiwa Wajumbe, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa kuwasilisha mswada huu jana, pia nichukue fursa hii kukupongezeni sana kwa michango yenu na marekebisho mbalimbali ambayo mumeyafanya katika sheria hii, kwakweli hii ni sheria muhimu sana kwa Wazanzibari na bila ya shaka muda utakapofika tutakapoanza kuitumia, basi tutaona wenyewe matunda yake.

Waheshimiwa Wajumbe, kwakuwa shughuli zote ambazo zimepangwa kwa ajili ya siku ya leo zimekamilika pamoja na kwamba muda bado tunaona, basi naomba nichukue nafasi hii sasa kuahirisha shughuli za Baraza hadi kesho saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:10 usiku Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 14/12/2017 saa 3:00 asubuhi)